

TUJIFUNZE UISLAMU



TUJIFUNZE UISLAMU

KIDATO CHA TATU



© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

Jina la Asili:

Dinimi Öğreniyorum İslam - Orta 3 (Şafii)

Watunzi:

Faruk SALMAN
Nazif YILMAZ
Dr. Recep ÖZDİREK
Dr. Faruk KANGER

Mfasiri:

Zubeda Ally HUKA

Mhariri:

Jopo

Mratibu:

Mustafa DİRİER

M pangiliaji:

Hamza Daudi MSUYA

Kuhakikiwa kwa mujibu wa madhehebu ya imam Shafii:

Dr. Recep ÖZDİREK
Mehmet Şirin KIZILKAYA

Mchapishaji:

Rehema Friendship and Solidarity Trust.

Anuani:

Plot 80395 block D Mbezi Beach Tangibovu, Dar es salaam.

Simu:

+255 757 837 003

Barua pepe:

refso2010@gmail.com

Tovuti:

www.islamicpublishing.org

Mchapaji:

Erkam Printhouse

ISBN:

978-605-302-447-7

Istanbul - 2022 / 1443 H

Language: Swahili / Kiswahili



DIBAJI

Himidi zote ni za Mola wetu aliyetupa heshima na furaha ya kuishi kama Waislamu!

Salama nyingi zimuendee kipenzi chetu Mtume Muhammad (Rehma na amni ziwe juu yake), familia yake na maswahaba zake walioishi na kuufundisha Uislam kwa namna iliyokua bora kabisa!

Mtume wetu Mpendwa (Rehma na amani ziwe juu yake), alikuwa mwalimu adhimu kabisa aliyefundisha Uislamu kwa wanadamu. Kitabu alichofundisha ni Qur'an Tukufu, muujiza usiomithilika. Mtume huyo aliyebarikiwa, aliso-ma na kuifafanua Qur'an. Na alitekeleza imani, matendo ya ibada na maadili yaliyofundishwa na Qur'an kwa nam-na nzuri kabisa. Baada yake, Maswahaba, shakhsia adhimu kabisa wa Uislamu na watangulizi wetu walifanya juhudii kubwa katika kuitekeleza dini hii adhimu na kuipeleka kwa vizazi nya baadaye. Na sasa, ni zamu yetu kujifunza.

Kitabu cha "Tujifunze Uislamu" kimeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa ngazi ya chini ya sekondari. Kitabu hiki kina sura kuu nne.

Iliojumuisha sura kuu nne,

Sura ya kwanza ilitufundisha juu ya Imani yetu.

Sura ya pili ilituelekeza namna bora ya kufanya ibada.

Sura ya tatu ilifikisha vipande vipande kutoka katika maisha ya Mtume wetu Muhammad (Rehma na amani ziwe juu yake).

Na sura ya nne ilitufahamisha habari juu ya tabia njema ambazo muislam anatakiwa kuwa nazo.

Ni matumaini yetu kuwa tunaweza kujifunza dini yetu nzuri kwa namna bora kabisa, na kuwa mionganii mwa Waislamu ambao Mtume aliyebarikiwa atatabasamu pindi atakapowaona huko Akhera.

Tunamuomba Allah aijaze imani katika nyoyo zenu, aujaze Uislamu katika maisha yenu, na roho zenu azijaze usafi wa moyo. Malaika wasuhubiane nanyi, na watu wema wawe marafiki zenu!

Tunamuomba Allah Mtukufu awapende na kuwasaidia!

Tunamuomba aifanye njia ya maisha yenu iwakeleke Peponi

Hivyo kwa jina la Allah:

رَبِّ يَسِّرْ وَ لَا تُعَسِّرْ رَبِّ تَمْ بِالْخَيْرِ

"Mola wangu, yafanye kuwa mepesi, usiyafanye kuwa mazito, na uyahitimishe kwa kheri".

YALIYOMO

MUONGOZO WETU KATIKA MAISHA: IMANI KATIKA VITABU VYA MWENYEZI MUNGU / 9

Hadithi: JIVIKE MBAWA ZAKO ZA HISIA	10
Watu wanahitaji Wahyi	13
Vitabu Vitukufu	14
Taurat	15
Zaburi ya Daudi	15
Injili	16
Qur'an Tukufu	16
Vitu tunavyovipata kwa kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu	17
Tukijue kitabu chetu kitukufu	20
Wahyi wa kwanza	21
Kuandika Qur'an Tukufu na kuihifadhi	23
Kuikusanya Qur'an Tukufu katika mfumo wa kitabu	23
Kuinakilisha Qur'an Tukufu	24
Faida za kusoma Qur'an Tukufu	25
Yaliyomo Ndani Qur'an	26
Mtume wetu na Qur'an Tukufu	30
MASWALI	33

WATU WA MIFANO: IMANI JUU YA MITUME / 37

Hadithi: MITUME (WAJUMBE WA MWENYEZI MUNGU)	38
Muongozo wetu	43
Mitume na sifa za mitume	44
Ujumbe wa Kufanana wa mitume Wote	46
Vitu tunavyovipata kwa kuamini mitume ma Mwenyezi Mungu	47
Mifano bora kwetu inapatikana katika maisha ya mitume	50
Adam (Amani iwe juu yake)	50
Nuhu (Amani iwe juu yake)	51
Ibrahim (Amani iwe juu yake)	52

Yusuf (Amani iwe juu yake)	53
Mussa (Amani iwe juu yake)	54
Yesu/Issa (Amani iwe juu yake)	56
Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake).....	57
Mtume wetu katika wahyi wa mitume wengine	60
MASWALI	63

**MSIMU WA REHMA NA IBADA:
RAMADHANI NA KUFUNGA / 67**

Hadithi: FUNGA YA KWANZA	68
Funga ni nini?.....	71
Juu Ya Nani Funga Ni Lazima/Faradhi?.....	71
Ni masharti gani muhimu kwa funga zetu kukubalika?.....	71
Baadhi ya masuala yanayohusiana na Ramadhani	72
Funga Inatulinda Sisi.....	74
Faida za funga	75
Aina za funga	77
Funga ya Qadha	80
Funga ya marekebisho (Kaffara).....	80
Matendo yanayobatilisha funga	81
Matendo ambayo hayabatilishi funga	83
Mambo Yapi Humfanya Mtu Asilazimike Kufunga?	84
Kiasi Kinachotolewa Kwa Masikini Mwishoni Mwa Mwezi Wa Ramadhani (Zakat al-fitr).....	85
Funga Ya Kutia Nadhiri	85
Swala ya Taraweh	86
Mafunzo ya kiroho	86
Usiku wa cheo (Lailat al-Qadir).....	87
Sherehe ya kumaliza mwezi wa Ramadhani (Eid al-fitr).....	88
Maisha ya Mtume Katika Kipindi Cha Ramadhani	89
Shairi: RAMADHANI	92
MASWALI	93

DARAJA BAINA YA MATAJIRI NA MASIKINI: ZAKA / 95

Hadithi: JARIBIO LA SHUKRANI	96
Nani ni mmiliki halisi wa mali zetu?	98
Sadaka na zaka	99
Zaka ni nini?	101
Faida za zaka	102
Hadithi: JE, YUPO MWINGINE ANAYETOA ZAIDI!	106
Nani anayewajibika kutoa Zaka?	108
Ni kipimo gani cha kuwa na tajiri kwa katika Uislam?	108
Yapi ni mahitaji ya lazima?	108
Ni kiwango cha Nisab (kiwango cha kulipwa zaka) na kiasi cha zaka	109
Kiwango cha Nisab na kiasi cha zaka kwa wafanyabiashara	109
Kiwango cha Nisab na kiasi cha zaka kwa wanyama	110
Kiwango cha Nisab na kiasi cha zaka kwa mazao	111
Hadithi: BUSTANI ILIYOHARIKBIKA	112
Ni nani anayestahili kupewa Zaka?	114
Ni nani asiyestahili kupewa Zaka?	115
Hadithi: KUTOA KATIKA VITU TUNAVYOVIPENDA	116
Kipi tunatakiwa kuzingatia tunapotoa zaka?	117
Kutafuta maisha kwa kufanya kazi za mikono ni bora zaidi kuliko kuomba	119
Ukarimu na utu wa Bwana Mtume (s.a.w)	120
Shairi: MBINGU NANE ZIKO TAYARI	122
MASWALI	123

NINAJIFUNZA KUHUSU MTUME WANGU: SIRA / 125


1- VITA YA UHUD (MWAKA 625)	126
a) Washirikina wakiugulia kwa matamanio ya kulipiza kisasi	126
b) Adui alipokua anakaribia	127
c) Usaliti wa wanafiq	127
d) Wapiga upinde walivunja amri ya Mtume	128
e) Kuuwawa kwa mjomba wake Mtume, Hamza (r.a)	129
f) Je, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuwawa?	130

2- TUKIO LA RAJI NA MAAFA YA KISIMA CHA MAUNAH (MWAKA 625)	131
a) Walimu waliojitoa kufundisha uislam.....	131
b) Usaliti mmoja baada ya mwininge.....	133
3- POMBE NA KAMARI: MATENDO YA SHETANI	134
Hadithi: ALIDHALILISHWA!	135
4- KIJANA ALIYEFANYA UTAFITI KUHUSU UCHAGUZI WA MTUME WA MWISHO	136
a) Tulikuwa tukiabudu moto.....	136
b) Nilishangazwa	136
c) Njiani kuelekea Damascus.....	137
d) Katika uchaguzi wa Mtume wa mwisho	138
e) Habari za Mtume wa mwisho.....	139
5- NGUO INAYOKINGA KUTOKANA NA AIBU NA MADHAMBI	140
6- VITA YA HANDAQ (MWAKA 627)	141
a) Angamizo kwa waislam	141
b) Mahandaki yanajengwa	141
c) Siku ngumu	143
d) Mwisho wa kuzingira	144
7- SULUHU YA HUDAYBBIYAH (MWAKA 628)	146
a) Waislam walikua wanaihitaji sana Ka'bah.....	146
b) Hofu ya watu wa Makkah.....	146
c) Mazungumzo ya Amani.....	147
d) Utii wa Ridwan	148
e) Kusainiwa kwa makubaliano ya suluhu	148
f) Tukio la kuhuzunisha.....	149
Hadithi: UFUNGUO WA KWENDA MBINGUNI	150
8- KWATUMA WAWAKILISHI NA BARUA ZA MWALIKO WA UISLAM (MWAKA 628/629)	151
a) Kumualika mtawala wa Byzantine Heraclius katika Uislam	152
b) Kumualika mfalme wa Persia Husraw Parwiz katika Uislam.....	153
c) Kwa Najashi Ashama, mfalme wa Abyssinia	153
9- USHINDI WA KHAIBAR (MWAKA 628)	154
a) Wayahudi wa khaibar wanataka kupigana.....	154
b) Ngome za Khaibar zinashindwa.....	154
c) Njama ya kumuuuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kisasi.....	156

10- MWAKA MMOJA BAADYE WALITEMBELEA KA'BAH (MWAKA 629)	157
11- VITA YA MUTAH (MWAKA 629)	159
a) Pindi mjambe wa Mtume alipokufa kwa kuulingania Uislamu	159
b) Nguvu ya maadui na hamasa waliyokua nayo waislam	160
c) Zamu ya kuheshimika kwa kuuawa mashahidi	161
Hadithi: MAYATIMA WA JA'FAR	163
MASWALI	164

**TABIA ZINAZOMFANYA MTU KUWA MUISLAM MZURI:
ADABU / 171**

1. ADABU KATIKA UDUGU	172
Hadithi: HADITHI YA TENDO	175
2. KUONYESHA HESHIMA KWA WAKUBWA	176
Hadithi: IKIWA TU WAMECHUKUA SOMO	179
3. ADABU YA KUINGIA NA KUTOKA NYUMBA	180
Hadithi: NI LAZIMA KUOMBA RUHUSA	181
4. ADABU YA KUPOKEA NA KUTOA ZAWADI	183
Hadithi: SHATI MOJA	185
MAJIBU	186



MUONGOZO WETU KATIKA MAISHA:

IMANI KATIKA VITABU VYA MWENYEZI MUNGU.



❖ *Watu wanahitaji wahyi*

❖ *Vitabu vitukufu*

❖ *Vitu tunavyovipata kwa kuaimini
vitabu vya Mwenyezi Mungu*

❖ *Kitabu chetu (Qur'an Tukufu)*

❖ *Mtume wetu na Qur'an tukufu*



JIVIKE MBAWA ZAKO ZA HISIA

Bakr alimkabili baba yake ambaye alikua anasoma Qur'an. Akainyooshea kidole Qur'an tukufu, kisha akamuuliza baba yake:


"Baba! Nafahamu Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu, lakini nahitaji kufahamu Zaidi kuhusiana na kitabu hiki. Je, waweza kuniambia Zaidi kuhusiana na Qur'an?"

Baba yake alifurahi sana kusikia ombi la Bakr. Hivyo akaanza kumuelezea:

"Mwanangu, Qur'an tukufu ni kitabu kitukufu kwa waislam. Mwenyezi Mungu amekua akituma vitabu vitukufu kwa watu kwa nyakati tofauti tofauti. Kwa namna hii, aliwafahamisha kuhusu yale aliyokua akiyahitaji na yapi alikua akiyatara jaria kutoka kwao. Muda mrefu umepita na vitabu hivyo vimekua vikipotea. Ndipo watu wakaanza kuishi maisha ya upotevu juu ya amri za Mwenyezi Mungu. Mara zote muumba wetu mtukufu hututakia kheri waja wake, Ndio maana akituma kitabu kipyta kwa Mjumbe mpya. Utaratibu huu ulikua endelevu. Na Qur'an tukufu ni kitabu cha mwisho kushushwa. Ameeleza katika Qur'an ya kwamba hatatuma tena kitabu kingine baada ya hiki.

— Baba, kwahiyo Qur'an ni kitabu cha kila mmoja, sivyo?

— Vizuri mwanangu! Qur'an tukufu ni kitabu ambacho watu wote kutoka zama za Mtume wetu Muhammad (Rehma na amani ziwe juu yake) hadi siku ya mwisho wanatakiwa wakiamini na kukifuata.



— Baba, je kuna maneno yoyote ya Mtume wetu ndani ya Qur'an?

— Hapana, mwanangu mpPENDWA. Yapo maneno ya Mwenyezi Mungu katika Qur'an tukufu. Je, unafahamu alivyokua makini Mtume wetu Muhammad(Rehma na amani ziwe juu yake) katika kuyaweka maneno yake nje ya Qur'an?

Kipindi cha mwanzo cha Uislam Mtume wetu alikua anapinga vikali maneno yake yasiandikwe. Hivyo basi aliwataka maswahaba zake kuchana maandiko yote yaliyomuhusu. Baada ya hatari ile ya kuchanganya maneno yake na aya za Qur'an kupita ndipo aliwaruhusu kuandika maneno yake walipohitaji kufanya hivyo.

— Baba! Nashangaa ni jinsi gani Mtume(Rehma na amani ziwe juu yake) alikua akipokea Qur'an.

— Kuna malaika ambaye anachukua maamrisha ya Mwenyezi Mungu na kuyapeleka kwa mitume. Jina lake ni Jibril. Jibril aliteremsha Qur'an kwa Mtume wetu.

— Ni kwa namna gani Jibril alishusha Qur'an? Na hakika aliteremsha kwa mpangilio mzuri.

— Hapana kijana wangu mpPENDWA. Qur'an Tukufu haikushushwa kama kitabu kilichoandikwa tayari. Ilishwa kwa njia maalumu iliyoitwa wahyi.

— Baba, wahyi ni nini?

— Wahyi maana yake ni kuongea kwa siri tena kwa kunong'ona. Ilikua ni njia aliyoitumia malaika Jibril kufikisha maamrisha ya Allah kwa

Mtume wetu. Malaika Jibril alikua akizisema aya za Qur'an alizokuja nazo kwa Mtume wetu. Kisha Mtume wetu alikua na maswahaba zake wakizandika na kuzihifadhi aya hizo.

— "Baba! Natamani ningezaliwa kipindi cha kipenzi chetu Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake). Natamani ningeona jinsi Qur'an Tukufu ilivyokua ikiteremshwa. Natamani tungepata wasaa wa kuitizama sura nzuri ya bwana Mtume na kusikiliza Qur'an toka katika kinywa chake."

— "Unaweza ukajaribu kuweka mbawa za hisia na kupaa hadi katika zama hizo. Unasemaje kuhusu hilo. Je, uko tayari kwa safari hiyo?"

— "Ndiyo baba nipo tayari."

— Sawa, twende.

kituo chetu cha kwanza ni Madina. Tunakwenda kuona mji wa Bwana Mtume. Fumba macho yako.

Tumefika sasa waweza kufumbua macho yako. Huu ni mji wa Madina.

Tumtafute Mtume wetu. Sidhani kama tutapata tatizo katika kumtafuta yeye, kwani mara kwa mara hutumia muda wake mwingu akiwa msikitini kwake. Tutizame hapo kwanza.

Ndiyo, yuko pale. Tizama! Aliyekaa katikati ya umati ule ni Mtume wetu Muhammad. Je, hujamtambua? Tizama! Ni yule mwenye uso wenye kung'ara na macho meusi. Kichwa chake ni kikubwa kiasi na nyusi zake zimepangika mithili ya mwezi mchanga. Alikua ana ndeu nzito na nywele za singasinga. Ngozi yake ulikua laini na mwli wake ulikua umejenjeka vizuri sana. Umeweza kumtambua sasa, sivyo? Huyu ndiye Mtume wetu.

Tupo ndani ya wakati. Ulikua ukishangaa ni namna gani Mtume wetu alikua akipokea wahyi. Nadhani tunakwenda kushuhudia wote pamoja.

Tizama! Uso wa bwana Mtume unaanza kufilia mng'ao wake wa asili. Je, unaona matone ya jasho katika paji lake la uso? Kila mtu yupo kimya. Macho yanatizama ardhini.

Hapo ina maana malaika Jibril (Amani iwe juu yake) anateremsha amri mpya toka kwa Mwenyezi Mungu. Ndio maana Mtume wetu anaonekana kuchoka na kupotelewa na fahamu.

Tizama amefumbua macho yake. Macho yanang'aa. Uso wake umewaka kutohakana na nuru ya wahyi mpya.

Tizama marafiki wa Mtume wetu. Kama unavyojua tunawaita wafuasi au maswahaba.



Maswahaba wanahamu ya kutaka kufahamu amri mpya toka Mwenyezi Mungu ni ipi. Wanashauku kusubiri kusikia ni kipi Bwana Mtume atakwenda kukisema. Tizama anaanza kuongea:

— Mwenyezi Mungu Mtukufu ameteremsha aya mpya. Wahyi huu unapaswa kuandikwa aya hii katika Surat Al-Baqara. Ninasoma taratibu. Sikiliza kwa makini. Jifunze kisha ukawafundishe wale ambao hawajafika hapa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Sio uchamungu kwa kugeuza nyuso zenu mashariki na magharibi, ila mchamungu wa kweli ni yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na malaika na vitabu na mitume na akatoa katika mali zake kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa watu wake wa karibu na mayatima na wenye uhitaji na wasafiri na ombo ombo na kuwaachia huru mateka, na kudumisha swala na kuwasaidia masikini na kutimiza ahadi zao wanapoahidi,

Na wale wenye subra kipindi cha mfadhaiko na mateso na kipindi cha magomvi.

— Hawa ni watu ambao ni wakweli (katika nafsi zao) na hawa ni watu ambao wanajiongoza(wenyewe kutokana na uovu). (Baqara 2: 177)*

— Umeona mwanangu punde tu baada ya Mtume Muhammad (Rehma na amani ziwe juu yake) kupokea wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu alizifundisha kwa maswahaba zake na kuwataka waziandike aya hizo. Baada ya Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) kuondoka, maswahaba huzisoma aya hizo, huzihifadhi kisha kuwafundisha wale ambao hawakuzisikia.

— Asante baba kwa safari hii ya kufikirika. Nimejisikia kama kweli niliishi katika zama zile. Vema, ni kwa muda gani Mtume wetu alitumia kupokea Qur'an nzima kwa ukamilifu wake?

— Wahyi wa kwanza ulishuka Mwaka 610 Makka. Baada ya hapo wahyi uliendelee kuteremka kwa miaka 13 huko Makka, na miaka 10 huko Madina, jumla ya miaka 23.

— Baba! Sihatiji tena uendelee kunisomea Qur'an Tukufu, ila nina swalii moja la mwisho. Kwanini Mwenyezi Mungu hakutiteremsha Qur'an yote kwa wakati mmoja na akaifanya kwa kipindi cha miaka hiyo 23?

— Kuwapa waislamu nafasi ya kujifunza vizuri na kujifunza kwa urahisi zaidi. Endapo ingeteremshwa kwa wakati mmoja, ingekua vigumu kuiandika na kujifunza. Ndio maana Qur'an ilishushwa vipande vipande pindi ambapo tukio Fulani lilitokea ama swalii kuulizwa. Hivyo waumini walizipata aya mpya kwenye mioyo yao walizifuata katika maisha yao na kuzilinda ili zisibadilishwe.

Sasa hivi ni wakati wetu mwanangu. tutaisoma Qur'an na kujifunza maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Tutapokea ushauri wake. Tutaishi kwa kuzingatia muongozo wa dini yetu na kuifikisha Qur'an kwa vizazi vijavyo.

Bakr sasa alifahamu kwanini baba yake anachukulia jambo la kusoma Qur'an kama jambo la muhimu sana. Ni sababu Qur'an ni ujumbe toka kwa Mwenyezi Mungu ni kitabu ambacho kinapaswa kusomwa kwa mazingatio, kuelewa na kuiishi katika maisha yetu.

M. Yaşar Kandemir

(imenakiliwa kwa matoleo mapya)

Kutoka sasa na kuendelea endapo patahitajika kurejea aya katika Qur'an tutasema kidogo kuhusu sura hiyo, kisha nambari ya sura na mwisho nambari ya aya.

WATU WANAHITAJI WAHYI

Macho yetu ni moja kati ya kiungo muhimu sana katika viungo vya mili yetu. Tunaona na kukusanya taarifa za vitu vinavyotuzunguka kwa kutumia macho yetu. Lakini macho yetu yana mipaka miwili. Kwanza macho yetu yanahitaji mwanga kuona vitu. Hatuwezi kuviona tukikosa mwanga. Jambo la pili ni kwamba macho yetu haya na uwezo wa kuona kila kitu. Hatuwezi kuona vitu vingi vidogo sana kwa mfano, virusi au atomi kwa macho yetu haya. Tunaweza kupata msaada kupiditia vifaa kama vile darubini ili tuweze kuona vitu hivyo.

Ufahamu wetu ni jambo la msingi sana ambalo linatufanya tuwe tofauti na viumbe wengine. Kwa ufahamu wetu tunaweza kutambua na kutenganisha kati ya mabaya na mema. Tunaweza kuutumia pia ufahamu wetu katika kuchanganua lenye madhara na lile lisokua na madhara. Japokua, mithili ya macho yetu, fahamu zetu pia zina mipaka. Ufahamu wetu pekee hautoshi kutofautisha kati ya sahihi na lisilo sahihi, au chenye faida na chenye madhara. Ni kama tunavyohitaji mwanga wa kawaida ili tupate kuona, tunahitaji pia kupata mwanga wa wahyi ili tuweze kutumia fahamu zetu kwa usahihi Zaidi. Hivyo hivyo tunahitaji pia wahyi katika masuala kama maisha baada ya kifo, moto na pepo ambavyo hatuwezi kuvielewa kwa kuijiliza maswali tu.

Mola wetu Mtukufu ametuunganisha sisi kupiditia vitabu na mitume wake aliowatuma. Toka kipindi cha Nabii Adam (Amani iwe juu yake), mitume wote wametuletea maneno na ujembe toka kwa Mwenyezi Mungu. Ujumbe huu na maneno hayo aliyoysteremsha Mwenyezi Mungu yanaitwa wahyi..

Wahyi uloshushwa na Mwenyezi Mungu ni mwanga unaoonesha nija iliyonyooka kwa fahamu zetu na mwangaza wa njia katika mai-sha. Tunaweza tukamfahamu sasa Muumba wetu na dhumiuni letu la kuumbwa. tunaweza pia tukapata msaada kutoka katika muongozo wa wahyi na kupata majibu ya maswali kama:

- ❖ Nini maana ya maisha?
- ❖ Ni kwa namna gani maamrisho katika maisha yetu yanapaswa kua?
- ❖ Ni zipi kazi zetu na majukumu yetu juu ya Mwenyezi Mungu?
- ❖ Ni kipi kitatokea katika maisha yetu baada ya kifo?
- ❖ Je, kuna ufufuo baada ya kifo?
- ❖ Wapi na namna gani tunaweza kuona matokeo ya matendo yetu katika ulimwengu huu?



VITABU VITUKUFU



Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“...Na wale wanaoamini wahyi ulioteremshwa kwao, na kabla yao...”

(al-Baqara 2; 4)

Moja ya katika nguzo za imani ya kiiislam ni kuamini ya kwamba kuna vitabu vilivyoteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na ya kuwa kila ujumbe katika vitabu hivi umetoka kwake.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha ujumbe wake kwa mitume wake aidha moja kwa moja au kwa kupitia malaika wake. Mitume walikua wakiwafikishia watu wao wahyi wanaoupokea. Vitabu vimejumuisha maamrisho, makatazo na ushauri wa Mola wetu Mtukufu vinaitwa “Vitabu vitukufu”. Tunajifunza nguzo za Imani, sheria zinazohusiana na kufanya ibada na namna gani tunapaswa kuishi katika ulimwengu huu kwa kizingatia vitabu hivyo. Tunatii utaratibu katika vitabu hivi na tunajaribu kuyapata mapenzi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa kategemea mahitaji ya watu, Mola wetu Mtukufu aliteremsha vitabu vidogo kwa baadho ya mitume wake vilivyokua na karatasi chache (Suhuf) na baadhi ya mitume wake vi-

tabu vilivyosheheni mambo. Pemberi ya kuirasa hizi, vitabu vine viliteremshwa kwa mitume wane. Vitabu hivi ni:

Vitabu vidogo vilikua na kurasa mia moja jumla yake navyo ni:

Kurasa kumi kwa Nabii Adam(Amani iwe juu yake),

Kurasa hamsini kwa Seth(Amani iwe juu yake),

Kurasa thelathini kwa Idris(Amani iwe juu yake),

Na kurasa kumi kwa Nabii Ibrahim(Amani iwe juu yake)

TAURAT:

Kiliteremshwa kwa Nabii Mussa(Amani iwe juu yake). Qur'an tukufu inat-ueleza taurati ni moja ya kitabu kitukufu kilichoteremshwa ili kuwaongoza watu katika njia iliyonyooka. Ndio maana waislam tunaamini kua taurati halisi kikua ni kitabu kilichobeba maneno ya Mwenyezi Mungu

Taurati iliteremshwa kwa wana wa Israel kupitia Nabii Mussa(Amani iwe juu yake) ingawa wana wa Israel au wayahudi hawakuweza kukiliinda kama kilivoshushwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nakala halisi ya taurati ilipotea. Ilikuja kuandikwa tena na msomi mmoja wa kiyahudi baada ya muda mrefu kupita.

Hata hivyo taurati halisi iliteremshwa kwa nabii Mussa (Amani iwe juu yake) na Mwenyezi Mungu Mtukufu ilikuja kuin-gia hitilafu nyingi ndani yake. Hata hivyo muda ulipokua ukipita watu walikibadili-sha. Kwa sababu ya hitilafu hizi, Taurati iliyopo leo hii imepoteza kabisa thamani yake ya kua kitabu kitukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na wale kabla ya hii (Qur'an), kulikua na kitabu cha Mussa kama muon-gozo na rehma..."

(Ahqaf 46; 12)

ZABURI YA DAUDI

Ilishushwa kwa Nabii Daudi(Amani iwe juu yake). kwa kua Daudi (A.S) alikua na sauti nzuri sana alipokua akisoma zaburi, kila mmoja aliyemsikiliza alipata athari ya hali ya juu sana. Leo hii kitabu cha zaburi kimekua ni sehemu katika Agano la Kale. Na namna yake ya sasa,

zaburi ni kitabu cha ushauri kilicho-andikwa kwa mtindo wa mashairi na hakijabeba maamrisha wala makatazo yoyote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"...Tuliwapendelea baaadhi ya mitume juu yao, na kwa Daudi tulimpa Zaburi."

(al-Isra 17; 55)

INJILI

Ni kitabu kilichoteremshwa kwa nabii Issa (Yesu) (Amani iwe juu yake)

Injili halisi iliteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ingawa, kama iliviyoka kwa Taurati na Zaburi iliingia hitilafu za kibinadamu. Injili haikua imerekodiwa mahali popote katika kipindi cha nabii Issa (Amani iwe juu yake), lakini baada ya kupoza kwakwe mbinguni nakala tofauti tofauti za injili zilandikwa. Katika baraza la kwanza la Nicaea lilikusanyika mwaka 325, baraza la maaskofu wa kikristo lilichagua ijili nne kama injili kuu. Zilandikwa na Maiko, Mathayo, Yohana na Luka na

hivyo zilikua na zilijulikana kwa majina ya waandishi wake. Hizi ndizo injili tulizanazo leo hii.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“...Tulimteremshia Issa (Yesu) injili, ndani yake palikua na muongozo na nuru, na kuthibitika kwa sheria zilizokua kabla yake uongofu na mawaidha kwa wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungullah.”

(al-Maidah 5; 46)

QUR'AN TUKUFU

Ni kitabu kitukufu cha mwisho kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kiliteremshwa kwa kipenzi chetu Mtume Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake). Baadhi ya vitabu vitukufu vimepotea na baadhi yake vimeengizwa hitilafu na binadamu. Lakini Mola wetu Mtukufu ametutumia ujumbe na mafundisho vyote kwa pamoja na yale yaliyopita katika vitabu vilivytangulia kuptilia Qur'an Tukufu.

Tunapaswa kuamini kua ni Qur'an Tukufu pekee ndicho kitabu mionganoni mwa vitabu kilichoteremshwa kwetu katika uhali-sia wake na hakijabadilika namna yake na asili yake). Baadhi ya vitabu vitukufu vimepotea na baadhi yake vimeengizwa hitilafu na binadamu. Lakini Mola wetu Mtukufu ametutumia ujumbe na mafundisho vyote

kwa pamoja nay ale yaliyopita katika vitabu vilivytangulia kuptilia Qur'an Tukufu. Sisi kama waislam tunatkiwa kuamini katika vitabu halisi vilivyopita ambavyo havikua na hitilafu yoyote na si matoleo haya ya sasa. Tunaamini vitabu vyote vitukufu vilivyoteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Kwa hakika tumeteremsha ukumbusho (Qur'an) na hakika tutakua ni wenye kuilinda

(Hijr 15; 9)

VITU TUNAVYOVIPATA KWA KUAMINI VITABU VYA MWENYEZI MUNGU

VITABU VITUKUFU

- Inatupa nafasi ya kuendelea kuwasiliana na Mola wetu Mtukufu.
- Inatufundisha dhamira yetu ya kuletwa duniani na majukumu yetu katika ulimwengu huu.
- Inalinda sheria za dini yetu kwa ujumla kutohana na kubadilikabadiili na kuingizwa hitilafu.
- Inaelezea vipindi muhimu katika historia ya binadamu ili kukifanya kizazi kijacho kupata somo kutoka kwao.

Hua tunarudiarudia kusoma sentensi za barua zinazotufikia kutoka kwa wapendwa wetu. Hua hatusahau baadhi ya sentensi kwa kipindi chote cha maisha yetu. Vitabu vitukufu vinavyobeba maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kama barua zilizotumwa kwetu binadam. Ni barua kubwa kabisa itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa ulimwengu, na kila neno moja linabeba idadi ya uzuri na hekma. Tunaposoma ni kama tupo katika mazungumzo na Mola wetu. Mara zote tunaposoma au kusikiliza maneno haya matukufu yanayokuja kutoka kwa **asiyekua na mwisho** huathiri nafsi zetu. Huongeza mahaba kwa Mola wetu Mtukufu. Hivyo **hutupa nafasi kuendelea kuwasiliana na Mola wetu Mtukufu**.

Kipenzi chetu Mtume Muhammad amesema:

Ninawaachia vitu viwili muhimu sana, kimoja wapo ni kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hiyo ni Kamba ya Allah. Yule atakayeikamata sawasawa atakua katika uongofu wa kweli na yule atakaye-iachilia atakua katika upoteve ulio Dhahiri" (rehma na Amani ziwe juu yake)

(Muslim, Fada'il al-Sahaba, 37)



Vitabu vitakatifu vinatuelekeza kuhusu amri na makatazo yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vinatu-fundisha juu ya malengo yetu ya kuletwa ulimwenguni na majukumu yetu katika dunia hii. Vinatu-amrisha kumuabudu Mwenyezi mungu mmoja tu na kuwachukulia mitume wake kama vigezo katika maisha yetu. Vinatushauri kufanya vitu ambavyo vina faida kwa wengine. Vinatutia moyo jinsi ya kuwa waja wema, kutenda haki na kuwasidia wenyehi maaadili mema.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hii (Qur'an) ni ujumbe ulio wazi kwa watu ili wapate kuonyeka kwayo, na wapate kujua kua Mwenyezi Mungu ni Mola mmoja, kisha wale wenye kuelewa wapate mazingatio."

(Ibrahim 14; 52)



Makala ya Imani hujumuisha misingi wa dini. Pale nakala halisi za vitabu vitukufu viliviyotuelekeza kanuni, vilipata uharibifu ndipo watu wakaanza kupotea katika Imani potofu. Walianza kwenda mbali kutoka katika Imani ya kumuamini Mungu mmoja. Wakaanza kuchukulia mambo yaliyokatazwa kuwa halali na yaliyokua halali kuyabatilisha. Ndipo Mwenyezi ungu Mtukufu akatuma tena ujumbe mwagine kuuhuisha ule uliopata uharibifu. Aliwfundisha watu Imani ya kweli na tabia njema kwa mara nyingine. Kwa namna hii vitabu vitukufu viliviyoteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu **vinakinga kanuni za dini yetu**

kutokana na kubadilika na uharibi-

fu. Qur'an Tukufu ni kitabu cha mwisho kuteremshwa na Mola

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Amaekuteremshia kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokua kabla yake, na aliteremsha Taurati na Injili kama muongozo kwa watu."

(Al-i Imran 3; 3)

wetu Mtukufu. Imejumuisha uzuri na ukweli wote wa vitabu vitukufu viliviyotangulia. Safari ya maisha ya binadamu ilianzia kwa Nabii Adam(Amani iwe juu yake). Toka hapo ustaarabu mbalimbali umekua ukigundulika na watu. Wale ambaao walifuata nyendo za mitume na kfanya matendo mema mara zote wamekua wakikumbukwa kwa shukrani. Wamekua mifano kwa vizazi vijazo, kisha wale ambaao hawakuukubali muongozo wa mitume na vitabu vitukufu viliviyotumika hapa duniani ila tu kwa faida yao wenyewe. Waliwakandamiza wanyonge na kutowatendea haki. Waliwaua watu wasiokua na hatia. Walitumia mali zao kwa madhumuni mabaya, na walijitenga na rehma za Mwenyezi Mungu. Waliacha alama mbaya sana na wakafutwa katika vitabu vya historia. Kwa hiyo vitabu vitukufu vilielezea kipindi hicho muhimu katika historia ya binadamu ili vizazi vijavyo vipate mafunzo.



Mwili wa firauni aliyejukufa akiwa anavuka katika bahari ya shamu, umetunzwa kwa karne nyingi.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na katika hadithi zao limo zingatio kwa wenyewe akili. Si maneno yenye kuzuliwa, bali ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufanuzi wa kila kitu, na ni uongofu na rehma kwa kaumu yenye kuamini."

(Yusuf 12; 111)



Mapiramidi ni makaburi ya mafaraao kwa misri.

TUKIJUE KITABU CHETU KITUKUFU

M pangilio wa ndani wa Qur'an Tukufu

Qur'an Tukufu ni kitabu kitakatifu chenye maajabu ambacho hakiwezi kuzalishwa na binadam. Kinaitwa "kalamullah" inamaanisha maneno ya Mwenyezi Mungu. Kupitia Malaika Jibril, iliteremshwa kwa kipenzi chetu Mtume Muhammad(rehma na Amani ziwe juu yake) vipande vipande kwa miaka 23. Inajumuisha kurasa 600.


Ndani yake kuna mpangilio maalum unaouna aya, sura na sehemu. Aya za Qur'an, ambazo kwa kiarabu zinaitwa "ayat" inahusisha sentensi moja au Zaidi ya moja. Vipande vya aya vinaunda sura za Qur'an. Kuna sura 114 katika Qur'an Tukufu. Kila sura ina jina lake la kipekee na kila namba za aya zinatofautiana kati ya sura moja na nyingine.

Sura hazijapangwa kutohana na ziliyaoanza kuteremka mwanzo isipokua kama ambavyo

Mwenyezi Mungu alivyotaka zipangike. Sura ndefu kuliko zote ni surat Al-Baqara ambayo ni sura ya pili kwa mpangilio katika qur'an na ina jumla ya aya 286, hali ya kua sura fupi Zaidi kuliko zote ni surat Al-Kawthar ambayo ni sura ya 108 katika mpangilio wa Qur'an yenye jumla ya aya tatu pekee. Qur'an Tukufu inaanza na surat Al-Fatiha na inaishia na surat Al-Nas.

Kila kipande chenye kurasa 20 za Qur'an kinaitwa "juzuu" au sehemu. Kuna jumla ya juzuu 30 katika qur'an. Kuigawanya Qur'an kunafanya iwe rahisi kuhifadhi na kuisoma.

Qur'an tukufu imeteremshwa kwa lugha ya kiarabu. Ndio maana imetafasiriwa kwa lugha mbalimbali ili kuwasaidia watu ambao hawaelewi kiarabu. Ufasiri huo kwa lugha tofauti tofauti unaitwa pia maana ya Qur'an(maal). Tunaweza kusoma na kujifunza maelekezo kwa undani Zaidi na maoni ya aya katika vitabu vya maoni vya qur'an (Tafseer).



WAHYI WA KWANZA

Mtume wetu Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) alifahamika kwa tabia zake njema katika jamii yake. Hakuwahi kuabudia masanamu na hakuwahi kula nyama iliyotokana na sadaka kwa ajili ya masanamu. Hakuwahi kunywa pombe au ulevi wowote. Hakuwahi kuhudhuria katika hafla na sherehe yoyote iliyofanyika kwa ajili ya masanamu. Alisifiwa na kila mtu na aliaminiwa kwa ukweli wake, uaminifu wake, kujidhatiti katika ahadi zake, haya, ukarimu na heshima yake.


Muhammad(rehma na Amani ziwe juu yake) alikua akifuata dini ya babu yake Ibrahim Hanif aliamini katika Mungu mmoja. Alipofikisha umri wa miaka 40, alianza kupata ndoto za kweli. Kila alichokiota katika ndoto hutokea kweli. Usiku mmoja(usiku wa Qadir) majira ya kupambazuka alfajir katika mwezi wa Ramadhan mwaka 610 alipokua katika pango la Hira, Malaika Jibril alimjia Mtume wetu(rehma na Amani ziwe juu yake). Malaika akamwambia:

"Soma!" Mtume wetu(rehma na Amani ziwe juu yake) kwa hofu ya hali ya juu akajibu:

"Sijui namna ya kusoma" Jibril akamwambia tena:

"Soma" Muitikio wa Mtume wetu uliku uleule:

"Sijui namna ya kusoma"



Malaika Jibril alimtaka tena asome kisha akamsomea aya tano za mwanzo za surat Al-alaq. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alizirudia aya hizi za mwanzo za Qur'an. Hapa chini ni maana ya aya hizi tano:

"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba. Amememuumba binadamu kwa tone la damu. Soma! Na Mola wako mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha binadamu aliyokua hayajui." (al-Alaq 96; 1-5)

Baada ya kurudia maneno ya Malaika aloyeteremsha wahyi, Mtume wetu alisimama juu. Alikua anashangaa na kutetemeka kwa hofu. Aliondoka pangoni. Mara hii sauti ile ile ilikua inasikika kutoka mbinguni. Sauti nzito ya malaika Jibril(Amani iwe juu yake) ilisikika kila mahali:

"Eeeh Muhammad wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mimi ni malaika Jibril."

Baada ya tukio hili Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake)alizidi kuogopa alishuka mlimani huku mapigo ya moyo yakiwa kasi sana, hadi pale alipofika kwa mkewe bi Khadija. Mama yetu bi Khadija akapata hofu kwa vile Bwana alivyokua

amechanganyikiwa. Mtume alikua bado anatetemeka. Alikwenda kitandani kwake na kusema, "Nifunike! Nifunike!" punde usingizi ukamchukua na alipoamka alimuhadithia kile kilichotokea. Mama yetu Bi. Khadija alimfariji na kumwambia:

"Usiwe na hofu! Mwenyezi Mungu hataweza kukaibisha. Unathamini mipaka ya udugu, unaongea ukweli, unasaidia masikini na mafukara, unawahudumia kwa ukarimu na kuwasaidia wale waliokumbwa na majanga. Unawasaidia wale ambao hawawezi kufanya kazi na wale wenye uhitaji."

Haya maneno mazuri ya bi Khadija yalimfanya Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) afurahi. Kisha wakaenda kwa Waraqa ibn Nawfal, mtoto wa baba yake mdogo na bi Khadija. Waraqa alikua ni mzee ambaye alikua anaifahamu vema taurati na injilli. Na pale bwana Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alipomwelezea kuhusu kile alichokiona. Waraka akastaajab sana kisha akasema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu wewe ni mtume wa zama hizi. Na malaika uliyemuona ni Malaika Jibril. Ni malaika huyo huyo ndiye alayeleta maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa Nabii Musa na Yesu pia."Waraqa aliendelea na kuzungumza:

"Natamani ningekua mdogo bado na ningekusaidia pindi watu watakapo kufukuza katika mji wako."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) aauliza kwa mshangao, "ni kweli watakuja kunifukuza katika mji wangu?" Waraqa akamjibu, "ndio.hakuwahi kuja mtume na kama kile ulichokuja nacho wewe, isipokua walimdhihaki na kumfukuzia mbali na nchi/mji wake."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na Qur'an tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na tumeit-eremsha kidogo kidogo."

(Al-Isra 17; 106)

Kuandika Qur'an Tukufu na kuihifadhi

Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikua akiwafikishia haraka sana aya za qu'ran kwa maswahaba wake. Aliwafanya baadhi ya maswahaba zake waandishi wa wahyi, waliokua wakinakili aya mpya zilizokua zikiteremka. Kwa namna hii aya za Qur'an tukufu hazikua tu zikhifadhiwa na Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) na maswahaba zake bali pia zilikua zikinakiliwa punde tu baada ya kuteremka.

Kwa mujibu wa zama hizo, waandishi wa wahyi walikua wakinakili aya za qu'ran katika vifaa vilivyowezekana kuandikia, mfano mawe membamba yaliyotambarare, nundu za ngamia, matawi ya mtende yasiyokua na majani na vigogo vya mashina ya mitende, mbavu za wanyama, vipande vya nguo au ngozi, vifaa vitokanavyo na mimea itambaayo majini (kutoka Misri) au mbaao nakadhalika.

Mtume wetu(rehma na Amani ziwe juu yake) alikua akizisoma kwanza aya mpya zilizoteremka na kuwfanya waandishi wazinakili. Kisha aliwaliza waandishi kusoma kile walichoandika na kutizama kama kuna makossa yejote katika maandishi yao. Makhalifa wanne wa mwanzo Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali(Mwenyezi Mungu awe radhi nao) walikua ni mionganoni mwa waandishi wa Wahyi. Maswahaba wengine mashuhuri kama Zaid Ibn Thabit, Ubai Ibn Ka'b na Muadh Ibn Jabal, nao pia walikua waandishi wa wahyi.

Mtume wetu(rehma na Amani ziwe juu yake) alikua pia akisoma aya za Qur'an katika swala

zake na wakati mwagine alikua akielezea kanuni na unyeti uliobebwa katika aya hizi kwa waumini. Kila mwaka katika mwezi wa Ramadhani, alikua akisoma na kuzipitia aya zilizokua zimeteremka hadi wakati huo kupitia Malaika Jibril. Katika mwezi wa Ramadhani mwaka ambao Mtume alifariki dunia, walipitia Qur'an nzima mara mbili.

Kuikusanya Qur'an Tukufu Katika Mfumo Wa Kitabu

Qur'an tukufu ilikua ikihifadhiwa pamoja na kulindwa kwa kuandikwa katika kipindi cha maisha ya Mtume wetu, japo aya pamoja na sura za qu'ran zilizokua zimenakiliwa hazikua zimechapishwa katika mfumo wa kitabu. Ilkua ni kwa sababu wahyi ulikua unaendelea kuteremka katika kipindi cha maisha ya Mtume wetu. Na pia kwa sababu wahyi ulikua haujakamilika hadi kipindi cha mwisho cha maisha ya Bwana Mtume, hivyo basi haikuwezekana kuweka katika mfumo wa kitabu.

Baada ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kufariki dunia, Abu Bakr (Mwenyezi Mungu awe radhi Nae) alichaguliwa kama khalifa. Katika ukhalifa wake maswahaba ambao walikua wamehifadhi Qur'an katika vifua vyao (Hafiz), waliuliwa katika vita. Kupungua kwa idadi ya maswahaba waliokua wamehifadhi Qur'an yote katika vifua vyao kulimfanya Umar (Mwenyezi Mungu awe radhi nae) apate hofu. Hivyo alimshauri Abu Bakr akusanye vifaa ambavyo aya za Qur'an zilikua zimenakiliwa. Ndipo Abu Bakr akaunda tume ambayo chini ya uongozi wa muandishi mkuu wa Mtume Zaid Ibn Thabit. Watu wote



waliokuepo katika tume hii walikua wakiifahamu Qur'an yote katika viua vyao. Baada ya kazi kubwa (Juhudi) iliyofanyinyika ndani ya muda wa mwaka mmoja maandiko yaliyokua yametawanyika yalikusanya na aya za Quran ziliandikwa katika kurasa safi. Mwisho kurasa hizi ziliwekwa pamoja katika mfumo wa kitabu na kukabidhiwa kwa Abu Bakr.

Kuinakilisha Qur'an Tukufu

Kipindi cha ukhalifa wa Umar na Uthman (Mwenyezi Mungu awe radhi Nao) ardhi ya waislam iliongezeka na kuwa na mikoa mijya kupitia ushindi uliopatikana katika vita. Watu kutoka lugha mbalimbali, tamaduni na mataifa

tofautitofauti waliukubali uislam. Kila mmoja alikua anataka kusoma na kujifunza kile ambacho Quyan inasema.

Ili kuweka mikakati thabitii kwa waumini kujifunza Quran, khalifa Uthman aliamua kunakilisha nakala ambayo ilikua imekusanya kipindi cha ukhalifa wa Abu Bakr. Uthman aliunda tena tume nyingine chini ya uongozi wa Zaid ibn Thabit na aliwataka wainakilitishe Qur'an Tukufu. Nakala moja ilibaki Madina. Nakala zingine zilpelekwa Makka, Kufa, Basra, Damascus, Yemen na Bahrain. Pamoja na nakala za Qur'an, mwalimu wa Qur'an alitumwa pia katika kila moja ya vituo hivo.

- ❖ **Qur'an Tukufu ilihifadhiwa na kuandikwa katika kipindi cha Mtume wetu.**
- ❖ **Ilikusanya na kuwekwa katika kitabu katika zama za ukhalifa wa Abu Bakr.**
- ❖ **Kuanzia kipindi cha ukhalifa wa Uthman, Qur'an ilinakilishwa na imetufikia hadi zama hizi pasina kubadilishwa hata kwa herufi moja.**



Faida za kusoma Qur'an Tukufu

Qur'an tukufu ni maneno makuu na mazuri sana. Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) amesema kwamba: "mmbora kati yenu ni yule anayesoma na kuifundisha Qur'an." Kwa maana hiyo jukumu letu kuhusiana na Qur'an ni kuisoma, kujifunza na kuwafundisha wengine. Tunahitaji kuishi kwa kufuata misingi yake(Qur'an).

Usomaji wa Quran ni kitendo cha ibada. Mola wetu Mtukufu ametoa habari njema juu ya pepo na baraka zake kwa wale amba wanaisoma Quran na kutumia kanuni zake katika maisha yao ya kila siku. Mtume wetu ametu-habarisha kuwa wazazi wa muumini mwenye

kuiosoma(Quran) watapata malipo maalum siku ya Kiama.

Kipenzi chetu Mtume Muhammad alikua akisoma Qur'an taratibu na kwa usahihi. Hivyo alikua akiwashauri wafuasi wake kuisoma Qur'an sawasawa na vizuri. Alitaka umma wake ukithiri katika kusoma Qur'an sana.amesema wale watakaokuwa wakiisoma vizuri watakuwa pamoja na malaika. Na kuwapa bishara njema wale wanaopata ugumu katika kuisoma kisha wakaendelea kuweka jitihada kuisoma.



Kipenzi chetu Mtume amesema:

Endapo mmoja wenu akiisoma Qur'an na kuiishi kutohata na ujumbe wake, siku ya Hukumu wazazi wake watapewa shada ya kuva ambayo nuru yake ni Zaidi ya mwanga wa jua ndani ya nyumba ambazo katika ulimwengu huu ulikua mionganii mwenu. Hivyo fikiria zawadi ya wale waliyoishi kwa .kuzingatia ujumbe wake

(Abu Dawud, Sunan, I, 355)



Mwenyezi Mungu amesema:

"Hakika wale wanaosoma kitabu cha Mwenyezi Mungu....(Mwenyezi Mungu) atawapa ujira na kuwapa Zaidi katika neema zake..."

(Fatir 35; 29-30)

YALIYOMO NDANI QUR'AN

Qur'an tukufu ina mtindo wake wa tofauti. Inahusisha mada tofauti katika aya moja au sura moja. Hutumia njia ya kuelezea ambayo inagusa kila nyanja ya binadamu. Kwa upande mmoja inavutia kwa utashi wa kibinadamu na upande mwininge inachukua saikolojia ya watu na hali zao kiimani katika kutafakari. Dhumuni lake si tu kutoa ujumbe, bali pia ni kuhamisha elimu na ujuzi katika Imani na Imani katika tabia na maadili mema.

Kabla ya yote haya Qur'an Tukufu inajaribu kuwa leta watu katika Imani sahihi. Inatufundisha sababu ya kuletwa hapa ulimwenguni. Imetutambulisha juu ya Mwenyezi Mungu kwetu. Inatuonyesha jinsi ya kukabiliana sisi kwa

sisi, Baba zetu na mama zetu, na watu wengine na viumbe wengine pia.

Masomo makuu yanayositisizwa katika qur'an ni: jambo la Imani, matendo ya ibada na kanuni za tabia njema. Pamoja na haya, kuna aya ambazo zinatuongoza katika nyanja mbalimbali za mahusiano ya binadam. Hadithi za mitume na matukio yaliyowatokea watu wa zamani zimeelezewa ndani ya Qur'an kwa sisi kupata mazingatio kuititia wao.

Tunapoidadisi Qur'an Tukufu, tunaona kua imebeba na katuongoza katika mazingira yafuatayo:

Masomo makuu yanayopatikana katika Qur'an

- Makala za Imani
- Matendo ya ibada
- Maadili mema
- Halali na haramu
- Mahusiano ya kijamii
- Dua
- Uumbaji na vyote vilivomo ndani ya ulimwengu
- Mitume na watu wa zama za kale.

Makala za Imani

Nyanja muhimu kabisa ya Qur'an Tukufu ni kuwa inatutambulisha kwa Mola wetu.

Inatuambia kuhusu uwepo na kumpwekesha Mwenyezi Mungu. Inamtambulisha Mwenyezi Mungu kwetu kupitia majina yake na sifa zake tukufu.

Makalazote za lmani zinazo fundishwa na Qur'an zinahusia ana na lmani kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine kwa mujibu wa Qur'an nguzo zote za lmani haziwezi kutengani shwa. Wale wana oamini juu ya Mwenyezi Mungu pia wataamini kuwepo kwa malaika, vitabu vyake aliyoviteremsha, mitume wake na siku ya kiyama. Pia huamini kila kitu hutokeea kwa hiyari na mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Matendo ya ibada

Qur'an Tukufu inatuamrisha sisi tuwe waja wa Mwenyezi Mungu. Inatupa kanuni za msingi zinazohusiana na ibada badala ya kutupa habari kwa uchache. Inavuta hisia zetu kwa ukaribu kati ya lmani na ibada. Inatuonyesha kua ibada inatakiwa kufanyika kwa aliji ya Mwenyezi Mungu na si kujifakharisha. Kupitia mifano mbalimbali inatuonyesha makosa ya kuabudu chochote isipokua Allah.

Matendo ya ibada, mfano, swala za faradhi, zaka, funga na hija yameelezwa dhahiri ndani ya Qur'an. Kila tendo ambalo linamfurahisha Mola wetu vinakubalika kama alama ya utumishi mwema. Kila kitu kinachomnufaisha binadamu, ikiwa ni pamoja na uso wenye tabasamu na maneno mazuri machache vyote vinajumuishwa ndani ya wigo wa ibada.



Maadili mema

Qur'an Tukufu inachukulia kua tabia njema ni kitu cha muhimu sana. Inajaribu kufanya tabia njema kushinda katika kila nyanja katika maisha. Ndio maana Qur'an inaongelea juu ya tabia njema katika nyingi ya aya zake. Inaelekeza watu katika wema pamoja na haki. Inaaamrisha kuwafanya ukarimu wazazi, na kusaidia ndugu, masikini na mafukara. Inakataza kufuja rasilimali na kudhuru maisha au mall za watu. Mara zote inatuvuta katika dhamira zetu katika misingi ya tabia njema kama vile kutimiza ahadi, kua mwaminifu na kudumisha mahusiano mazuri na wengine. Inaelezea kua tabia hiyo inapelekea mtu kupata furaha hapa duniani na kesho akhera.

Uumbaji na ulimwengu



Qur'an Tukufu inaleta hamasa katika ulimwengu na vitu vyote vilivymo ndani yake, inawakaribisha watu watafakari juu ya uumbaji na sababu za kuumbwa kwao. Inaendelea Zaidi kutuelezea ya kua Mwenyezi Mungu ameuumba huu ulimwengu katika hali ya kutokuepo kwa chochote.

M pangilio madhubuti wa ulimwengu umeelezewa ndani ya Qur'an. Inaleta hamasa katika uumbaji wa binadamu, wanyama, mimea, dunia, anga, jua, mwezi na vitu vingine vingi kabisa. Inaelezea kua dalili zinazoonyesha uwepo wa Mwenyezi Mungu na umola katika uumbaji wa kila kitu. Tunatakiwa kuchunguza kwa makini dalili hizi na kugundua nguvu zisizokua na mwisho na rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Dua

Swala ndio kiini cha ibada. Tunaelezea shukrani zetu kwa Mola wetukupitia dua zetu. Tunapohitaji msaada na tunapohisi kuzidiwa na jambo, tunakimbilia katika milango yake ya rehma na msamaha. Tunafungua mikono yetu na kuomba msaada kutoka kwake. Tunapata kukimbilia kwenye upole na msamaha wa Mwenyezi Mungu.

Mifano ya swala za uaminifu na kweli, hasahasa mifano ya swala za mitume, imechukua nafasi maalumu katika kitabu chetu kitukufu katika Quran Mola wetu mtukufu anatufundisha namna ya kumuabudu yeye. Ametuamrisha tufanye ibada kwake tu na anatuambia ni yeye pekee anaeyeweza kujibu maombi yetu.

Halali na Haramu


Kile kilichoruhusiwa katika uislam huitwa halali na kile kilichokatazwa kinaitwa haramu. Qur'an Tukufu imeelezea vitu vya halali na vya haramu. Inaelezea kua vitu vyenye faida, vizuri, na visafi ni halali. Pia imeelezea kua vitu vya halali vinatosha kwa binadamu na hakuna yeyote atakayetangaza uharamu wa vitu ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyofanya halali. Imekatazwa kula na kunywa vitu kama damu, nyama ya nguruwe, mizoga ya wanyama, na vinywaji vyenye vilevi. Zimepigwa marufuku pia njia zisizokua halali ya kujipatia kipato mfano, udanganyifu,wizi,riba,Kamari na rushwa. Inayajumuisha hayo mionganoni mwa makosa makubwa mno kwa Mwenyezi Mungu na jamii ya kiislamu. Inaonya watu wote wanaotumia mifano mibaya kwa wale waliochukua haki za wengine kwa kuadanganya katika kupima na usawa.

Uhusiano wa kijamii

Lengo kuu la Qur'an Tukufu ni kumpandisha mtu katika watu wenye Imani thabiti, maarifa ya kweli na tabia njema. Inakusudia kutengeneza jamii ya watu wema kutoka kwa huyu mtu mmoja. Qur'an Tukufu imeimarisha kanuni na miongozo katika mahusiano yetu ya kijamii. Ndio maana kuna aya kadhaa wa kadhaa katika Quran ambazo zinahusisha mahusiano ya kijamii kama vile ndoa, talaka,biashara,miamala,urithi,uongozi na elimu. Nyongeza katika aya hizo za miongozo, kuna aya ambazo zinahusisha makosa na adhabu kwa wale ambaao wanadhulumu haki za mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla. Mauaji, wizi wa kutumia silaha, uzushi au kumuharibia mtu sifa yake yote hayo yanakubalika kama madhambi makubwa ndani ya Quran. Aya za Quran pia zinafanua jinsi dhambi hizi zitakavyotolewa adhabu na upi utakua ukubwa wa adhabu hizi.

Mitume na watu wa zamani

Kuanzia kwa Nabii Adam (Amani iwe juu yake) historia ya binadamu imejaa mafunzo. Qur'an Tukufu inatupa mifano kutoka katika maisha ya mitume na watu wa zamani ili kuwapa kizazi kijacho kitu cha kujifunza kutoka kwao. Inaelezea mapito mazuri na mabaya ya jamii. Inatutaka kuchukua mazingatio na sio kuangukia katika makosa yale yale.



MTUME WETU NA QURAN TUKUFU

Kipenzi chetu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikua anapenda kusoma Quran tukufu. Alikua akisoma taratibu na kwa usahihi. Usomaji wa Bwana Mtume ulikua unampa mtu uzuri na ladha tofauti. Watu waliokua wakisikiliza akisoma mara moja walikua wakiathirika na usomaji wake. Siku moja Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alisoma surat tin katika swala ya usiku, mmoja wa maswahaba zake akasema kwamba hajawahi kusikia mtu yoyote mwenye sauti nzuri kama sauti ya Bwana Mtume.

Mtume wetu wakati mwagine alikua akisoma Quran kwa sauti alipokua anaendesha mnyama wake. Kwa mfano siku walipokwenda kuiteka Makka alisoma aya za mwanzo za surat Fatih 48 juu ya ngamia wake. Wale maswahaba waliokuwa wakisikiliza walisema kua sauti

yake nzuri haikuwahi kufutika katika masikio yao na mioyo yao.

Kipenzi chetu Bwana Mtume alikua akitafakari maana ya aya alizosoma kisha aliswali mahususi kwa maana zake. Alipokua anasoma aya zinazomtuka Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi alimtuka. Ikiwa anasoma aya iyotaka kuomba jambo toka kwa Allah, alikua akimuomba yeye. Wakati mwagine alikua anatafakari aya moja tu kwa usiku mzima. Usiku mmoja alikua akirudia aya, "Endapo utawaadhibu, hakika ni watumwa wako, na endapo utawasamehe, hakika ni watumwa wako. Hakika! Wewe,wewe pekee ni Mkuu na mwenye hekima (maida 5:118) mara kwa mara. Kisha alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa upendo wake juu ya umma wake na kwa sababu ya wasiwasi wake kwamba wanaweza



kuadhibiwa. Alimuomba Mwenyezi Mungu kuusamehe umma wake.

Wakati mwagine Mtume wetu alihamishwa na aya alizosoma na machozi yalikua yakimtiririka katika mashavu yake yaliyobarikiwa. Aliwashauri maswahaba zake waisome Quran kwa huzuni.

Siku moja mama yetu bibi Aisha (Mwenyezi Mungu awe radhi nae) aliulizwa:

"Waweza kutuambia kitu cha kushangaza Zaidi ulichowahi kukishuhudiya kwa Bwana Mtume?"

Bi Aisha akajibu:

"Kitu ambacho hakikua cha kawaida? Kisha akasimulia tukio lifuatato:

"Usiku mmoja alilingia kitandani. Baadaye aliniomba ridhaa na akatoka kitandani. Akachukua udhu na akaanza kuswali. Akiwa anaswali akaanza kutokwa na machozi sana kiasi cha machozi kutiririka hadi katika kifua chake, akarukuu na kuanza kulia. Aliendelea kulia hata alipofikia katika sujudu na alipoinua kichwa kutoka katika ardhi. Hali hii iliendelea hadi Bilal alipokuja na kuadhini swala ya alfajir. Bilal(Mwenyezi Mungu awe radhi nae) alipomuona Bwana Mtume Analia, akauliza:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Japokua umesamehewa madhambi yako yaliyopita na yajayo, kipi kinakufanya ulie?"

Mtume Wetu(rehma na amani ziwe juu yake) akamjibu: "Je, siwezi kua mja mwenye kushukuru kwa Allah?"

Kisha akasema kua ameshushiwa wahyi usiku na kwamba aya hizo zinatakiwa kusomwa kwa umakini mkubwa na kutafakariwa. Kisha akasoma aya zifuatazo:

"Kwa hakika katika uumbaji wa mbingu na ardhi na kubadilika kwa usiku na mchana kuna mazingatio kwa watu wenye kufahamu. Wale wanaomkumbuka Allah wakiwa wamesimama na wakiwa wamekaa na wakiwa wamelala kiubavu na kutafakari juu ya mbingu na ardhi wakisema: Mola wetu! hukuviumba hivi kwa bahati mbaya! Utukufu ni wako. Tuokoe katika adhabu ya moto." (Al-i Imran 3; 190-191)

Mtume alikua akisoma Quran katika mwezi wa Ramadhan kuliniko kipindi kingine chochote cha Mwaka. Jibril(Amani iwe juu yake) alikua akija mara kwa mara kwa Mtume wetu katika mwezi huu na kwa pamoja walikua wakizipitia aya zilizokua zimeteremka hadi katika kipindi hicho.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikua akipenda kusikiliza watu wengine wakisoma Quran pia. Alikua akiwaambia maswahaba zake wenye sauti nzuri kumsomea. Mara moja alimuomba Abdullah Ibn Mas'ud(Mwenyezi Mungu awe radhi nae) kumsomea Quran. Abdullal Ibn Mas'ud akamwambia Bwana Mtume,

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa namna gani naweza kusoma Quran kwako hali ya kua imeanza kuteremshwa kwako?" hapo Mtume akasema;

"Napenda sana kusikia Quran kutoka kwa mtu mwagine" kisha Abdullah Ibn Mas'ud akaanza kusoma kutoka katika Surat Al-Nisa(4). Alipoisoma aya, "Basi itakuaje pindi tukiwaleta katika kila umma shahidi, na tukakuleta wewe kama shahidi wa hawa?" (Al-Nisa 4:41)

Mtume akasema, "Hii inatosha kwa sasa" Abdullah Ibn Mas'ud msimulizi wa tukio hili alisema, "Nilipomtazama Bwana Mtume usoni,

nilliona machozi yakidondoka katika macho yake mawili."

Kipenzi chetu Mtume aliichukulia Quran tukufu kama kipimo katika kila Nyanja ya maisha. Aliishi maisha yake kwa kuzingatia Quran. Matendo yake yote, tabia, maadili, na mawazo yake yalitawaliwa na aya za Quran. Bi Aisha mama wa waumini alisema kuwaambia wale waliouliza kuhusu maadili ya Mtume:

"Hamsomi Quran?" maadili yalikua yanategemea kanuni za maadili ya Quran."

Kwa maneno haya, bi Aisha(Mwenyezi Mungu awe radhi nae) alisisitiza kuwa matendo


na tabia za Bwana Mtume zilikua ni kwa mujibu wa Quran na alikua mithili ya quran iliyo hai. Na kwa kuzingatia sifa ya Mtume, Mola wetu Mtukufu amemleta yeye kwa watu kama mfano bora.

Quran tukufu haikutengeneza tu maisha ya Mtume lakini pia maisha ya waislamu wote waliokua wakimfuata yeye. Kizazi cha mwanzo cha waumini walishi maisha yao binafsi nay a jamii kwa ujumla kutokana na kile ambacho quran imekieleza. Kwa kuchukulia Mtume kama kigezo chao, walikua wataalamu wa kwa kwanza wa Quran.



MASWALI

FUMBO LA MANENO



Kwenda kulia

2. Maelezo na maoni yaliyojitosheleza kuhusu aya za Quran; maoni ya Quran
7. Kitabu kitukufu cha mwisho mionganini mwa vitabu vitukufu
8. Ni aya za sura gani ziliteremka kwanza?
10. Sura ya kwanza katika Quran
12. Vijitabu vitukufu vidogo vidogo
13. Sura ya mwisho katika Quran
15. Mtu anayefahamu Quran yote kwa moyo
16. Habari na ujumbe uliotumwa kwa binadamu na Mwenyezi Mungu kupitia mitume
17. Malaika anayeteremsha wahyi

Kushuka chini

1. Kitabu kilichoteremshwa kwa Naabii Daudi
3. Sura ndefu kuliko zote katika Quran
4. Mwezi ambao Quran ilianza kuteremshwa
5. Jina linalotumika kwa kila kurasa za Quran
6. Kitabu alichoteremshiwa Nabii Mussa
9. Usiku ambao Quran tukufu ilianza kushuka
11. Kitabu alichoteremshiwa nabii Issa (Yesu) (Amani iwe juu yake)
14. Tafasiri ya Quran kwa lugha nyingine



Tafuta Maneno Yanayowiana Kwa Usahihi



1	Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha ujumbe wake kwa mitume wake.	Kimetufikia sisi katika uhalsia wake bila mabadiliko.
2	Toka zama za nabii Adam(Amani iwe juu yake) mitume wametuletea	Maamrisho na makatazo ya Mola wetu Mtukufu.
3	Tunafuata amri katika vitabu hivi na,	Uzuri na ukweli wa vitabu vyote vilivyo-tangulia.
4	Kwa kuzingatia mahitaji ya binadam Mola wetu mtukufu ametuma	Watu walipoanza kuhamia katika Imani isiyokua sahihi.
5	Tunaamini kuwa Quran Tukufu ni	Aidha moja kwa moja au kupitia ma-laika.
6	Vitabu vitukufu vinatuambia	Kujaribu kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.
7	Ni lini nakala halisi za vitabu vitukufu vilingia hitilafu,	Maneno na ujumbe wa Mwenyezi Mungu.
8	Quran Tukufu inajumuisha	Kwa baadhi ya mitume wake vitabu vi-dogo vilivyoitwa <i>suhuf</i>



Tujipime wenywewe



- 1. Ni jina gani waliitwa mswahaba waliokua wanaandika wahyi kipindi cha zama za Mtume?**
 - A) Maswahaba
 - B) Wahamiaji
 - C) Waandishi wa wahyi
 - D) Wasaidizi

- 2. Ni ipi kati ya habari zifuatazo haziwezi kusemwa kuhusiana na Quran?**
 - A) Imeteremshwa na malaika Jibril
 - B) Iliteremka kwa lugha ya kiarabu
 - C) Uteremsho wake ulianza usiku wa Mi'raj(kupaishwa).
 - D) Imetufikia sisi pasipo na mabadiliko yoyote

- 3. "Tizama, Luqman alisema kumwambia mwanae alipokua anamuonya: Ewe mwanangu usimfanyile Mwenyezi Mungu mshirika. Hakika!kumfanyia mshirika naye ni dhulma kubwa... Ewe mwanangu! Dumisha swala zako na uamrishe mema na ukataze mabaya, na kuwa na subra kwa yale yatakayokukuta, ama hakika matendo haya yanahitaji ujasiri; na usigeuze uso wako kwa watu wanaokudharau, na usitembee katika ardhi kwa majigambo; hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wale wenye kujifakharisha." (Luqman 31; 13-18)**

Ni lipi kati ya haya yafuatayo ni kitendo kibaya kwa mujibu wa aya iliyotajwa hapo juu?

 - A) kutoonyesha subra unapopatwa na shida
 - B) kumshauri ukweli mtu anayeongopa
 - C) kuswali
 - D) kutomshirikisha Mwenyezi Mungu

4.

- I. Imekua rahisi kuhifadhi
- II. Imesaidia kuiandika Quran
- III. Imetoa nafasi ya kujifunza kanuni za Quran vizuri

Haya ni matokeo ya:-

- A) Kuteremka kwa Quran kidogo kidogo
- B) Kuteremshwa kwa Quran kwa lugha ya kiarabu
- C) Kuteremka kwa Quran kwa Mtume Muhammad
- D) Kuteremka kwa Quran kupitia malaika Jibril

5. Ipi ni sababu ya kwanza ya kuteremshwa Quran?

- A) Kuisoma katika swala zetu
- B) Kuwaunganisha waislam
- C) Kuisoma kwa ndugu zetu waliofariki
- D) Kutuhabarisha kuhusiana na akhera

6. Ipi kati ya zifuatazo sio miongini mwa sababu ya kuteremshwa kwa vitabu vitukufu?

- A) Kutupa maamrisho na makatazo
- B) Kutupa habari kwa undani Zaidi
- C) Kuanzisha maadili mema
- D) Kutupa habari kuhusiana na akhera

Jaza Sehemu Zilizoachwa Wazi Kwa Kutumia Maneno Haya:-

(kitabu cha Mwenyezi Mungu, watu, mkumbushaji, nuru, shada, muongozo sahihi, kilichomo ndani yake, taurati, mlinzi, injili, kitabu, kwa sehemu)


1. "Tumemtuma yeye (Yesu).....ndani yake kuna muongozo na....., na kusadikisha sheria zilizokuja kabla yake, muongozo na onyo kwa wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu." (al-Maidah 5; 46)
2. "Kwa hakika tumeteremsha.....(Quran) na kwa ukweli tutakua..... wake" (Hijr 15; 9)
3. "Ameteremsha kwenu.....kwa haki, kuthibitisha yaliyokuwa kabla yake, na ameteremsha.....na injili hapo zamani kama muongozo kwa watu." (Al-i Imran 3; 3)
4. "Na ni hii Quran tulioiteremsha.....kwahiyio mnawenza kuisoma kwa..... kwa kiwango cha polepole, na tumeiteremsha hatua kwa hatua." (Al-Isra 17; 106)
5. "Ninawaachia vitu viwili muhimu sana, moja ya hivyo ni.....kilichoinuliwa na utukufu, na hiyo ni kamba ya Mwenyezi Mungu. Yule atakaye ishikilia mapema atakua katika.....na yule atakayeliachilia atakua katika upotevu." (Muslim, Fada'il al-Sahaba, 37)
6. "Endapo mmoja wenu akiisoma Quran na kutenda kwa mujibu wa..... katika siku ya hukumu wazazi wake watavalishwa.....ambalo mwanga wake ni Zaidi ya mwanga wa jua katika nyumba za dunia hii. Hivyo fikiria thawabu za yule anayeishi kwa mujibu wa yaliyomo ndani yake." (Abu Dawud, Sunan, I, 355)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hii (Qur'an) ni ujumbe ulio wazi kwa watu ili wapate kuonyeka kwayo, na wapate kujua kua Mwenyezi Mungu ni Mola mmoja, kisha wale wenye kuelewa wapate mazingatio."

(Ibrahim 14; 52)






WATU WA MIFANO:

IMANI JUU YA MITUME

- ✿ Mitume na sifa za mitume
- ✿ Ujumbe unaofanana kwa mitume wote
- ✿ Vitu tunayovipata katika Imani juu ya mitume
- ✿ kuna mifano bora kabisa tunaipata katika maisha ya mitume
- ✿ Mtume wetu na mitume wengine



MITUME (WAJUMBE WA MWENYEZI MUNGU)

Kazi za nyumbani za Husein zilikua ni kuhusu utume. Alikua akienda kupitia vitabu vya kiada na kijiandaa na somo na marafiki zake walikua wakienda kwake kumuuliza chochote walichokua wakitaka kumuuliza. Muda ambao masomo yalikuwa yakianza, mwalimu wake alikua akimuuliza yeye swali la kwanza:

— “Niambie Hussein! **Nini maana ya mtume?**”

— “Mtume ni mtu ambaye anayewafikisha watu maamrisho ya Allah” Hussein alijibu. Mwalimu alipendezwa na muitikio wa Hussein kisha akawageukia wanafunzi wengine:

— “Ni zamu yako sasa! Waulize marafiki zako kitu chochote unachohitaji kujifunza. Kwa njia hii nitaona ni jinsi gani unalipenda somo hili.”

Sulaiman akanyanya mkono wake:



— Je, mtu yeyote anaweza kua Mtume?

Hussein akajibu swalii la rafiki yake kama ifuatavyo:

— "Utume si kazi ambayo unaweza ukaipata kwa kufanya kazi kwa bidi au kuabudu. Mwenyezi Mungu humchagua yule anayemtaka mionganii mwa waja wake ili awe mijumbe wake. Kwa sababu utume si kazi nyepesi kuifanya, Mwenyezi Mungu Mtukufu huwapa kazi hii waja wake ambayo wataifanya kwa ufashaa Zaidi."

Ahmad alinyanya mkono wake:

— "Je, utume unarishishwa toka kwa baba kwenda kwa mtoto wake kama ilivyo usultani au ufalme?"

— "Hakuna sheria kama hiyo, japo kuna mitume ambaao watoto wao wa kiume walichukua na kuendeleza majukumu ya baba zao. Kwa mfano baada ya Nabii Ibrahim, watoto wake Is'haqa na Ismail walikua mitume. Hivyo hivyo baada ya Nabii Yaqub mwanae Yusuf; Baada ya Nabii Daudi mwanae Sulaiman (Amani ziwe juu yao) walikua mitume. Ingawa, hii si sababu ya utume kua kitu cha kurithiwa, lakini ilikua ni kitu ambacho Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka iwe hivyo."

Batul akasema:

— "Hiyo inamaanisha kua watoto wa mitume pia walikua watu wema kama baba zao."

— "Hiyo si mara zote sababu," Hussein alisema. Palikua na baadhi ya mitume ambaao watoto wao hawakuamini kama watu wengine wakati wao. kwa mfano mtoto wa nabii Nuhu hakuamini utume wa baba yake na aliangamizwa pamoja na wasioamini wengine(makafiri) katika mafuriko."

Zainab alichangia katika mazungumzo kwa kusema:

— "Mitume lazima walikua matajiri na watu wenye kuheshimika katika jamii zao. **Vinginevyo hakuna ambaye angewasikiliza.**" Hussein alijibu kwa kuzingatia mapendekezo ya Zainab:

— "Tunaweza kupata jibu la swalii katika maisha ya Mtume wetu. Mtume wetu Muhammad (rehema na Amani ziwe juu yake) alitoka katika familia iliyokua inaheshimika, lakini hakua tajiri. Baadhi ya watu wake wa karibu walikua wakimpinga kwa kusema: "endapo watu wangekua na haja ya mtume basi angekua ni mmoja kati ya watu matajiri mionganii mwetu." Walikua hawaelewi ni jinsi gani malaika mlela ujumbe anavyoweza kuleta wahyi kwa mtu masikini. Kwa hiyo mali ina nafasi gani katika majukumu ya heshima kama utume?" Abdurrahman aliuliza:

— "Je, unafahamu walikuepo mitume wangapi?"

— "Majina ishirini na tano ya mitume yametajwa katika Qur'an" Hussein alisema. Kisha mwalimu wake akaongezea:

— "Katika historia ya binadamu watu wengi wamehudumu kama mitume. Wengi katika mitume walijotajwa katika Qur'an wana uhusiano kati yao. Kwahiyo mitume hao wameishi kwa kutekeleza dhamira ya utume kuzunguka ghuba ya uarabuni. Bila shaka walikuepo mitume wengine ambaao walitumwa kwa watu sehemu zingine ulimwenguni. Mtume wetu amesema namba ya mitume ilikadirwa kufikia laki moja na elfu ishirini na nne."

Aisha akauliza:

— "Je, Qur'an tukufu iliteremshwa kwa mitume wote?" Hussein akatabasamu:

— "Swali lako haliko sahihi. Qur'an tukufu ni jina la kitabu kitukufu kilichoteremshwa kwa Mtume wetu. Hivyo swalii lako lingekua "**Palikua na kitabu chenye kufanana na Qur'an Tukufu kilichotumwa kwa mitume wote?**" na jawabu langu kwa swalii hilo lingekua "hapana."

Tumejifunza majina ya mitume ambao vitabu viliteremshwa kwao pamoja na majina ya vitabu hivyo katika sura iliyopita kuhusu kuamini vitabu vya Allah." Ndipo Ali akauliza:

— "Wakristo na wayahudi hawakumuamini Mtume wetu. Je haitokua sahihi ikiwa nasi pia hatutowamini mitume wao?" Hussein hakujibu haraka swali lile. Hivyo mwalimu wake alikuja kumsadia:

— "Hiyo ndio tofauti kubwa kati yao nasisi waislam. Tunaamini mitume wao kwakua Qur'an Tukufu imetaja majina yao na maisha ya nabii Mussa na Issa (Yesu) pamoja na mitume wengine. Si katika tabia njema kubishana katika jambo hili. Tunaamini katika mitume wote pasipo kuweka tofauti baina yao." Fatima akauliza:

— "**Ni mtume yupi mkubwa kuliko wote?**" Hussein akajibu:

— "Mtume wetu Muhammad ndio mtume mkubwa kuliko mitume wote." Fatima alihitaji kufahamu sababu zake na akauliza:

— "**Kwanini Mtume Muhammad ndiye mkubwa kuliko mitume wote?**"

— Hussein alipogundua kua hawezи kujijibu swali lile, akamgeukia mwalimu wake na kumuuliza:

— "Mwalimu waweza kutufafanulia jambo hili tafadhalii? Kwa kuzingatia ombi hili mwalimu akasema:

— "Ukubwa wa mtume hupimwa kwa ukubwa wa kazi mahususi aliopewa, matendo yake pamoja na mateso alivyokutana navyo.

Kwa mujibu wa Qur'an, nabii Nuhu (Amani iwe juu yake), kwa mfano aliishi miaka 950 mionganoni mwa watu wake. Watu walikua wakiishi umri mrefu wakati huo, nabii Nuhu alifikisha ujumbe wa Allah kwa watu wake na alifanya kila jambo liliowezekana kuwaongoza katika njia iliyonyooka, lakini ni watu wachache tu ndio waliomwamini. Na mwisho, kama

tunavyofahamu, wale wote ambao hawakumuamini waliangamizwa kwa mafiriko makubwa kabisa.

Kumbuka Ibrahim (Amani iwe juu yake), watu aliomwakaribisha katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu waliadhimi kumwadhibu kwa moto. Lakini Mwenyezi Mungu hakutaka jambo lile litokee na aliubadilisha moto ule kua bustani yenye kupendeza ya mawaridi. Hivyo alimuokoa Ibrahim asichomwe moto.

Ingawa mateso ya nabii Mussa, Issa (Yesu) na Mtume wetu Muhammad yalikua ni zaidi ya tufikiriyavo, waliyapitia mateso yale kwa ajili ya kazi yao mahususi. Kwa subra ya hali ya juu walistahmili kupigwa, kudhalilishwa na hata kufukuzwa katika mijji yao waliyokuwa wakiishi,

Kuna sababu za msingi kwa Mtume wetu Muhammad kua mkubwa kuliko mitume wengine.

Yeye ni Mtume wa mwisho.

Utume wake umekua ukiendelea kwa karne kumi na nne zilizopita na utaendelea hadi siku ya mwisho. Yeye ni mtume alotumwa kwa walimwengu wote; ukilinganisha na mitume waliotangulia kabla yake walitumwa kwa kundi Fulani la watu.

Na tunajifunza katika maneno yake, Mtume wetu pia amekua ndiye kipenzi Zaidi cha Mola wetu mionganoni mwa waja wake.

— "Lakini mwalimu, **kuna mamilioni ya wakristo katika dunia. Tunapofikiria kuhusu kizazi kijacho, nabii Issa (Yesu) (Amani iwe juu yake) angetakiwa awe mkubwa kama alivyoo Mtume wetu**" Mariam alisema.

Mwalimu akajibu swali lake kama ifuatavyo:

— Anapokuja mtume mwingine, kazi ile mahususi alotumwa kwayo hufikia mwisho wake. Jambo hili hujirudia katika historia. Hata nabii Issa (Amani iwe juu yake) alituhabarisha kuhusu ujio wa mtume mwingine baada yake. Kumfuata nabii Issa (Amani

iwe juu yake) inalinganishwa na kuendelea kutumia mishumaa hali ya kua umeme umeshagundulika. Hali hii pia imepelekea Nabii Issa (Amani iwe juu yake) kutojisikia vizuri.

Zaki alinyanya mkono wake na kuuliza swali jingine tofauti:

— **“Je, katika uhalisia ni kweli tunahitaji mitume? Watu hawataweza kuipata hiyo njia iliyonyooka endapo pasingekuwepo na mitume?”**

Mwalimu akamchagua Hussein na Hussein akajibu swali ilie:

— Watu wasingeweza kuupata ukweli endapo pasingekuepo na mitume. Wangeweza kuelewa uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini wasingeweza kufahamu namna gani sahihi ya kumwabudu yeye. Wasingeweza kujua kama kuna malaika, yakua kuna maisha ya milele baada ya kufa, na wangekua wanajiuliza kuhusu nini wamekifanya katika ulimwengu huu. Kwa kuzingatia sababu zao, wangekuja na baadhi ya matendo maovu japo si yote ambayo mitume

wamewatahadharisha kwayo.

Ila kwa kua Mwenyezi Mungu anatupenda sana waja wake, akawatuma mitume wake kuja kutufundisha habari hizi zote. Wajumbe hawa pia wamekua mifano kwa watu kwa tabia na adabu njema.

Ruqiya akauliza:



— “**Nastaajabu! wangeaminika zaidi endapo Mwenyezi Mungu angetuma ujumbe wake kupitia malaika wake.**” Hussein alifikiria kwa muda kidogo namna ya kujibu swali hili la kushangaza. Kisha akasema:

— “Tusingefahamu haya. Endapo hii ingekua njia bora zaidi, Mwenyezi Mungu angeifanya njia hiyo.” Mwalimu wake akafikiria swali hili la Ruqiya linahitaji maelezo ya ziada hivyo aliongezea:

— “Alichokisema Hussein kipo sahihi. Tunaweza pia kujibu swali hili kama ifuatavyo: Endapo Mwenyezi Mungu angetuma maamrishi yake kupitia malaika wake, baadhi ya watu wangesema:

— “**Kwasababu hatuwezi kuwaona malaika, hivyo hatuwezi kuwaauliza maswali yetu.** Hatutokua huru kuzungumza kwa sababu tunawaogopa. Ni rahisi kwa malaika kusema “**Usifanye dhambi**” kwakua wao hawatendi madhambi. Tungetamani endapo wangekua binadamu kama sisi angetufikishia ujumbe huo kwetu. Tungestaajabu kama yeye angefanya yale anayotuamrisha sisi kuyafanya.”

H a o ambao hivyo wangekua sahihi kwa kile wakisemacho, kwa sababu, ni jambo rahisi kusema, “fanya hiki au usifanye kile.”

Lakini ni vigumu kufanya yale unayoyaamrisha wewe binafsi. Hii ni sababu Mola wetu Mtukufu alituma ujumbe wake kupitia mitume wake ambao waliyatekeleza

maamrisha hayo, na kujitenga nayale aloyakataza, na walikua mifano bora kabisa kwa watu wao."

Akif alinyoosha na kuushusha mkono wake. Ilionekana kana kwamba anahofia kuuliza swali alilokua nalo. Mwalimu alipoona hofu aliyokua nayo Akif , akauliza:

— "Unahitaji kuuliza jambo Akif,sivyo?"

— "Ndiyo lakini....."alisema Akif kisha akanyamaza kuongea.

— "Usiogope. Uliza chochote unachohitaji kufaham Akif" mwalimu alisema

— "Je, mitume walikua wanapata ujira kwa kazi yao? Kama walikua wanapata, ni kutoka kwa nani walikua wanapata pesa?"

M w a l i m u
akatabasamu.
Akif alikua bado



anasita. Alihisi fedheha na hofu endapo aliuliza swali lisilokua na maana. Watoto wengine walikua wanasubiri kwa hamu muitikio wa mwalimu wao. Mwalimu:

— Vizuri sana, Akif!"umeulizaswalizurisana. Swali hili limejibowi katika Qur'an Tukufu mara kadhaa. Mitume wote walikua wakiwalingania katika njia iliyonyooka: **"Sihatiji malipo yoyote kutoka kwenu; malipo yangu nayapata toka kwa Allah pekee"** Kukinai kwa wajumbe wake juu ya Mwenyezi Mungu ni malipo makubwa sana kwao. Na huduma kubwa na za kuendelea bila ukomo ni zile zinazofanywa pasina malipo

Baada ya hapo kengele ya shule ikagongwa. Mwalimu alimshukuru Hussein kwa kazi nzuri na majibu mazuri. Hussein akamjibu:

— "Kwakweli napenda kukushukuru sana mwalimu. Nimejifunza kila kitu kutoka kwako. Endapo usingenisaidia, nisingeweza kuandaa kazi hii."

M. Yaşar Kandemir

MUONGOZO WETU

Mfereji wa Bosporus ambao unapatikana kati ya mabara mawili Asia na Ulaya una uzuri wa kipekee. Kila siku mamia ya meli yanapita katika mfereji huu unaouunganisha Bahari Nyeusi na Bahari ya Marmara. Ingawa, kuna baadhi ya sehemu katika mfereji huu una kina kifupi zaidi kwa meli kubwa, inakua hatari sana kupita hapo. Hasahasa meli kubwa za mafuta na meli kubwa za abiria ambazo zinatakiwa ziwe makini sana zinapopita katika mfereji wa Bosporus. Ndio maana manahodha wa meli hizo huwaomba waongozaji wa vyombo baharini kutoka katika mamlaka ya mji kwa ajili ya kuwakinga na ajali pamoja na kugonga wanapokua wanashuka pwani. Na wanaweza wakapita kwa usalama katika mfereji kwa msaada wa muongozo kwa wale wanaojua vizuri kuhusu meli zinazopita katika mfereji huo, kina pamoja na hali ya pwani.

Maisha katika dunia hii ni kama meli. Na sisi kama binadamu ni wasafiri katika meli hii kutoka ulimwengu wa kiroho kwenda katika nyumba ya maisha baada ya kifo. Endapo tungekua nahodha tukihitaji kupita katika mfereji wa Bosporus, tungeomba muongozaji wa vyombo baharini kutoka katika mamlaka ya mji. Sisi pia tunahitaji miongozo ili kuishi maisha mazuri hapa ulimwenguni, kuipata pepo na kuepushwa na

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na tumewafanya mitume viongozi, wawaon-
goze watu kwa amri yetu..."

(al-Anbiya 21; 73)

moto wa jahanam baada ya kufa na kuondoka. Mitume ndio hao waongozaji waliotumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Sababu ya kuumbwa wanadamu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu ili kufikia radhi zake. Binadamu ambao wanapata mitihani katika huu ulimwengu wanapaswa kumpinga shetani, kwa hisia zinazopelekea kua na tabia mbaya kama kusema uongo, uftinshajji na kugombanisha pande mbili. Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuwaacha hivyo pasina muongozo katika safari hii ngumu. Amewaonyesha njia iliyonyooka na amewapa ushauri namna ya kuupata ukweli. Pia amewachagua waongozaji miongozi mwao ili kuwaonyesha mifano bora zaidi.



© Adem Özdemir

MITUME NA SIFA ZA MITUME

Kuamini mitume ni moja kati ya nguzo sita za Imani. Kuwaamini kwao ni kuamini kua walikua wajumbe waliotumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kukubali kila ujumbe waliokuja nao ni wa kweli. Kuwapinga mitume ni kuipinga dini. Kwa sababu mitume ndio waliokuja na dini, kufundisha vitabu vitukufu, na kufikisha ujumbe walokuja nao kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Tunawaita wajumbe hao ambao walikua na jukumu la kufikisha maamirisho ya Mwenyezi Mungu na kukataza mabaya kwenye utu. Mola wetu Mtukufu alimteua mwanadamu wa kwanza nabii Adam (Amani iwe juu yake) pia kama mtume wa kwanza. Nabii Adam alifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu. Kuna wakati binadamu walimsahau Mwenyezi Mungu na akhera, na wakapotoka. Ndipo Mwenyezi Mungu akawatumia mitume mwininge kwa ajili ya kuwatahadharisha. Bainya ya mitume wa mwanzo nabii Adam na mitume wa mwisho Mtume Muhammad (Amani iwe juu yao) pamekua na mitume wengi. Katika moja ya maneno ya mitume wetu Muhammad inasemekana kua mitume laki moja na elfu ishirini na nne (124,000) walitumwa. Katika Qur'an Tukufu majina ishirini na tano pekee (25) kati yao ndio yametajwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu anatupa mifano ya habari zao kuhusu maisha ya mitume hao.

Nabii Adam, Idris, Nuhu, Hud, Saleh, Ibrahim, Lut, Ismail, Is'haq, Yaqub, Yusuf, Ayub, Shuaybu, Harun, Daudi, Suleiman, El'yasa'a, Al-yasa'a, Yunus, Dhul-kifl, Zakariya, Yahya, Issa (Yesu) na Muhammad (Amani iwe juu yao)

Mwenyezi Mungu Mtukufu amechagua mitume wake mionganoni mwetu wanadamu. Walikua ni kama sisi. Walikua wakila, wakinywa, wakifanya kazi na kua na ujuzi na taaluma fulani. Walioa na kua na watoto. Walipatwa na maradhi na walikufa. Ingawa mitume walikua tofauti na sisi kwa kua kua wao walipokea wahyi. Walikua ni watu maalum waliobarikiwa waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kufanya kazi mahususi. Walikua na jukumu la kufikisha dini ya Mwenyezi Mungu kwa watu na kuishi katika misingi ya Allah.

Kwa kuwachagua mitume wake Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaalia kwa baadhi ya sifa za kipekee. Kutokana na sifa hizo walikua na uwezo wa kufanikisha kazi zao za utume kwa namna iliyokua bora zaidi. Na walikua wanaweza kuyatatua matatizo yaliyokua yakiwakabili. Mitume wote walikua na sifa hizi. Tabia hizi ambazo zilifahamika kama "Sifa za mitume" kama:-

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"(Tumewatuma) wajumbe kama wabashiri wa habari njema na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungubaada ya kuletewa mitume....."

(al-Nisa 4; 165)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"...Na hapakua na watu pasina mwonyaji ali-yeishi mionganoni mwao(kipindi cha nyuma).

(Fatir 35; 24)

Sidq	Sifa ya kua na unyenyekevu, ukweli na haki kwa mitume katika maneno yao na matendo yao.	Mitume hawajawahi kusema uongo katika maisha yao. Ukweli ni tabia njema kabisa ambayo wametunukiwa binadamu wote. Ikiwa mmoja wa marafiki zetu akituambia uongo, hatuwezi kumwamini tena. Lakini tunawaamini na kuwaheshimu wale wanosema ukweli. Kwahiyu haiwezekani kabisa kumfikiria yoyote anayeleta ujumbe wa Mwenyezi Mungu na asiwe anasema ukweli ila uongo mara zote. Kwa ujumla watu hawawaamini nahawachukui mifano kutoka kwa watu wanaosema uongo ambao maneno yao na matendo yao hayaendani.
Amanat	Sifa ya uaminifu ya mitume	Mitume ni "amin" au watu waaminifu. Kwa sababu ya tabia hii, watu wanawaamini katika shughuli zao hapa duniani na katika masuala yanayohusiana na dini. Kwa kua watu wanaamini maneno ya mitume na tabia zao, waliwasikiliza na kujaribu kua kama wao.
Fatanat	Sifa ya mitume ya kua na akili na mtazamo wa hali ya juu.	Kwa kua na uwezo mkubwa sana wa kufikiria na kutoa maamuzi kwa uharaka, mitume waliletewa wahyi na kuupokea kwa uharaka. Kwa hiyo walitoa majibu yenyeye kuridhisha kwa maswali ya watu waliokua wakiongea nao.
Ismat	Sifa ya kutoenda dhambi	Mitume hawajawahi kutenda madhambi katika maisha yao yote. Haiwezi kufikirika kuwa walikua wakimshirkisha Mwenyezi Mungu, kuiba, kunywa vinywaji vyenye kilevi au uzinifu. Watu walikua hawakubali kabisa watu wenye tabia kama hizo na hawakuwachukua kama mifano kwao.
Tabligh	Sifa ya mitume kufikisha maamisho na makatazo yote waliyoyapokea toka kwa Mwenyezi Mungu.	Kila mtume alikua akifikisha amri zote kama zilivyoziwakea toka kwa Mwenyezi Mungu. Hata kama walipata vikwazo na mateso, mitume hawakurudi nyuma katika kulitekeleza jukumu hili. Mitume wengi walitishiwa kifo kwa kua walifanya jukumu hili. Baadhi yao kama Nabii zakaria na Yahya wao walikufa mashahidi.

UJUMBE WA KUFANANA WA MITUME WOTE

Kuna baadhi ya kanuni zisizobadilika katika ujumbe wa mitume kutoka kwa binadamu wa kwanza Nabii Adam hadi kwa mtume wa mwisho Mtume Muhammad(rehma na Amani ziwe juu yake). mitume wote waliwashauri watu kuamini kwa Mwenyezi Mungu, malaika wake, vitabu vyake, mitume wake na kuamini siku ya kiyama na hatima(Qadar). Ukweli, wema,

na kusaidia wengine ni kipimo cha maadili kilichokubalika kwa watu wote toka uumbaji wa mwanadamu. Kusema uongo, kumsingizia mtu maovu, Kamari, wizi, mauaji, kufanya uharibifu katika jamii vinaweza kusemekana kama tabia mbaya zisizokubalika. Tunaweza tukazijumuisha kanuni kuu katika vichwa vifuatavyo;



Kuilinda dini	Dini ni kipengele cha muhimu sana ambacho kinalinda uwepo wa jamii. Na hitajio muhimu la dini yenye nguvu ni Imani juu ya Mwenyezi Mungu. Hii ndio sababu ya mitume wote kuwakaribisha watu wake katika kuamini Mola mmoja na kumuabudu yeye pekee. Tauhid au kumpwekesha Mwenyezi Mungu umekua ujumbe kwa mitume wote.
Kulinda maisha	Maisha ya mwanadamu ni ya thamani sana. Kuutoa uhai wa mtu asiyekua na hatia ni dhambi kubwa sana. Kama inavyoelezewa katika Quran tukufu kuwa, "kuutoa uhai wa mtu mmoja asiyekua na hatia ni sawa na kutoa uhai wa binadamu wote."
Kuwalinda wenyewe akili	Aina zote za vyakula na vinywaji vinavyomfanya mtu kutofikiria na kutafakari sawasawa vimekatazwa. Hii ni sababu pombe na madawa ya kulevyia yamepigwa marufuku kabisa na uislam.
Kuilinda familia	Kukikuza kizazi chenye uaminifu na maadili mazuri inaweza kufikiwa tu kwa kulinda familia. Hii ni sababu dini yetu inakataza kila tabia isiyokua na maadili mazuri mfano, uzinifu jambo ambalo linasababisha uharibifu wa familia.
Kulinda mali	Kujitafutia kipato halali inakubalika kama jambo takatifu katika ujumbe wa mitume. Mali zinazopatikana kwa mtu kutumia nguvu zake mwenyewe na haki ya kupata Zaidi uko chini ya ulinzi huu mtukufu. Matendo na tabia hatarishi kama vile wizi, kula riba, kuiba na kula rushwa vyote vimekatazwa vikali katika uislam.

VITU TUNAVYOVIPATA KWA KUAMINI MITUME WA MWENYEZI MUNGU

MITUME

- Wametutambulisha dhana ya Mwenyezi Mungu mtukufu
- Wametufundisha jinsi ya kufanya ibada.
- Wametupa taarifa kuhusu makazi ya milele au akhera.
- Wamekua ni waanzilishi wa misingi ya ustaarabu.
- Wamekua ni mifano bora ya kuigwa kwa maadili na tabia zao njema.

Tunapochunguza ulimwengu, tunaweza tukaona ni kwa namna gani ulivyopangiliwa vizuri. Tunafikiri kwamba mpangilio huo sahihi hauwezi kutokea kwa bahati mbaya. Hivyo, tunafikia hitimisho kuwa ulimwengu huu na vyote vilivymomo ndani yake vimeumbwa na muumbaji. Lakini hatuwezi kuelewa ni nani hasa muumbaji huyo na sifa gani za muumbaji anazo kwetu. Mola wetu anayetujua sisi vema kuliko sisi wenyewe hakuwahi kuacha kutusaidia na kutuonea huruma katika hili. Aliwateua baadhi ya waja wake kama wajumbe wake. Wajumbe hawa ni waongozaji watukufu **na ndio wao waliotutambulisha dhana ya Mola mtukufu.**

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"(Ibrahim alisema kuwaambia watu wake) hakika hayo (masanamu) ni maadui kwan-gu, na pia kwa Mola wa walimwengu aliyeniumba mimi, kisha akaniongoza katika njia, na anayenipa mimi chakula na anayenipa mimi kinywaji, na ninapokua na maradhi ndiye anayeniponya na ndiye atakayenitaka mimi kufa kisha akanipa tena maisha.

(al-Shuara 26; 77-81)

Kama binadam, tunatakiwa kujua kua tupo katika ulimwengu huu, na tunatakiwa tujigundue wenyewe na Mola wetu aliyeumba kila kitu katika ulimwengu huu. Tunapata hisia za kuomba, kuswali, kusoma dua na kumuabudu yeye ambapo hatutawezza kutambua jinsi ya kumuabudu sisi wenyewe. Ndio maana Mwenyezi Mungu akawachagua wajumbe wake kutekeleza jukumu hili. Mitume ni mifano yenyewe kuishi inayotuonyesha jinsi ya kumuabudu Mola wetu. Wao ndio **waliotufundisha jinsi ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu.**

Mtume wetu amesema:

"Swalini kama mnavyoniona mimi ninavyoswali"

(Bukhari, Ahad, 1)

Vitabu vitukufu na mitume ndio vyanzo vyetu pekee vya maarifa kuhusu maisha baada ya kufa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuma taarifa kuhusu akhera kupitia mitume wake. Mitume wanatupa habari kuhusu mambo yatakayotokea akhera. Wanatupa habari njema za thawabu zinazowasubiri wale walimuamini Mwenyezi Mungu na kufanya matendo mema. Waliokuwa pia wakiwaonya wale waliokua hawamuamini Mwenyezi Mungu na akhera kwa kutukumbusha kuhusu adhabu zinazowangojea. Mitume ni waongozaji wetu hapa duniani na **wanatupa habari kuhusu makao ya miele au akhera.**

Kipenzi chetu Bwana Mtume amesema:

"Mola wenu mlezi ataongea na kila mmoja na hapatakuawepo na mtafasiri. Mmoja wenu antaangalia upande wake wa kulia na ationa matendo yake mema na kushoto ationa matendo yale maovu. Na kisha atatizama mbele yake hatooma kingine chochote isipokuwa Moto wa jahanamu. Kwa hiyo yoyote (kila mmoja wenu) ajinasue mwenyewe na moto japo kwa kutoa kipande cha tende kama (sadaka)."

(Bukhari, Zakat, 9)



Mitume walikua ni viongozi na uongozi wao ulikua unasaidiwa na wahyi. Na walijihuisha na Sanaa, kilimo, biashara, na shughuli nyingine. Hivyo walileta mchango katika utamaduni na ustaarabu. **Walikua ni waanzalishi wamisingi ya ustaarabu ambapo watu waliishi kwa amani na utulivu.** Walijaribu kuwafanya wale waliokua wakiwafuata wawe na furaha hapa katika dunia na akhera. Miogoni mwa mifano iliyotolewa na Quran tukufu ni ule wa Nabii Nuhu (Amani iwe juu yake) alijua namna ya kuunda meli na Daudi (Amani iwe juu yake) alifahamu kuyeyusha na kutumia chuma."



Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"...Tumekifanya chuma laini kwake (Daudi) tukamwambia tengeneza (nguo za chuma pana) na kadiria sawa katika kuunganisha na tendeni mema..."

(Saba, 34;10-11)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"(Ewe Nuhu!) tengeneza safina/meli mbele ya macho yetu na kwa mujibu wa ufunuo wetu..."

(Hud 11; 37)

Familia zetu na mazingira yana athari kubwa katika kutengeneza mienendo mema na tabia zetu. Toka utotoni tumewafanya baba zetu, mama, walimu, watu wazima na vipenzi vyetu kama mifano katika maisha yetu. Tunaathirika kwa matendo yao na kujaribu kufanya kama wao. Mola wetu mtukufu amewatuma mitume wake ili wawe vigezo kwetu.

Mitume wanatufundisha ukweli, haki, uaminifu, nguvu, rehema, upole, usamehevu, na huruma. **Wamekua mifano bora kabisa kwetu kwa maaadili na tabia njema..**

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Kwa yakini kwao ni mfano bora kabisa kwenu nyinyi kuufuata..."

(Mumtahina 60; 6)

MIFANO BORA KWETU INAPATIKANA KATIKA MAISHA YA MITUME

Mwenyezi Mungu mtukufu ameyaweka maisha na maadili mema ya mitume kama mifano bora kwa binadamu wote.

Hadithi za mitume zilizotajwa katika Quran pia ni ushahidi wa utume wa Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) kwa sababu alikua "Ummi" yani (Asiyejua kusoma wala kuandika). Isingekua rahisi kwa mtu asiyejua kusoma wala kuandika kuelezea habari za maisha ya mitume tena walioishi karne nyingi zilizopita kwa ufasaha. Ni lazima alikua anajifunza habari hizi katika chanzo chenye kuaminika au ni lazima awe amefundishwa. Chamzo hiki ni Mwenyezi Mungu mtukufu na wahyi wake. Ukweli huu unaelezewa katika quran kama ifuatavyo:

"Na kwa hakika tumewatuma mitume kwenu, wapo baadhi tuliovataja kwenu na wapo baadhi ambao hatujawataja kwenu..." (Mu'min 40; 78)

Kwa kifupi kabisa tuangalie mitume walioorodheshwa katika Quran:

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Katika hadithi zao(mitume) hakika kuna mafunzo kwa watu wenye kufahamu....."

(Yusuf 12; 111)

ADAM (Amani iwe juu yake)

Ni binadamu wa kwanza na ni mtume wa kwanza. Mwenyezi Mungu mtukufu alimfundisha majina ya kila kitu na jinsi ya kuongea.

Mwenyezi Mungu mtukufu aliwaamuru Malaika wake kumsujudia Adam kama ishara ya heshima. Malaika wote walimsujudia kwa heshima isipokua shetani hakutii amri hiyo kutokana na wivu. Shetani alidhamiria kweli kuwapoteza binadamu katika njia iliyonyooka. Mola mtukufu akampa kibali hicho cha kuishi hadi siku ya hukumu na kuwatahadharisha watu kua makini sana na mitego ya shetani. Adam na mkewe Hawa walishawishiwa na shetani na wakala katika matunda ya mti uliokatazwa wakati wakiishi peponi. Na matokeo yake walishushwa katika dunia. Adam na Hawa mara moja wakagundua makosa yao kwa kuwa warerubuniwa na maneno ya shetani. Mara moja walianza kuomba msamaha kwa ukaidi wao. walikua wakilia kwa miaka mingi sana. Kuomba msamaha, walisujudu kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Mwisho Mwenyezi Mungu mtukufu alipokea toba yao na akawasamehe.

Maisha ya nabii Adam ni muhimu sana kuelewa binadamu ni wa heshima na thamani kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Msamaha walioonyeshwa Adam (Amani iwe juu yake) na Mwenyezi Mungu baada ya kula tunda la mti uliokatazwa inaonyesha huruma ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake. Kwa namna hii Mwenyezi Mungu alimfundisha binadamu namna ya kufanya toba.

Adam (Amani iwe juu yake ni mfano bora kwetu kufanya toba kwa madhambi yetu na kuomba msamaha kwa Mola wetu.

NUHU (Amani iwe juu yake)

Nuhu (Amani niwe juu yake) ni mmoja wa mitume waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu kama kiongozi kuonyesha njia iliyosahihii kwa watu wote. Watu wa Nuhu (Amani iwe juu yake) walikua wameiacha njia iliyooonyeshwa na mitume wa mwanzo. Watu wenyehe nguvu walikua wanawakandamiza wale wanyonge. Watuwalianza kuabudia masanamu waliyoyatengeneza kwa mikono yao wenyeewe. Nuhu aliwaita tena warudi katika imani ya Mwenyezi Mungu mmoja. Alijitahidi kila njia kuwaonyesha watu wake njia iliyonyooka na kuwafanya wamuabudu Mwenyezi Mungu. Watu walimdhalilisha na kumkejeli, lakini hakuwahi kurudi nyuma kulitekeleza jukumu lake. Alijaribu kuwafundisha watu kuhusu dini ya Mwenyezi Mungu kwa takribani miaka 950. Usiku na mchana aliwafundisha watu kuhusu ukweli. Alijaribu kila njia iwezekanayo kuwaonyesha watu njia ya haki, lakini ni watu wachache pungufu ya mia moja walimuamini.

Wasioamini walikua na majibizano mengi nayeye. Walifanya kila kitu kumuumiza. Wakati Nuhu (Amani iwe juu yake) akiwahofisha juu ya adhabu ya Mwenyezi Mungu, walimdharaau na kusema:

"Ewe Nuhu! Tuletee sasa juu yetu hilo unalotutishia nalo, kama wewe unasema ukweli."

Nuhu alikua na huzuni sana kwa kile ambacho watu wake walikua wanafanya. Mwisho Mwenyezi Mungu alimuamuru atengeneze meli na kuwaingiza wale walioamini pamoja naye pamoja na jozi moja ya kila mnyama. Kisha ikaanza kunyesha mvua kwa miezi kadhaa. Maji yalijaa dunia yote. Nuhu nawaliomuamini walinusurika na mafuriko kwa kuingia ndani ya safina. Hali ya kuwa wale waliokua hawajamuamini na kumkejeli kwa kumwambia, "Tuletee sasa juu yetu hilo unalotutishia nalo" waliangamizwa na mafuriko. Baada ya mvua kuacha kunyesha safina ya Nuhu ilitua katika mlima Judi. Nuhu (Amani iwe juu yake) pamoja na wale alicoua nao walishuka salama toka katika safina.

Watu hawa pamoja na jozi zile za wanyawa walitawanyika ulimwenguni na kuanza tena kuzaliana. Hi ni sababu Nuhu (Amani iwe juu yake) anajualikana kama "Baba wa pili wa walimwengu"

**Jitihada na uvumilivu wa Nuhu
katika njia ya ukweli ni mfano
mzuri kwetu.**



Ibrahim (Amani iwe juu yake)

Nabii Ibrahim ni mtume mkubwa aliyeitwa na Mwenyezi Mungu kama "Khalil" au rafiki. Katika umri mdogo nabii Ibrahim alianza kuhubiri kwa watu uwepo na upweke wa Mwenyezi Mungu. Ingawa watu wa mji wa Babylon kuanzia baba yake Azar, hawakumwamini. Japokua baba yake alimdhalilisha na kumfukuza mbali, alimchukulia baba kwa uzuri kabisa.

Ibrahim alipingana na Nimrod mfalme wa zama zake. Kwa kuamini mali zake na uhuru Nimrod alijitangaza yeye mwenyewe kama mungu. Aliwatesa wale ambao hawakua wamekubaliana na madai yake. Ibrahim (Amani iwe juu yake) alimlingania Nimrod katika dini ya kweli. Alijaribu kumshawishi Nimrod akate tamaa juu ya uungu wake. Alimuomba Nimrod kumuamini Mwenyezi Mungu aliyeviumba vyote ambavyo havikuepo, anayeua kila kitu na kukipa uhai kwa mara nyingine tena. Nimrod alidai kua anaweza kufanya kama hivyo. Aliwaita mabwana wawili mmoja akamuhukumu kuuliwa na mwagine akasamehewa. "Tizamalninaua na kutoa uhai, alisema. Mara hii Ibrabim akamwambia:

- "Mwenyezi Mungu anatoa jua kutoka mashariki kwanini wewe usilitoe kutoka magharibi?" Nimrod alishtushwa na swali hilo.

Ilikua ni siku ya tafria. Watu walikuja kwa tukio la tafria. Ibrahim akajua kua hii ilikua nafasi yake, hivyo akaenda katika jumba la masanamu na kuyavunja yote isipokua lile lillokua kubwa Zaidi. Kisha akatundika shoka katika bega la sanamu mkubwa.

Watu walipokuja toka kwenye tafria, walifadhaika sana kukuta kilichotokea katika nyumba ya masanamu yao. Walimkumbuka Ibrahim na maneno aliyokua akiyasema kuhusiana na masanamu yao. Hivyo wakamuita Ibrahim na kumuuliza:

- "Ewe Ibrahim! Je ni wewe ndiye uliyefanya haya kwa miungu wetu? Ibrahim (Amani iwe juu yake) akajibu:

- "Huenda sanamu hili kubwa ndilo lilihofanya hayo kwa wenzake, liulizeni kama linaweza kuongea. Watu ilikua wadhihirishe ya kua masanamu hawakuwa viumbe wenyewe maisha na walikua hawawezi kuongea. Hapo ndipo Ibrahim akawakumbusha kuhusu Imani ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa kusema:



- "Kisha kwanini mnajitenga mbali na Mola mmoja na wa pekee na kuabudu hawa masanamu ambayo hayawapi faida wala hayawadhuru kitu? Aibu juu yenu na aibu juu ya kile mnachokiabudu! Je! Hamtii akilini?"

Japokua wanaoabudu masanamu hawakua na la kujibu kutokana na swali hilo la msingi, hawakuachana na njia yao potofu. Wakakubaliana kumtupa na kumuunguza Ibrahim katika moto.

Moto mkubwa sana ulianza kuandaliwa. Ibrahim(Amani iwe juu yake) akatupwa motoni kwa kutumia manati kubwa. Lakini Mwenyezi Mungu mmiliki wa kila kitu akasema, "Ewe moto, kua bariidi na salama kwa Ibrahim" (al-Anbiya 21:69). Moto ultii sharti hilo na haukumuunguza Ibrahim. Watu walistaajabu sana kuona kua moto haukumuunguza Ibrahim.

Baada ya tukio hili Ibrahim alitoka Babylon na kwenda Misri na Jerusalem. Alianzisha maisha yeye na mke wake Sarah. Pia alikua na mke wake mwagine Hagar na mwanae mdogo Ismail wakiishi katika bonde la Makka. Pamoja na kijana wake Ismailinalijenga Ka'aba Makka. Umoja(upweke au tawhid) ilikua ni misingi ya dini iliyoletwa na Ibrahim(Amani iwe juu yake).

Ibrahim (Amani iwe juu yake) ni mfano mzuri kwetu katika kutathmini juu ya ulimwengu na kua na mtazamo kuhusu uwepo wa Mwenyezi Mungu.

YUSUF (Amani iwe juu yake)

Yusuf alikua ni mmoja wa watoto wa nabii Yaqub (Amani iwe juu yao). Alikua ni mzuri wa sura na kijana mwenye aklili sana. Alipokua mtoto kaka zake walikua na wivu dhidi yake na kumtupa katika kisima jangwani. Kisha wakaongopa kwa baba yao wakisema, "Yusuf ameliwa na mbwamwitu". Msafara ulikua ukichota maji katika kisima ukamkuta Yusuf. Wakamchukua hadi katika kasri ya mtawala wa kimisri(waziri) na wakamuza kama mtumwa. Alizushiwa ndani ya kasri na kupelekwa magereza pasina hatia. Yusuf (Amani iwe juu yao) alikaa gerezani katika miaka yake ya ujana.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimjaalia Yusuf uwezo wa kutafsiri ndoto. Alikua akiwatafasiria



ndoto wafungwa wenzake na kisha kuwalingania katika kumuamini Mola mmoja na kuamini akhera. Usiku mmoja Mfalme wa Misri aliota ndoto yenze kuvutia sana. Hakuna aliyeweza kuitafsiri ndoto ile. Mfungwa wa zamani aliyekua kafungwa pamoja na Yusuf alimwambia Mfalme wa Misri kua Yusuf(Amani iwe juu yao) anaweza kuitafsiri ndoto yake. Nabii Yusuf (Amani iwe juu yake) aliitafsiri ndoto ya Mfalme vizuri sana. Alisema kua kutakuja kua na njaa mbaya miaka ijayo, japo watu wataishi kwa msaada wa kuchukua tahanadhi. Mfalme alipenda sana tafsiri hii. Ndipo akagundua pia Yusuf alikua gerezani kwa makosa. Hivyo akamtoa Yusuf gerezani na kumpa majukumu katika hazina zake.

Nabii Yusuf (Amani iwe juu yake) aliwatambua kaka zake walipokuja Misri kuchukua ngano katika kipindi cha miaka ya njaa. Aliwalika wazazi wake na kaka zake waje Misri kuishi pamoja naye. Alionyesha msamaha mkubwa na upendo wa hali ya juu.

Hadithi ya maisha ya nabii Yusuf inaelezewa katika Quran. sura kuhusu Yusuf (12) inahusika na baadhi ya hali ya hisia kama vile utengano na muungano ambao kila binadamu anaweza akapitia katika maisha yake. Pia inazungumzia kuhusu ni namna gani ambavyo wivu unaweza ukapelekea katika maovu. Matokeo ya maradhi ya uzushi pia yameelezewa katika sura hiyo.

MUSSA (Amani iwe juu yake)

Mussa (Amani iwe juu yake) ni mionganini mwa miotume waliotumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa wana wa Israel.

Wana wa Israel, amabao walitokea katika kizazi cha nabii Yaqub, walliishi Misri katika kipindi cha Nabii Yusuf. Kwa wakati huo walipoteza sifa yao Misri na wakaanza kutumikishwa kama watumwa.

Watawala wa Misri walikua wakiitwa mafarao. Farao aliyekua madarakani wakati Mussa alipokua anazaliwa alikua ni mtu katili sana. Aliamuru kua watoto wote wakiume watakaozaliwa na wazazi wa kiisrael wauawe. Mwenyezi Mungu mtukufu alimuamuru mama yake Mussa amuweke mtoto wake katika kikapu na kumtia katika mto Naili. Mwenyezi Mungu alimuambia kua mtoto wake atakwenda kulelewa katika kasri ya kifalme na baadaye atakuja kua mtume. Ndipo mama yake Mussa akamuweka mtoto wake katika kikapu na kikitosa mtoni. Mke wa farao alikichukua kikapu kile na kwenda nacho ndani ya kasri. Hivyo farao alikwenda kumlea na kumtunza mtu ambaye atakuja kusimama mbele yake kupinga matendo yake maovu na kumuhubiria habari za Mwenyezi Mungu katika kasri yake mwenyewe.

Kipindi cha utoto wa Nabii Mussa ulipita akiwa katika kasri. Kipindi cha ujana wake alitoka kwa muda na kwenda kuishi kwa nabii Shuaybu huko Madiani. Alipokua anarejea Misri, na mke wake na familia yake, alipokea wahyi wakwanza katika mlima Sinai. Kwahiyo alichaguliwa na alitunukiwa na Mwenyezi Mungu miujiza mbalimbali. Aliamriwa kuswali swala zake na kumlingania farao katika njia iliyonyooka. Kaka yake Haruni aliteuliwa kama msaidizi wake.

Mussa pamoja na kaka yake Haruni (Amani iwe juu yao) walismama dhidi ya farao katili na kumueleza habari za Mwenyezi Mungu na amri

**Nabii Yusuf ni mfano mzuri kwetu
kuhusu kuwasamwehe wale
wanaotudhuru na kulipiza ubaya
kwa wema.**



zake. Farao alikua na kiburi na mtu mwenye majigambo kwa wengine. Alidhania ya kua yeye anamiliki kila nguvu na alikua akimuasi Mwenyezi Mungu. Mussa alionyesha miujiza ili kumfanya aamini, lakini farao hakuamini na kusema kua miujiza ile ilikua ni matendo ya kichawi. Kwa hiyo alimtaka Mussa kushindana na wachawi. Nabii Mussa (Amani iwe juu yake) akakubaliana na wazo hilo. Wachawi wa farao wakaanza kwa kutupa Kamba na vijiti vyao katika ardhi. Waliwadanganya watu waliokuwepo katika eneo hilo na Kamba na vijiti vyao vikageuka na kua kama nyoka.

Mussa alitupa firbo yake ardhini pia. Na ikabadiika na kuwa joka kubwa liliowameza vijoka vyote vidogo. Wachawi walishatuka sana na kumoromoka na wakasujudu, wakakiri kumuamini Allah. Farao aliwatishia, lakini hawakubalidi msimamo wao katika Imani yao. Walikufa mashahidi kwa kukatwa mikono na miguu yao katika pande tofauti.

Waisraeli walipogundua kua farao anataka kumuua Mussa na waumini wote, waliondoka Misri chini ya uongozi wa Mussa (amni iwe juu yake). Mussa na wana wa Israel walikwama

baina ya bahari ya shamu upande wa mbele na jeshi la farao upande wa nyuma yao. Mwenyezi Mungu Mtukufu akafanya muujiza na kuigawanya bahari pande mbili na kufungua njia kwa waumini kupita. Baada ya waumini kupita katika njia ile, firauni na majeshi nyake wakajaribu kupita katika njia ile. Mara tu baada ya firauni na majeshi yake kuingia katika njia ile, hata hivyo ilijifunga na waliteketea ndani ya bahari.

Mussa (Amani iwe juu yake) alipigana na farao na wana wa Israel waliweza kuepuvu vitimbi na mateso ya farao. Mussa alitumia muda wake uliobaki katika kuwafundisha wana wa Israel kuhusiana na taurati na kanuni zake.

Maisha ya Nabii Mussa (Amani iwe juu yake) ni mfano mzuri kwetu jinsi ya kupigana na watu wanyanyasaji na wasiokua na shukurani.

Yesu / ISSA (Amani ikwe juu yake)

Bi Mariamu alikua ni mmoja wa wana mionganini mwa familia ya Imran ambaye aliyeletwa kwa watu kama mfano na Mwenyezi Mungu mtukufu. Mke wa Imran bi Hanna alimtoa mtoto wake aliye kua anatarajia kumpata katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alipojifungua mtoto wake, Hanna alimuuta Mariam. Kisha akatekeleza ahadi yake na kumtoa mtoto wake kufanya shughuli katika msikiti wa Al-aqsa. Mariam alilelewa kama mwanamke mtawa chini ya usimamizi wa mume wa shangazi yake aliyeitwa Zakariya.

Mariam alikua akiutumia muda wake kwa kufanya ibada katika chumba chake alichotengewa katika masjid Al-Aqsa kwa kuutunza na kuufanya usafi msikiti. Siku moja malaika Jibril alikuja kwa Mariam na kumwambia kua Mwenyezi Mungu mtukufu atamjaalia mtoto wa kiume. Mariam alilezea alivyokua msafi na aliuliza ni kwa namna gani hayo yatawezekana hali ya kua yeye alikua bikira. Malaika Jibril akamwambia kua chochote akitakacho Mwenyezi Mungu hutokea. Hivyo Issa (Amani niwe juu yake) alizaliwa kwa muujiza pasina baba.

Wana wa Israel hawakuamini uzao wa Yesu toka kwa mwanamke bikra na wakamtuhumu Mariam na kusema "amefanya jambo la aibu sana." Baada ya hapo mama yetu bi Mariam alikua akimnyoshea kidole mtoto mchanga aliyezaliwa na kuwataka watu kuongea naye. Muda si mrefu ambapo wana wa Israel walisema kua watoto hawawezi kuongea ndipo muujiza mwagine ukatokea na mtoto akaanza kuongea:

"Alisema: kwa hakika! Mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu; amenipa kitabu na kunifanya kua nabii; na amenifanya mbarikiwa popote ninapokua, amenlamrisha kushika swala na zaka maadamu ni hai. Na mama yangu anastahili wema, wala hakunifanya jeuri, mwovu; Amani iko juu yangu siku nillyozaliwa, siku nitakapokufa na siku nitakapofufuliwa hai. Huyo ndiye Yesu

(Issa), mwana wa Mariam (Haya ni) maneno ya ukweli kuhusiana na kile walichokua wanashaka nacho. Haifai(ukuu) wa Mwenyezi Mungu ya kua alijifanyia mtoto. Utukufu ni wake Mwenyezi Mungu! Anapotaka kitu anakiambia tu Kuwa! nacho Huwa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na Mola wenu pia, hivyo basi muabuduni yeye na hii ni njia iliyonyooka." (Maryam 19; 30-36)

Kama ilivyokua kwa Mwenyezi Mungu kumuumba Adam bila baba wala mama, alimuumba "Issa" Yesu bila baba. Katika umri wa miaka thelathini(30) Yesu(Amani iwe juu yake) alipewa jukumu la utume na miujiza kadhaa wa kadhaa. Lakini, ni watu wachache tu walioitwa Hawaris au wanafunzi. Ndio waliomwamini.

Mayahudi walitaka kuzuia Yesu na wanafunzi wake wasieneze ujumbe waliokuja nao, hivyo walikubaliana kumuua. Lakini, Mwenyezi Mungu mtukufu alimuepusha nao. Mayahudi walimkamata mmoja aliye fanana na Yesu (Amani iwe juu yake) na kumtundika msalabani. Wakasema kuwa wamemuua Yesu "Issa" mwana wa Mariam. Hali ya kua hawakumuua Issa ila mtu mwagine aliye fanana naye. Mwenyezi Mungu mtukufu alimpaliza mbinguni.

**Kuna mifano mingi sana kwetu sisi
juu ya tabia njema za nabii Issa, hur-
uma yake, utayari wake wa kujenga
urafiki mionganini mwa watu na kuta-
kasa nafsi zetu.**



MUHAMMAD (Rehma na Amani ziwe juu yake)

Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) ni mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu. Mola wetu mtukufu amesema yeye ni mtume wa mwisho katika surat Ahzab 33:40: "...lakini ni mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa manabii..."

Kabla ya Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuchaguliwa kua mtume wa Mwenyezi Mungu, watu walikua wamepotea katika njia iliyonyooka. Maadili yalikua yamepungua. Unyanyasaji na dhalma vilikua vimeenea kwa kasi. Wenye nguvu walikua wanawanyanya wanyonge. Watu walikua wametopea katika vinywaji vyenye ulevi na Kamari. Wizi na unyang'anyi kwa wengine vilikua ni vitu vya kawaida. Watu walikua wanasubiria kiongozi kuwaonyesha kipi kizuri na kipi kibaya, kuwatoa gizani na kuwaleta katika nuru. Ndipo sasa Muhammad(rehma na Amani ziwe juu yake) alitumwa kama mtume kwa watu.

Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) alizaliwa Makka mwaka 571. Mama yake alilitha Amina na baba yake alilitha Abdullah. Baba yake alifariki kabla Bwana Mtume hajazaliwa. Mtume wetu alipelekwa kwa mama wa kunyonya aliyeitwa Bi Halima muda mfupi baada ya kuzaliwa. Alikua na siku za furaha sana kwa Bi Halima. Alipokua na miaka saba, mama yake mzazi Bi Amina alifariki dunia. Baada ya kifo cha mama yake Mtume wetu alichukuliwa na kuishi kwa babu yake Abdulmuttalib. Alipokufa baada ya miaka miwili, baba yake mdogo Abu Talib alimchukua kumtunza. Maisha ya utoto ya Mtume(S.A.W) yalipita akiwa kwa baba yake mdogo. Mtume wetu alikua akimsaidia baba yake mdogo kazi za kila siku. Aliwahi kuchunga wanyama wa baba yake mdogo. Alikua mtoto wa tofauti na watoto wengine. Hakuwahi kusema uongo wala kuabudu masanamu.

Mara zote alikua akikimbilia kuwasaidia wenzake. Watu wote walimuamini. Hii ni sababu malaika Jibril alimuita "Muhammad al-amin au Muhammad mwenye kuaminika."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na hatukukutuma wewe (Muhammad) uwe mbashiri na mwonyaji kwa watu wote...."

(Saba' 34; 28)



Mtume wetu (Rehma na amani ziwe juu yake) alifanya biashara pamoja na baba yake mdogo Abu Talib kipindi cha ujana wake. Aliflikia umri wa miaka ishirini na tano(25) alimuoa bi Khadija

Mtume wetu (Rehma na amani ziwe juu yake) alipofika umri wa miaka arobaini(40) alianza kujitenga na kukaa katika jabal hira karibu na Makkah. Siku moja kipindi cha mwezi wa Ramadhan alipokua katika jabal Hira, alijiwa na malaika Jibril (Amani iwe juu yake) na kumtaarifu kua amechaguliwa kama mjambe wa Mwenyezi Mungu. Mtume wetu alimwambia kila kitu mkewe bi Khadija. Na mara moja alimuamini. Baada ya Khadija Ali, Abu Bakr na Zaidi(Mwenyezi Mungu awe radhi nao) wakawa nao waislam.

Kisha Mtume wetu aliwaalika watu wa Makkah kuupokea Uislam. Japokua, baadhi yao walimuamini, wengi katika watu wa Makkah hawakumuamini. Walianza hata kuwataabisha waumini. Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na wale walioamini walivumilia katika kila namna ya mateso. Jukumu la Mtume katika mji wa Makkah liliendelea kwa miaka kumi na tatu (13).

Ili kuishi kwa mujibu wa Uislam na kuufikisha ujumbe wake, Mtume pamoja na waumini wengine walihamia mji wa Madina mwaka 622. Mtume wetu aliishi Madina kwa miaka 10. Katika miaka hii waumini walijenga msikit

Madina. Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alitangaza hali ya udugu kati ya waumini wa Madina(ansar au wasaidizi) na wahamiaji wa Makkah (Muhajirun). Aya za Quran zilizohusisha maisha ya kijamii ziliteremka katika zama hizo. Hivyo matendo mengi ya ibada mfano kutoa sadaka, kifunga na kuhiji yalitangazwa lazima katika kipindi hiki.

Mtume wetu (Rehma na amani ziwe juu yake) alituma wajumbe kwa viongozi wa nchi za jirani na kuwakaribisha katika uislam. Mwaka 630 aliivamia Makkah na kuharibu masanamu yote ndani ya Ka'aba. Uislam ukasambaa sehemu zote kuzunguka ghuba ya uarabuni. Mwaka 632 alifanya hija ya mwisho na alitoa hotuba maarufu iliyobeba ujumbe muhimu kwa watu. Katika mwaka huo huo alipokua na umri wa miaka sitini na tatu(63) alifariki dunia akiwa katika mji wa Madina.

Kipenzi chetu Bwana Mtume ni mtumishi maarufu zaidi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mola wetu Mtukufu amezisifia tabia zake njema na ametuamuru sisi katika Quran kumfanya yeye mfano wetu katika kila Nyanja katika maisha yetu kwa kusema: "Hakika mnaye mtume wa Allah mfano bora kabisa, kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, kisha akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." (Ahzab 33; 21)



**Kipenzi chetu Mtume ni mtu wa mfano aliyebeba
maadili mazuri na tabia njema za mitume wote
waliotangulia.**

Ewe Mola wetu! Muumba wa viumbe wyote viliyopo ardhini na mbinguni! Umechagua mitume miongan mwa binadamu na kuwatuma kqwetu kama mifano. Tunafungua mikono yetu kwako na tunakuomba wewe! Mola wetu mlezi! Tujaadie juu yetu sisi furaha kua kama mitume.	Adam	Aliyeomba msamaha wa dhati kwa madhambi yake
	Idris (Enoch)	Aliyepalizwa katika mbingu za juu
	Nuhu	Aliyefanya kila kitu kuitangaza dini yako
	Hud (Eber)	Aliyesimama kwa ajili ya wanyonge na wenye uhitaji dhidi ya wanyanyasaji
	Saleh	Aliyewatembelea wagonjwa na kuwahudumia masikini na wenye uhitaji
	Lut	Aliyejitalihidi kuzuia upotofu wa maadili
	Ibrahim	Aliyenyenyekeea amri zako
	Ismail	Aliyeonyesha jithada kuyatoa maisha yake kwa ajili yako
	Ishaqa	Aliyewaonyesha watu njia iliyonyooka
	Ya'qub	Ambaye hakukata tamaa kwako
	Yusuf	Aliyekua mwanaume msafi
	Shu'ayb	Aliyekua mwaminifu
	Mussa	Ambaye hakua na uoga kuwaambia ukweli wakandamizaji na wasiokua na shukuran
	Haruni	Aliyewasaidia waliofuata njia iliyonyooka
	Daudi	Aliyekua na shauku ya kukuabudu wewe
	Sulaiman	Aliyetumia mali yake yote katika njia yako
	Ayyub (Job)	Aliyekua na subra
	Dhu'l kifl	Aliyekua anakumbuka miomgoni mwa waja wema kaika uwepo wako
	Yunus	Aliyekukumbuka wewe katika hali zote ya utajiri na umaskini
	Il'yas	Aliyekukumbuka wewe kwa mazuri
	Al-yasa	Aliyekua miongan mwa waja wema
	Zakariya	Aliyekua anakuabudu wewe kwa unyenyekevu
	Yahya(yohana mbatizaji)	Aliyekufa shahidi katika njia yako.
	Yesu/Issa	Aliyejitatasa moyo wake na maasi
	Muhammad	Aliyezipamba tabia zake kwa maadili ya Quran.

Amani iwe juu yake

MTUME WETU KATIKA WAHYI WA MITUME WENGINE

Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) ni mtume wa mwisho kutumwa kwa watu. Wakati mitume waliotangulia walikua wanatumwa kwa kundi maalum la watu au taifa la wakati wao, **Mtume wetu alitumwa kwa walimwengu wote ukijumuisha wale watakaokuja hadi siku ya mwisho.** Ndio maana Mtume wetu alituma barua na wajumbe kwa baadhi ya nchi na miji katika maisha yake kufikisha ujumbe wa Uislam. Kwa mfano aliwaalika watawala wa wawili toka katika falme zenyne nguvu sana kwa wakati huo Persia na Byzantium. Aliwataka kuukubali uislam pamoja na watu wao. Leo kuutangaza

ujumbe wake mtukufu kwa ulimwengu wote na kuwafikisha watu ni jukumu la wanaomfuata.

Mitume walichaguliwa na Mwenyezi Mungu mtukufu walifanya kazi kwa nguvu na furaha kwa watu. Walikua wakisema "malipo yetu tunayapata toka kwa Mwenyezi Mungu mwenyewe" **Hawakuhitaji gharama yoyote toka kwa mtu yoyote katika kazi yao.**" Mtume wetu kipenzi pia alitekeleza kazi zake kwa ufanishi mkubwa na hakika alikua anaishi kwa mujibu wa mfumo wa maisha ulioamrishwa ndani ya Quran tukufu. Alionyesha jitihada ya hali ya juu na kufanya kila aina ya sadaka kwa ajili tu ya jukumu lake. Na aliunda jamii yenye

Amani na mfano wa kuigwa katika mwanga wa aya za Quran.

Ni jukumu la mitume wote kuwaalika watu kwa Mwenyezi Mungu na kuwaonyesha njia iliyonyooka. Tunasoma maisha ya mitume na mambo waliyokua wakiyafanya kwa watu katika Quran tukufu. Na pia tumejifunza ukweli usio na ukomo na tabia njema. Mitume wote ni wajumbe wanokuja kutoka katika chanzo kimoja na kuwaita watu kwenye ujumbe unaofanana.

Kipenzi chetu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alielezea kwamba, "mitume wote watatoka katika chanzo kimoja, dini yao ni dini inayofanana na uhusiano kwa kila mmoja ni kama ndugu wa mama mmoja." Ndio maana mitume waote toka kwa Nabii Adam hadi kwa Mtume Muhammad (Amani iwe juu yao) walifafanua na kusaidiana kwa kila ujumbe wa mmoja. Hakuna mtume aliyetofautiana na mitume wengine. Kipenzi chetu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) kwa kutumia mfano ufuatao ya kuwa mitume wote walifafanua ujumbe wa mwengine:

"Muendelezo wangu unafana na ule wa mitume waliokuja kabla yangu, ni sawa na mtu aliyejenga nyumba bora na nzuri, isipokua kwa tofali moja katika kona. Watu watazunguka na kuishangaa uzuri wake,lakini watasema: "Ingekua nzuri Zaidi endapo hili tofali lingewekwa mahali pake?" hivyo basi mimi ndiye lile tofali na mimi ni mtume wa mwisho."

(Bukhari, Manaqib, 18)

Kipenzi chetu Mtume alikua akiwakumbuka mitume wa mwanzo kwa upendo na heshima. Alipokua akitaja majina yao alikua akiongezea kionjo cha "mtume wa Mwenyezi Mungu" au "kaka yangu." Kwa mfano mara moja alipokua anazungumzia juu ya Nabii Mussa, alianza maneno yake kwa kusema "kaka yangu Mussa."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Sema: mtii'ni Mwenyezi Mungu na mtii'ini Mtume. Na mkikengeuka, basi yaliyo juu yake na aliyobebeshwa, na yaliyo juu yenu na mliyobebeshwa nyinyi. Na mkimtii ye ye mtaongoka. Na hapana juu ya mtume ila kufikisha ujumbe wazi wazi."

(Nur 24; 54)

Alipokua anarudi kutokea Taif, alimuuliza mtumwa mkristo Addas ni wapi alipokua anatokea. Alipokua anamjibu kuwa anatokea Ninova(Mosul), Mtume akamwambia Addas "unatokea katika mji wa kaka yangu Yunus?" kisha akaongezea Addas na kumkaribisha kuamini upweke wa Mwenyezi Mungu. Addas aliupokea mwaliko wake kwa uwazi na kuingia katika Uislam.

Kipenzi chetu Mtume alikua akitoa mifano ya kutoka kwenye maisha ya mitume wa mwanzo. Alikua akiwatia moyo umma wake kufuata mifano hii na kuishi maisha ya usafi kama waliyokuanayo mitume. Kwa mfano alitoa mfano wa Nabii Daudi, aliyejipatia kipato chake kwa njia ya kufanya kazi za mikono, alielezea kwamba "**kipato halali na kizuri ni kile ambacho mtu anakipata kwa mikono yake mwenyewe.**" Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) aliwashauri wale waliyokuwa wanataka kufunga Zaidi ya mwezi wa Ramadhan kufunga kama alivyokua anafunga nabii Daudi (Amani iwe juu yake); alikua anafunga siku moja na anakula siku moja.

Kipenzi chetu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikuakismulia kwa maswahaba zake hadithi zenye kuvutia zilizowatoka mitume walio tangulia. Aliwataka watu kuchukua mafunzo kutoka katika maisha ya mitume na namna walivyowachukulia watu walio kua wamewakaribisha kuukubali ujumbe wao.

Mtume wetu alikua pia akizungumzia mateso na ugumu walioupitia mitume katika kutekeleza majukumu yao na wakaonyesha subra na kupambana kama

mifano. Kwa namna hii aliweza kuwafariji waumini walio kua wanakandamizwa kuto kana na Imani yao. Waliyapata mateso na ugumu Kipenzi chetu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) yeye mwenyewe pia alikua anafarrijika kwa kukumbuka yale yaliyowakuta mitume walio tangulia. Alipokua anagawa ngawira baada ya vita ya Hunain, baadhi ya watu walilalamika ya kua Mtume afanye haki. Maneno haya yalimumumiza sana Bwana Mtume na akasema:

"Kama nisipokua mtenda haki basi ni nani atakua hivyo?" kisha akajifaraji mwenyewe kwa kusema, "Mwenyezi

Mungu aonyeshe huruma kwa Mussa. Japokua alikua akifanyiwa mambo mabaya Zaidi ya haya, lakini bado hakutetereka na subra yake.

Kipenzi chetu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) pia aliyasema ya kua jukumu la mitume ilikua ni kufanya kazi ya ukombozi kwa watu. **Alisema umuhimu wa kuwatii mitume na kufuata maamrisho waliyokuwa wanapewa na mitume hao.** Kuna muda aliwalinganisha

mitume kama mtu aliyepewa ujumbe muhimu sana kwa watu wake akisema:

"Mfano wangu na mifano ya uislam niliyotumwa kwayo ni kama mtu aliye kujua kwa watu na kusema:

— Enyi watu! Nimeliona jeshi la maadui kwa macho yangu mwenyewe, na mimi ni muonyaji Dhahiri; hivyo jilindeni wenyewe na okoeni maisha yenu."

Kisha kundi la watu wake walimsikiliza na kuondoka usiku wakaendelea na uzinzi hadi walipokua salama, wakati kundi jingine halikumu amini na wakabaki katika maeneo yao hadi asubuhi wakati majeshi yalipowafikia, yakawaua na kuwaharibu kabisa.

Kwa hiyo huu ni mfano wa yule anayenitii mimi na kufuata yale niliyokuja nayo (Quran na sunna), na mfano wa wale ambao hawakunitii mimi na hawaku amini ukweli niliyokuja nao." (Bukhari, l'tisam, 2)


Kipenzi chetu Mtume alikua akilinganisha ili kuelezea kwamba mitume walifanya kazi kwa maslahi ya watu:

"*Mfano wangu na mifano wenu ni ule wa mtu alltewasha moto na pindi wadudu na nondo(mduku mithili ya kipepeo)arukae Zaidi usiku wanapoanza kudondo kea ndani yake, na atafanya juhudili kuwafukuza. Na nimewashikilia katika mishipi yenu kwa nyuma kuwazuilia msiukaribie moto, lakini mnajaribu kunitoroka kutoka katika mikono yangu na kwenda katika moto.*" (Muslim, Fada'il, 19)



MASWALI

FUMBO



Kwenda kulia

1. Jina la mfalme aliyetawala kipindi cha Nabii Ibrahim na kujinasibisha mwenyewe na mungu kwa sababu ya umaarufu, mali na madaraka
6. Neno la kiarabu lilitumika kwa mitume kua na akili na maarifa/ufahamu
8. Neno la kiarabu lilitumika kuonyesha uchamungu wa mitume
9. Jina la pango ambamo wahyi wa kwanza ulimshukia Mtume (S.A.W)
11. Neno la kiarabu lilitumika kwa watu waliopewa jukumu la kipeleka ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu.
13. Jina la mama yake nabii Issa (Yesu)
15. Neno la kiarabu lilitokua linamaanisha uaminifu wa Bwana Mtume
16. Jina alilopewa bwana Mtume na watu wa Makka kwa sababu ya ukweli na uaminifu wake
17. Neno la kiarabu lilitumika kwa wafalme wa Misri
18. Neno la kiarabu lilitumika kuelezea sifa ya mitume kuchukua ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kuufikisha kwa watu

Kushuka chini

2. Neno la kiarabu lilitumika kuonyesha kua mitume hawakua wakitenda madhambi
3. Jina la mtume aliyekua anaitwa na Mwenyezi Mungu "Rafiki yake" (khalilullah)
4. Neno la kiarabu lilitumika kwa waislam wa Madina waliowasaidia wahamiaji toka Makkah
5. Jina la mlima ambaao safina ya nabii Nuhu ilitua baada ya mafuriko
7. Jina la mtume aliyewaokoa watu kutokana na mafuriko na anayekubalika kama "Baba wa pili wa walimwengu"
8. Jina lilitumika kwa kiumbi aliyefukuzwa pponi na huruma ya Mwenyezi Mungu toka alipokataa kumsujusia Adam
9. Neno lilitumika kwa waumini wa mwanzo wa nabii Issa (Yesu)
10. Jina la binadamu wa kwanza na mtume wa kwanza
12. Neno la kiarabu lilitumika kuonyesha upweke wa Allah na ujumbe huohuo kwa mitume wake
14. Jina la mtume aliyekua mfano wa walimwengu wote kutokana na haiba yake ya subra

1	Kuwapinga mitume		Upweke wa Mwenyezi Mungu na kumuabudu yeye peke yake.
2	Mitume walikua na jukumu la kupeleka dini ya Mwenyezi Mungu kwa watu		Mitume waliotangulia kwa upendo na heshima.
3	Japokua walipitia katika mateso na ugumu wa hali ya juu,		Ni alama ya huruma ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake.
4	Mitume wote waliwaita watu wao kuamini		Kuhusu kuwasamehe wale waliotudhuru na kulpizia ubaya kwa wema.
5	Mola wetu mtukufu alituma mitume wake		Na kuishi kwa mujibu wa kanuni zake.
6	Kumsamehe Adam baada ya kula katika mti uliokatazwa		Kua kigezo chetu.
7	Kipenzi chetu bwana Mtume alikua anakumbuka		Mitume hawakurudi myuma katika kuyaendea majukumu yao.
8	Nabii Yusuf ni mfano mzuri kwetu		Inamaanisha kuipinga dini.

Tujipime Wenyewe

- 1. Vipi tunamwita yule anayepokea wahyi toka kwa Mwenyezi Mungu, kuwafikishia watu maamrisho na makatazo yake, na kuwakaribisha watu katika njia iliyonyooka.?**
- A) Mwalimu
 - B) Msomi
 - C) Mtume
 - D) Rafiki wa Mwenyezi Mungu
- 2. Nini maana ya neno “Sidq”**
- A) Uaminifu, ukweli, uwazi wa mitume
 - B) Kutotenda dhambi yoyote
 - C) Kuwa na akili na mtazamo
 - D) Kuwa mwaminifu

- 3. Ni upi ilikua muujiza mkubwa wa Mtume Muhammad?**
- A) Tukio la Isra(safari ya usiku kati ya Makka na Jerusalem)
 - B) Quran tukufu
 - C) Kuwagawanyika kwa mwezi katikati
 - D) Tukio la Mi'raj(kupalizwa mbinguni)
- 4. Ni sifa ipi ya Mitume inahusu kua na akili na mtazamo?**
- A) Amanat
 - B) Fatanat
 - C) Ismat
 - D) Sida
- 5. Namna gani tunayaita matendo ambayo si ya kawaida yaliyofanywa na mitume kuhakikisha utume wao?**
- A) Muujiza
 - B) Uchawi
 - C) Ajabu
 - D) Utume

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi Kutohana Na Maneno Uliyopewa:

(Swala, Kufuata, Kiongozi, Habari njema, Somo, Mfano bora kabisa, Hoja, Uelewa, Maamrisho yetu, Ninafanya)


1. "Na tumewafanya mitume.....wawaongoze watu kwa" (al-Anbiya 21; 73)
2. "(Tumewatuma) wajumbe kama watoaji wa.....na pia kama waonyaji, ili watu wasiwe nadhidi ya Mwenyezi Mungu baada ya (kuja kwa mitumme)" (al-Nisa 4; 165)
3. "Hakika ndani yao.....kwenu nyie ili" (Mumtahina 60; 6)
4. "Katika hadithi zao(mitume) kwa yakini kuna.....kwa watu wenye" (Yusuf 12; 111)
5. "Tekelezenikama" (Bukhari, Ahad, 1)

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"(Tumewatuma) mitume kama
wabashiri wa habari njema ili watu
wasiwe na hoja dhidi ya Mwenyezi
Mungu baada ya (ujio) wa mitume..."

(al-Nisa 4: 165)





MSIMU WA REHMA NA IBADA:

RAMADHANI NA KUFUNGA



✿ Utukufu wa mwezi wa Ramadhan

✿ Maneno yanayohusiana na ramadhan na kufunga

✿ Faida za kufunga



✿ Aina za funga

✿ Sharia zinazohusiana na funga

✿ Taraweh, itikaf, usiku wenye cheo(lailat al-qadir) na

eid al-fitr

✿ Maisha ya mtume wetu ndani ya mwezi wa ramadhan



FUNGA YA KWANZA

Burak na familia yake walikua wamechoka sana. Kubeba mizigo waliyokuwa wamenunua kutoka sokoni kwa ajili ya iftar viliwafanya wachoke sana. Baada ya kupeleka mizigo jikoni Burak na baba yake walijweka katika kochi. Manunuzi waliyoyaanza tangu asubuhi, yalifiki mwisho mchana sana. Kuna kila kitu mtu anaweza akatizama na kupata katika soko. Asali tamu, aina mbalimbali za matunda ya zaituni zinazoweza kuwapa wateja hamu ya kula, siagi, nyama za kukaanga, nyama zilizotiwa pilipili na kusindikwa....Burak alijali sana chokoleti na alinunua aina chache tofauti tofauti kwa ajili ya kula wakati wa kufuturu.

Mama yake na Burak tayar alikua ameanza kufanya maandalizi kwa ajili ya Ramadhan siku kadhaa zilizopita. Alifanya usafi wa nyumba, kitindamlo(kitu kitamu kinacholiwa baada ya mlo) juisi za matunda na unga wa phyllo....kila kitu kilikua tayari kwa ajili ya mwezi wa Ramadhan ambao utaanza kesho yake.

Burak ana miaka kumi sasa na kesho itakua mara yake ya kwanza kufunga. Katika Ramadhan zilizopita alikua akifunga "husu funga" hii ni funga ya watoto. Ilikua inaanza baada ya sahur(Daku) na kuisha mlo wa mchana, na kwa msaada wa chakula cha mchana, ilifika hadi muda wa kufuturu jioni. Kwa

kuwa Burak amekua sasa, ataanza kufunga funga ya watu wazima wafanyavyo.

Baba yake alimwambia Burak:

— Mwanangu usiku wa leo swala ya kwanza ya taraweh itaanza kuswaliwa. Kama utataka unaweza kuja na mimi msikitini, lakin hakikisha kwanza umemaliza kazi zako za nyumbani kufikia jioni. Burak akamjibu:

— Nitazimaliza mapema.

Baada ya mlo wa jioni, Burak na baba yake walikwenda msikitini. Burak alijihisi kama mtu mzima baada ya kuvala kofia yake nyeupe ya kuswalia aliyotolewa na mama yake sandukuni. Walisikiliza kwanza mawaidha kabla ya kuanza kuswali. Baada ya adhana, swala ilianza. Aliswali swala ndefu ya taraweh kwa furaha. Alijiunga na mkusanyiko wa watu, wakimswalia Mtume kwa sauti (rehma na Amani ziwe juu ya Mtume) iliyosemwa katikati ya swala. Waliporudi nyumbani, ilikua ni muda wa Burak kwenda kulala, alipokua anakwenda kulala alisisitiza;

— "Mama, niamsheni kwa ajili ya sahur(daku) pia. Alikua hata anasema kua endapo atashindwa kuamka wammwagie maji usoni. Mama yake alimpeleka kitandani na kumwambia;



— "Usijali mwanangu nitakuamsha..

Burak alipitiwa na usingizi punde tu baada ya kuweka kichwa chake kitandani. Muda mfupi kabla ya kupambazuka, mikono laini ya mama yake ilikua ikimpapasa katika mashavu yake na alikua anamwambia:

— Amka kijana mkubwa, muda wa daku karibia uishe. Burak aliyekwenda bafuni akiwa ana usingizi bado, alijimwagia maji ya baridi usoni ili apoteze usingizi. Alikaa katika meza ambayo mama yake alikua ameandaa. Mama yake aliamua kumfanyia mshangao Burak kwa kumuandalia chakula kile anachokipenda zaidi kwa ajili ya daku yake ya kwanza. Alimkumbatia mama yake na kusema:

— "Mama yangu mpendedwa naweza kumaliza hiki chakula chote peke yangu.

Ili nisipate njaa sana mchana. Burak alipata mlo mzuri. Baba yake alimtahadharisha:

— Mwanangu! Usisahau kunywa maji, hivi punde itakua muda wa adhana kwa ajili ya swala ya alfajir. Kama unavyoja, hadi jioni hakuna kula wala kunywa." Alikunywa vikombe kadhaa vya maji ili asipate kiu wakati wa mchana. Kisha akasafisha kichwa chake na kutia (An-niyya) kwa ajili ya funga, alimsikiliza baba yake aliyekua anasoma Quran sebuleni. Baada ya kuswali swala ya asubuhi alirudi tena kulala ili kupumzika Zaidi

Alipoamka Burak alikwenda jikoni kwa nia ya kunywa maji. Ilibaki kidogo tu anywe maji ila akakumbuka kua amefunga. Alitizama muda ilikua ni karibia saa nne. Alianza kuwaza kwa namna gani atawenza kuvumilia kukaa bila kunywa maji kwa muda wote hadi saa ya kufuturu jioni. Kwanza, aliwaza kufungulia. Lakini sauti ilitoka ndani yake ikimwambia kua alikua kijana mkubwa sasa na hakupaswa kufungulia.

Burak alikata shauri; ya kua hata kama itakua na ugumu kiasi gani lazima ateketeze ahadi aliyoweka kwa Mwenyeze Mungu. Kuamka kwa ajili ya kula daku ilimaanisha kumuahidi Mwenyezi Mungu kufunga siku ya leo.

Ili kutimiza muda, aliamua kutafuta jambo ambalo litamshughulisha. Kwanza alicheza na midoli yake kwa muda. Japokua midomo yake ilikauka na macho yake yalikua yakinazama chupa ya maji iliyokuwepo mezani. Kufikia mchana kulikuwepo na njaa baada ya kiu. Hadi kufikia jioni aliwenda kukaa kwa mama yake

aliyekua anaandaa chakula kwa ajili ya futari ya jioni. Mama yake alimtania alipomuona amekwenda kukaa kwenye meza ya jikoni kimya;

— Kimetokea nini mwanangu! Inaonekana funga ya leo imekuchosha sana Burak!

— "Unajua mama, nilitamani hata maji ya Mavish(ndege mdogo) katika kizimba chake. Sasa naweza hata kula supu ambayo unajaribu kunitengenezea nitumie kijiko ulichonacho mkononi mwako.

— Mwanangu mpendedwa, tizama siku moja uliyofunga imekufanya uwazo hivyo! Hali ya masikini ambao hawana uwezo japo wa kupata kipande cha mkate cha kula,hii ni thamani ya kipande cha mkate na maji ya kunywa ambayo Mwenyezi Mungu ameturuzuku sisi kuvipata katika meza yetu....njoo na unisaidie kupanga meza. Tuandae tayari kabla baba yako hajarejea.

Burak alikua amebeba sahani za chakula ambazo hakuwahi kujua thamani yake hadi leo kwa kuzibeba kwa umakini kama kitu cha thamani sana na kuziweka juu ya meza kwa makini.

Muda wa kufuturu ulipokua unakaribia familia nzima ilikaa pamoja mezani na kusubiria. Baba yake alisema huku nakatabasamu;

— "Kazi nzuri Burak, umeikamilisha funga yako ya kwanza kikamilifu. Ninanunua funga yako, alisema kwa utani, akaweka pesa katika mfuko wa Burak mshahara wa wiki moja.

Hata kabla funga haijakkamilika, Burak alikuwa amepata tayari zawadi. Chakula ambacho alikula jana pasina kufikiria kilikuwepo katua mkono wake sasa. Ingawaje alikua na njaa na hakuna aliyekua akimzuia, alikua anasubiria kibali toka kwa Mwenyezi Mungu.

Muda ambao kila mmoja alikua anausubiri ulinadiwa mjini kwa mwanga wa minara na adhana. Burak aligungua saumu yake na alikua na furaha sana. Alipata furaha ya kuptitia mtihani mgumu na kutekeleza ahadi aliyokua amejivekea kwa Mwenyezi Mungu.

Hasan Tahsin KARAMAN (kifupisho)

Ramadhan ni mwezi ambao tunafunga mchana na kuswali swali ya taraweh wakati wa usiku

Quran tukufu ilianza kuteremka katika mwezi wa ramadhan

Matendo yetu mazuri pamoja na ibada nyingine zinazofanyika mwezi wa ramadhan hulipwa Zaidi

Usiku ulio mbora (lailat al-qadir) ambao una thamani kuliko miezi 1000 upo ndani ya mwezi wa ramadhan

YA SEHRI RAMAZAN
RAMADHAN : SULTANI WA MIEZI KUMI NA MOJA

Ramadhan ni mwezi ambao vipato yetu vinapata Baraka

Ramadhan ni mwezi wa subra, Thawabuya subra ni pepo

Kuna rehma katika mwanzo wa ramadhan, msamaha katikati ya mwezi wa Ramadhan ni na kuwekwa mbali na moto katika mwisho wake.

Ramadhan ni mwezi wa kusaidiana

INAN ALLAHADIR



FUNGA NI NINI?



 **Funga**, ni kujizuia kula, kunywa na kujamiihana toka alfajir hadi linapozama juu.



Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Enyi mlaoaminil Mmefaradhishiwa funga kama walivofaradhishiwa waliokuwepo kabla yenu ili mpate kufaulu."

(al-Baqara 2: 183)

Juu Ya Nani Funga Ni Lazima/Faradhi?

Ni faradhi


Kufunga mwezi wa ramadhani

Kwa kila muislam

* Ambaye ana akili timamu na amepevuka na mwenye afya kiasi cha kutosha kufunga

 Ingawa si lazima funga kwa watoto, inashauriwa kuwazoresha kufunga ikiwa kufanya hivyo hakuwaleti madhara. Kwa namna hii, itawajengea tabia ya kufunga na kujumuika katika furaha na wakubwa zao.



Ni masharti gani muhimu kwa funga zetu kukubalika?

Ili funga zetu zikubalike:-

* Kutia nia
* Kukaa mbali nayale yote yanayobatilisha funga toka alfajir hadi juu linapozama

Vyote hivyo vinahitajika..


BAADHI YA MASUALA YANAYOHUSIANA NA RAMADHANI



Ni wakati gani na namna gani tunaweka nia ya kufunga?

Tunaweka nia ya kufunga kabla ya mapambazuko kwa kusema: "Nanuiya kufunga siku inayofuata ya ramadhani kwa ajili ya Mwenyesi Mungu."



Kipi kinatokea iwapo mtu amesahau kutia nia usiku kwa funga ambazo sio faradhi yaani za sunna?



Si lazima sana kuweka nia kwa funga za sunna kabla ya mapambazuko. Niya inaweza kuwekwa dakika 45 kabla ya swala ya adhuhuri.



je, ni lazima kusema nia kwa mdomo?

Hapana, inatosha kutia nia moyoni. Kuamka na kula daku, kuamua kufunga toka usiku kabla ya siku mpya au kujua ya kua mtu atafunga siku nzima vinatosha kusema umetia nia. Japokua ni vizuri kama tutasema nia zetu kwa vinywa.



Imsak ni nini?



Imsak maana yake ni "kuacha" na inamaanisha kua muda wa kufunga umeanza, ambapo ni kabla ya mapambazuko jua linakaribia kuchomoza. Muda huu pia ni muda ambaa swala ya alfajir inapoingia



Sahur ni nini?



Muda kabla ya imsak unaitwa sahur. Chakula kinacholiwa muda huu kinaitwa "Daku"



Kipi kinatokea ikiwa mtu amesahau kutia nia kabla ya mapambazuko kwa ajili ya funga ya Ramadhani?

Ikiwa tutatia nia baada ya mapambazuko, vyote yaani nia pamoja na funga vinakua batili.





Je, tunatakiwa kutia nia kila usiku wa ramadhani? Tunaweza kufunga mwezi mzima wa Ramadhani kwa nia tulioitia mwanzoni mwa mwezi wa Ramadhani?



Mtu anatakiwa kutia niya kila siku kwa ajili ya kufunga siku hiyo kabla ya mapambazuko. Niya ya mara moja kwa ajili ya mwezi mzima haitoshi.

- ✿ Muda wa sahur(Daku) ni muda ambaa dua zinakubaliwa. Chakula cha daku kinatupa nguvu na uvumilivu wa kufunga. Mtume wetu alitushauri tule daku na kusema, "kuleni daku hakika kuna faida nyingi sana katika chakula cha daku." (Bukhari, Sawm, 20)

Muda wa daku ni muda kabla ya mapambazuko. Ni muda ambaa rehma na Baraka za Allah zinatumiminiika.

Sahur ni kipindi cha muda mtukufu ambacho wale wanaompenda Mwenyezi Mungu hupitisha muda wao wakifanya ibada,

Iftar ni nini?



Muda wa kufunga unaithwa Iftar. Muda wa Iftar ni sawa na muda wa kuingia swala ya magharib.



- ✿ Iftar ni muda wa furaha kwa wale ambaa wamemaliza siku yao pasina chakula wala maji kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyeze Mungu. Muda wa kufuturu tunapata furaha kwa kuikamiliosha funga ya siku hiyo. Tutaipata ile furaha ya kweli tutakapopata thawabu za funga huko akhera.

- ✿ Kipindi cha jioni katika ramadhani, kuwapa futari wale waliofunga ni kitendo chenye malipo makubwa mno.

- ✿ Kama ilivyo kwa kipindi cha daku/sahur kipindi cha kufuturu pia ni kipindi dua zetu zinapokelewa. Mola wetu anapokea sala zetu za unyenyekevu tunazozifanya wakati wa futari. Tunatakiwa kutumia ipasavyo mida hii na kuomba dua.

wakiomba dua, na kumkumbuka sana Allah(SW). Waumini ambaa wanamka kwa ajili ya Sahur(daku) ni kama wanasesma:

Mola wetu! Asante sana kwakua mimi ni mionganoni mwa mwale wanaokujua wewe, wanaokupenda, na kutoa mioyo yao kwako. Ili kuonyesha unyenyekevu wangu kwako, nmeamka na kukatisha usingizi wangu, nitafunga kwa ajili ya kutaka radhi zako leo. Ewe Mwenyezi Mungu! Ninamatumaini kua utakua radhi namie.

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Kuna nyakati mbili za furaha kwa wale ambaa wanafunga, moja wapo ni pindi wanapofungua funga yake na nyingine ni pale wanapoungana na Mola wao na thawabu za funga"

(Bukhari, Sawm, 9)

"Yoyote anayefuturisha mtu aliyefunga anapata malipo sawa na yale ya aliyefunga. Hakuna chochote kitakachopungua kwa yule aliyefunga."

(Tirmidhi, Sawm, 82)

"Dua ya watu watatu hua hairejeshwi, dua inayofanywa na mtu aliyefunga wakati kwa kufuturu, dua ya mtawala mwadilifu na dua ya mtu aliyedhulumiwa."

(Tirmidhi, Daawat, 128)

Dua ya wakati wa kufuturu

Ni sunna kufanya dua hii ifuatayo katika kipindi cha kufuturu:

اللَّهُمَّ لَكَ صُنْتُ وَبِكَ آمَنْتُ وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْكَ رِزْقَكَ أَفْطَرْتُ
وَصَوْمَ الْعَدْ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ نَوَيْتُ فَاغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ وَمَا أَخْرُتُ.


"Allahumma laka sumtu wa bika amantu wa alaika tawakkaltu
wa ala rizqika aftartu wa sawma al-ghadi min shahri ramadana
nawaytu faghfir li ma qaddamtu wa ma akhkhartu."

"Ewe Mola wangu! Nimefunga kwa ajili ya kupata radhi zako.
Ninakuamini wewe peke yako na ninaweka Imani yangu kwako.
Ninafungua swaumu yangu kwa kile ulichoniruzuku. Ninaweka nia ya
kufunga kesho. Tafadhalni nisamehe madhambi yangu ya nyuma na ya
sasa."



FUNGA INATULINDA SISI

NI KWA NAMNA GANI TUNAFUNGA?



Tunaamka usiku na kula chakula cha "daku" na kutia niya ya kufunga. Wakati wa mapambazuko (imsak) tunaanza kufunga.



Toka muda wa Imsak hadi kuzama kwa jua,
tunajiweka mbali na matendo yanayoharibu
funga kama kula na kunywa.

Jua linapozama tunafungua kwa
kula chakula cha Iftar. Tunamshukuru
Mwenyezi Mungu kwa kulturuzuku
neema mbalimbali.

Hivyo tunakamilisha funga ya siku moja

KWA NAMNA FUNGA ZINATUKINGA?

Funga sio tu kujizuia kula na kunywa hadi jioni. Wakati huo huo funga, ni kuijweka mbali na matendo yote yasiyopendeza na maovu kabisa kama vile kupigana, kusengenya, na kuumiza hisia za wengine. Funga iliyo fanyika kwa namna hii, kama mwalimu wetu Mtume inaweka "Ngao ambayo inamlinda mtu kuto kana na madhambi na moto".

Tusipokaa mbali na vitu vilivyokatazwa (Haram), hata tukijizulia kula na kunywa vitu vilivyoruhusika, funga zetu hazina maana yoyote mbele ya Mwenyezi Mungu. Kipenzi chetu Mtume Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) alituhabarisha kuhusu usemi huu:

"Yoyote ambaye hataacha kusema maneno ya uongo na matendo maovu, Mwenyezi Mungu hana haja ya kukaa kwake na njaa na kiu." (Bukhari, Sawm, 8)"

FAIDA ZA FUNGA

Kwa kufunga:

Tunamridhisha Mwenyezi Mungu na kupata mapenzi na kuridhiwa ya Allah.

- Tunakumbuka kua Mwenyezi Mungu anaturuzuku Baraka nyingi sana hivyo tunamshukuru yeye Zaidi.
- Tunajifunza kua na uvumilivu.
- Tunajitenga na mambo maovu na machafu na kujikinga na moto.
- Tunaelewa kwa kuhisi nini maana ya kua na njaa na kua maskini.
- Tunalinda afya zetu.

Tunafunga kwa kukaa mbali na kula na kunywa kwa kua ni amri ya Mwenyezi Mungu. Hatufungu swaumu zetu kwa siri hata kama hatukonekani na mtu kwa kujua kua Allah anatuona. Kwahiyu, tunamridhisha Mola wetu Mlezi na tunapata mapenzi na kuridhiwa na Mwenyezi Mungu.

Mwalimu wetu Mtume Muhammad amesema Allah(SW) anasema:

"Ameacha chakula chake, kinywaji chake na matamano yake kwa ajili yangu. Funga hiyo ni kwa ajili yangu. Hivyo nitamlipa(Mfungaj) kwa funga yake." (Bukhari, Sawm, 4)

Muda mwangi hua hatutambui thamani ya vitu tulivyonavyo hadi pale tutakapovikosa. Tukiwa tumefunga tunahisi njaa na kiu kwa mchana mzima. Tunatambua thamani ya maji na neema mbalimbali tulizoruzukiwa. Kwahiyu tunakumbuka kua Mwenyezi Mungu ndiye aliyeturuzuku neema mbalimbali na tunamshukuru yeye Zaidi.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hivyo nikumbuke mimi name nitakukumbuka wewe, na kua na shukurani kwangu na wala usinikufuru. "

(Al Baqarah - Ng'ombe 2: 152)

Mtu anaweza akapitia baadhi ya ugumu na mateso katika maisha. Ili kuyavuka hayo ni lazima awe na uvumilivu. Uvumilivu ni kanuni muhimu sana ya kufikia mafanikio. Tunapokua tumefunga tunastahili njaa na kiu kwa mchana mzima na kujifunza kua wavumilivu.

Mtume Muhammad amesema:

"Funga ni nusu ya uvumilivu"

(Ibn Majah, Siyam, 44)

Matendo mabaya kama vile kusema uongo, kusengenya, kugombana, kutotenda haki kwa wengine na kumvunja mtu moyo ni madhambi ambayo yanatuweka karibu na moto. Tunaweza kujitenga na hayo endapo tunadhibiti mienendo yetu. Katika mwezi wa Ramadhan, tunaingia katika mazingira ya mafunzo ya kiroho. Tukifunga, tunajua kua tunaendeleza ibada kwa Mwenyezi Mungu na kujifunza kujidhibiti wenyewe. Hivyo, tunajiweka mbali na matendo machafu na kujikinga na moto.

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Funga ni ngao au ulinzi dhidi ya moto na kutenda madhambi.

Mtu anajizula
kujamiliana na mke
wake na kugombana.
Na ikiwa anataka
kugombana au
kumkwaza, anatakiwa
aseme, 'Nimefunga.'



(Bukhari, Sawm, 9)

Wale ambaو hawajawahi kupitia njaa hawawezi kufahamu njaa na ugumu ambaو maskini wanaupitia. Watu wasiokua na shida na wenyе mali hawawezi kuhisi maumivu yale maskini wanayahisi. Tunapofunga, tunaanza kuelewa nini maana ya njaa na kua maskini ilivyo kwa kupitia hali hiyo. Tunahisi katika miyo yetu namna gani watu masikini wanaishi maisha yao na ni tabu gani wanazipitia. Hisia zetu za kujali na huruma zinakua. Na matokeo yake tunawasaidia maskini na mayatima na kugawana neema tulizo neemeshwa.

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Angalieni wale ambaو wana vipato
ya chini kuliko nyinyi, kuliko wale
ambaو wako juu kuliko nyinyi, kwa
sababu hili litawafanya mgundue ni jinsi
gani mlivyonemeshwa na kuwazuua
kuzidogosha neema hizo."

(Muslim, Zuhd, 9)


Matumbo yetu pamoja na viungo vingine vinafanya kazi usiku na mchana kwa kipindi cha miezi kumi na moja. Wote tunajua kua matatizo ya matumbo yanatibiwa kwa chakula bora. Kwa mantiki hii funga inafanya kazi kama chakula bora. Katika mwezi wa Ramadhan kitu cha kwanza ni matumbo yetu na viungo vingine vinavyohusiana na mmeng'enyo wa chakula unapata mapumziko. Kwa hiyo tunaimarisha afya zetu.

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Fungeni ili mpate afya."

(Tabarani, Mu'jam al-awsat, VIII, 174)







AINA ZA FUNGA



Zipo aina nne za funga ambazo ni: Faradhi, Sunnah, zilizokatazwa na zilizohalali.


FUNGA YA FARADHI(WAJIB) ☺☺☺

- ✿ Funga ya mwezi wa Ramadhani,
- ✿ Funga ya kulipa(Qadha) siku ulizoacha kufunga katika mwezi wa Ramadhan,
- ✿ Funga kusahihisha(kaffara) kwa kufungua kabla ya muda katika mwezi wa Ramadhan.
- ✿ Funga ya kutia nadhiri

FUNGA YA SUNNAH ☺☺

Ilikua ni utamaduni wa Mtume wetu kufunga siku nyingine ambazo si katika mwezi wa Ramadhan. Pia aliwashauri maswahaba zake kufunga katika siku hizo. Baadhi ya siku hizo alizokua na tamaduni ya kufunga ni:

- * Kufunga siku ya 9 na 10 au ya 10 na 11 katika mwezi Muharram,
- * Kufunga siku sita(6) katika mwezi wa Shawwal
- * Kufunga siku za jumatatu na alhamis
- * Kufunga siku ya 13,14 na 15 ya kila mwezi (Masiku meupe)
- * Funga ya Nabii Daudi(unafunga siku moja na unakula siku moja)
- * Kufunga siku moja kabla ya Eid al-adha(Hii ni sunna kwa wale ambao hawaajaалиا kuhiji)



79

FUNGA AMBAZO ZIMEKATAZWA ☹☹☹

- * Kufunga siku ya kwanza ya eid al-fitr.
- * Kufunga siku nne za eid al-adha(Sikukuu ya kuchinja).
- * Kufunga siku za mwisho za mwezi wa Shaaban(yawm shak) siku ya mashaka ukifikiri kua ni siku ya kwanza ya Mwezi wa Ramadhan.
- * Kufunga nusu ya mwisho ya mwezi wa Shaaban, ikiwa mmoja wenu hakufunga katika nusu yake ya mwanzo.

FUNGA YA HALALI LAKINI NI MAKURUHU ☹☹

- * Kufunga siku ya kumi pekee ya mwezi Muharram, Ashuraa, bila ya kufunga siku ya baada au kabla yake
- * Kufunga siku za ijumaa tu
- * Kufunga siku za jumamosi tu
- * Kufunga siku za jumapili tu
- * Isipokua wale ambao wanaendelea kufunga katika siku hizo kama sehemu ya sunna nyingine
- * Kufunga mwaka mzima

FUNGA YA QADHA (KULIPA)

Nini maana ya funga ya kulipa?

☞ Ni aina ya funga ambayo inafungwa ili kufidia zile siku ambazo mtu hakufunga katika mwezi wa Ramadhan, swaumu yake iliharibika ama allisahau ama kwa udhuru mwingine wa kisheria.

Ni wakati gani mtu anatakiwa afunge funga hii ya Qadha?

Inaweza ikafungwa siku yoyote baada ya mwezi wa Ramadhan isipokua kwa siku ambazo zimekatazwa kufunga (Zisizokua za kisheria au halali) kufunga.



FUNGA YA MAREKEBISHO (KAFFARA)

Kaffara ni nini?

☞ Ni nyongeza katika kulipia funga, funga hii ya marekebiso ni lazima kwa mwanaume kwa kufunga mwezi wa Ramadhan na kubatilisha funga kwa kujamilana na mke wake. Funga hii inajumuisha kufunga siku za miezi miwili inayofuatana. Funga hii inakua ni faini inayoitwa "Kaffara."

Ni siku ngapi za kaffara?

Urefu wa kaffara ni miezi miwili. Mara nydingi hua siku 60. Ambapo siku moja ya nyongeza inakua ni kufidia siku iliyoharibika funga hiyo inajumlishwa na siku hizi za kaffara, ambapo inafanya jumla ya siku sitini na moja (61). Kwa sababu hii, funga hii inakua inachukuliwa kama siku sitini namoja (61).



MATENDO YANAYOBATILISHA FUNGA

Kutokufunga siku katika masiku ya mwezi wa Ramadhan au kufungua kabla ya muda wake bila sababu yoyote ya kisheria inachukuliwa kama dhambi. Ikiwa tutafungua funga zetu kabla ya kuzama kwa jua na huku tukijua kua tumefunga, ni wajibu kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kwa dhambi ambayo tumeifanya. Wale ambao wanafungua swaumu zao kabla ya wakati kwa sababu nyingine tofauti na tendo la jimatilishi wa kuzama kwa kufungua siku hiyo kwa siku nyingine au kutokana na hali Fulani kutoa kiasi Fulani cha chakula kwa wenyewe uhitaji (Fidiya).

Ikiwa tutafanya katika matendo yafuatayo,funga zetu zitakua batili:

- Kula na kunywa kwa makusudi.
- Kuingiza kitu ndani ya mwili kupitiya pua, Mdomo, Masikio au sehemu za siri.
- Kujitapisha kwa makusudi.
- Kujamili ana kwa makusudi.
- Kutokwa na manii kutokana na kuwaza au kutizama kwa matamano.
- Kwa wanawake,kutokwa na damu ya hedhi au nifasi(damu baada ya kujifungua).
- Kupoteza fahamu kutokana na kuzimia, kulewa au kurukwa na akili
- Kutoka katika uislam.

Yanabatilisha funga.

81

Funga ambazo hazikutekelezwa ndani ya mwezi wa Ramadhan zinatakiwa zitekelezwe kabla ya mwezi mwengine wa Ramadhan kuingia. Ikiwa mmoja atachelewa bila udhuru wowote wa kisheria kulipa siku ambazo hakuzifunga kipindi cha ramadhani hadi ramadhani nyingine inafiki,mtu huyo anahesabika kama mkosefu. Kwa nyongeza, kulipia siku ambazo hukuzifunga, mmoja wenu anatakiwa kulipia fidiya au kutoa fedha kama fidiya kwa kila siku ambayo hakufunga. Fidiya inalipwa kwa chakula ambacho ni maarufu kinacholiwa na watu wa mji ule. Wanatakiwa wapewe watu wenyewe uhitaji kama sadaka. Ikiwa mtu atalipa siku alizokua hajazifunga miaka kumi baadaye, anatakiwa kulipia fidiya kwa miaka kumi.

Ikiwa sababu ya mmoja wenu kutofunga ni yenye kuendelea, basi ni ruhusa kwake kuchelewa kulipa kutokana na sababu hiyo kuwepo hadi wakati huo. Mtu huyo haitamlazimu kulipa fidiya kwa kuchelewa hata kama ramadhani kadhaa zitapita, lakini ni wajibu kulipa siku ambazo hakuzifunga.





VITU AMBAVYO NI HALALI LAKINI NI MAKURUHU KUVIFANYA UKIWA UMEFUNGA ☹☹

Kufanya mambo yafuatayo ni ruhusa kwa mtu aliyefunga:

Wakati
umefunga.

- ☹ Kugombana na wengine
- ☹ Kuchelewa kugungua baada ya jua kuzama
- ☹ Kuonja chakula bila kukimeza
- ☹ Kutoa damu
- ☹ Kumbusu mke wako bila kua na matamano
ya kujamiihana
- ☹ Kumkumbatia mke wako
- ☹ Kuoga
- ☹ Kutumia mswaki wakati wa mchana
- ☹ Kuvuta wanja
- ☹ Lining the eyes with kohl

Ni makuruhu.



MATENDO AMBAYO HAYABATILISHI FUNGA

- ✖ Kula au kunywa bila kukusudia kutohaka na kusahau,
- ✖ Kumeza chembe ya chakula ndogo sana iliyobaki baina ya meno wakati wa kula.
- ✖ Kufanya jambo ambalo kihalali linabatilisha funga lakini kwa sharti ya kutishiwa.
- ✖ Kumeza mate yako mwenyewe
- ✖ Kumeza majimaji yaliyobaki pamoja na mate baada ya mtu kua amepiga mswaki,
- ✖ Kuvuta au kuingiwa na vumbi pasina kukusudia.
- ✖ Kuota ndoto nyevu,
- ✖ Kuoga,
- ✖ Kutumia dawa ya matone ya macho,
- ✖ Kung'oa jino ila kwa sharti la kutomeza damu.
- ✖ Kutapika bila kukusudia,
- ✖ Kutumia mswaki bila dawa ya meno.
- ✖ Kutoa damu
- ✖ Kuchoma sindano

Haya hayabatilishi funga.

💡 Ikiwa mtu amekula au kunywa bila kujitambua, anatakiwa kuacha kula au kunywa mara moja atakapokumbuka. Hali hii halibatilishi funga.

💡 Anachotakiwa kufanya ni kuosha vizuri kinywa chake na kuendelea kufunga. Ikiwa hataacha kula au kunywa hata akikumbuka kua amefunga funga itakua imebatilika.

💡 Na atalazimika kuja kuilipa baada ya ramadhan.

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Mtu atakayekula au kunywa mchana wa ramadhanie kutohaka na kusahau, anatakiwa akamilishie funga yake. hiyo ni kwa sababu mwenyezi Mungu amemfanya ale au anywe."

(Bukhari, Sawm, 26)

MAMBO YAPI HUMFANYA MTU ASILAZIMIKE KUFUNGA?

Uislam ni dini ambayo imeweka maisha ya watu kua mepesi. Mwenyezi Mungu Mtukufu hua ham lazimishi mtu jambo ambalo mjaa hana uwezo nalo. Hukmu hiyo inahusika katika funga pia. Ni dhambi kutofunga mwezi wa Ramadhan bila udhuru wowote. Japokua kuna baadhi ya hali, ni ruhusa kutofunga au


kukatisha funga uliyokua umelianza. Baada ya Ramadhan, funga abazo hazikufungwa zinatakiwa kulipwa mara moja.

Zifuatazo ni hali ambazo dini yetu inazikubali kama udhuru wa kutofunga au kufungua katika mwezi wa Ramadhan:

1	Kusafiri	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Katika mwezi wa Ramadhan wale wanaosafiri walau km. 83 na wamedhamiria kukaa kwa siku chini ya nne hawana haja ya kufunga.
2	Ugonjwa	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Wale amba wanamashaka ya kua maradhi waliyonayo yataku na madhara kwa afya zao au matibabu yataku ya taratibu wameruhusiwa kutofunga. Katika hali kama hizi mtu anaweza pia akafungua funga aliyokua amelianza tayari. ✍️ Mtu anatakiwa ahakikishiwe na tabibu/daktari mwadilifu kua ugonjwa alionao unaweza ukawa mbaya Zaidi endapo atafunga na endapo hatapata wasaa huo wa kumuona daktari basi anatakiwa awe anahisi kua yupo katika hali hiyo.
3	Umri mkubwa	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Wazee amba hawawezi kufunga si lazima kwao kufunga. ✍️ Wale amba hawana matumaini ya kuweza kufunga tena wanatakiwa walipe fidiya kwa kila siku amba hawakuweza kuifunga.
4	Kunyoshesha au kua mjamzito	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Endapo mwanamke ananyonyesha au ni mjamzito anaogopa kua funga itamdhuru yeye au mtoto wake, anaruhusiwa kutofunga.
5	Kutokwa na damu ya hedhi au damu ya nifasi.	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Ikiwa mwanamke ameanza kutokwa na damu ya hedhi au nifasi, anavunja funga yake. hafungi kwa siku ambazo anatokwa na damu ya hedhi au ametoka kujifingua.
6	Kugombana na adui	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Askari ambaye anahofu kua hana nguvu za kupambana na adui hatakiwi kufunga kipindi cha ramadhan.
7	Kua chini ya shinikizo au tishio	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Mtu ambaye yupo chini ya shinikizo la kuuwawa au kujeruhija hatakiwi kufunga au anaweza akaifungua funga aliyokua amelianza.
8	Njaa na kiu vilivyopindukia	<ul style="list-style-type: none"> 📖 Mtu ambaye anaogopa kua njaa na kiu kikali vinaweza kumuathiri ubongo au mwili wake anaweza kuvunja funga aliyokua amelianza tayari. Hivyo hivyo kwa mtu anayefanya kazi ngumu kama kazi za shambani kisha anaogopa kua funga inaweza kumletea madhara, asifunge.

KIASI KINACHOTOLEWA KWA MASIKINI MWISHONI MWA MWEZI WA RAMADHANI (ZAKAT AL-FITR) ☺☺☺☺

   Zakat al-fitr ni aina ya kiwango kinachotolewa na waislam ambao wana kadiriwa kua matajiri kutokana na kipimo cha sharia ya kiislam kwa ajili yao na kwa wanafamilia wanowategemea. Kiwango hiki ni wajibu kinachotolewa katika mwezi wa Ramadhan hiutwa "zakat al-fitr."

  Zakat al-fitr inatakiwa itolewe kabla ya sikukuu ya eid al-fitr. Kwa namna hii watu masikini watakua na furaha na watajua na uhakika kwa kutimiza mahitaji yao kabla ya sherehe.

Kiwango cha zakat al-fitr kinakadiriwa kua (gram 2.400) ya aina fulani ya nafaka. Muumini anatakiwa atoe zakat al-fitr yeye mwenyewe, kwa watoto wake na kwa wale wanaomtegemea.

  Zakat al-fitr inaweza kutolewa katika mtindo wa nafaka ambazo ni maarufu katika mji huo mfano, ngano, mchele, zabibu kavu, choroko au mahindi.

  Leo hii thamani ya nafaka kuu inafanyiwa tathmini na zakat al-fitr inaweza kulipwa katika mfumo wa pesa. Kwa sababu pesa daima hua afadhali kuliko chakula kwa ajili ya kuhudumia

mahitaji ya watu. Kwa chakula watu wanawezwa wakatosheka kutokana na njaa tu, wakati ukiwa na pesa unaweza ukaribuanu kitu unachokitaka.

  Zakat al-fitr inatakiwa itolewe kwa watu wanaishi maeneo ya karibu ya mji huo. hairuhusiwi kupelekwa kwa masikini wanaishi katika miji mingine. Japokua kama hakuna watu wenye uhitaji wanaishi katika mji huo, fitr inaweza kupelekwa katika miji mingine.

  Wakati wakutoa fitr: zakat al-fitr inakua ni faradhi jua linapotua jioni ya mwisho ya siku ya Ramadhan. Ingawa kama iliyokua kutoa sadaka za lazima kabla ya muda wake, inaruhusiwa kutoa zakat al-fitr muda wowote ndani ya mwezi wa Ramadhan.

  Ni makuruhi kuchelewa kutoa zakat al-fitr hadi usiku wa kwanza wa eid al-fitr na pia ni dhambi kuchelewa hadi baada ya eid. Japo baada ya siku ya kwanza ya eid kupita muda wa kulipa zakat al-fitr hua umemalizika, ila inalazimika kulipwa.


  Zakat al-fitr ni sadaka ya miili yetu na afya. Ni njia ya kuonyesha shukrani zetu kwa Mola wetu mlezi aliyetuumba, kutufanya tuishi kama waislam na kutuwezesha kuufikia mwezi wa Ramadhan tukiwa na afya na ustawi.

FUNGA YA KUTIA NADHIRI ☺☺☺☺

     Funga ya nadhiri ni funga ambayo tunaahidi kuifanya kwa ajilinya Mwenyezi Mungu. Ni lazima tutimize ahadi/nadhiri hizo.

Kuna aina mbili ya funga ya nadhiri:

1. Funga ya nadhiri inayohusisha hali Fulani.

  Kwa mfano, "ikiwa tumeahidi kufunga siku tatu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, italazimika kufunga siku hizo tatu. Au "kama tumedhamiria kufunga kwa siku Fulani kama vile jumatatu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, inatulazimu tufunge katika siku hiyo.

kufunga siku tatu pindi mama yake atakapopata nafuu ya maradhi yake.

2. Funga ya nadhiri isiyohusisha hali yoyote.

  Kwa mfano, "ikiwa tumeahidi kufunga siku tatu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, italazimika kufunga siku hizo tatu. Au "kama tumedhamiria kufunga kwa siku Fulani kama vile jumatatu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, inatulazimu tufunge katika siku hiyo.

SWALA YA TARAWEH ☺☺

- ✿ Swala ya taraweh ni swala yenye rakaa ishirini ambayo inaswaliwa katika mwezi wa Ramadhan. Kutekeleza swala hii inasisitizwa(sunna muakkada) kwa wanaume na wanawake.
- ✿ Swala hii inaswaliwa katika misikiti penye mkusanyiko wa watu, pia tunaweza tukaswali majumbani mwetu. Japokua ni vizuri ikiswaliwa katika mkusanyiko wa watu kwa ajili ya kupata thawabu zaidi.
- ✿ Pia ni sunna kuswali swala hii kwa wale ambao hawajajaaliwa kufunga kutohara na udhuru. Inatakiwa kuswaliwa kwa rakaa mbili mbili.

MAFUNZO YA KIROHO ☺☺

- ✿ "I'tikaf" maana yake kukaa msikitini au nyumba ya ibada kwa muda Fulani kwa niya ya kufanya ibada.
- ✿ Baada ya funga kuwa faradhi, Mtume alitumia siku kumi za mwisho za Ramadhan katika I'tikaf hadi anafariki dunia. Kwa hiyo ni sunna kutafakuru katika misikiti kwa siku kumi za mwisho za Ramadhan.
- ✿ Kabla ya kufanya tafakuru msikitini tunavaa nguo safi na kujipaka manukato. Wakati tukiwa katika kipindi cha tafakuru, tunasoma quran tukufu, tunaomba dua, kusoma hadithi za bwana Mtume Muhammad(S.A.W) na vitabu kuhusu uislam. Tunasoma majina ya Mwenyezi Mungu na kukithirisha ibada au kuswali Qadha kwa swala tulizokua tumeacha. Tunaendelea kuswali na kujizuia na kukaa bila shughuli na mazungumzo yasiyokua na ulazma. Tunatathmini tabia zetu, kujifikiria kua tupo mbele ya Mwenyezi Mungu.

TARAWEH YA KWANZA

Ilikua ni usiku wa ramadhan katika kipindi cha furaha.zilikua zimebaki siku saba tu kabla ya kufikia mwisho wa Ramadhan. Hadi siku hiyo Mtume Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikua akikaa nyumbani kwake baada ya kuongoza swala ya I'shaa. Ingawa, usiku huo kwa mara ya kwanza, alitoka nje tena na kuongoza swala ya taraweh. Swala ya taraweh iliisha ndani ya theluthi ya usiku kupita.

Siku iliyofuata, habari kua Mtume(Rehma na Amani ziwe juu yake) aliswalisha swala ya taraweh zilisambaa. Ingawaje hakuswalisha swala ya taraweh usiku huo.

Siku iliyofuata aliswalisha tena swala ya taraweh. Swala iliswaliwa hadi usiku wa manane. Na siku iliyofuata hakuswalisha tena swala ya taraweh.

Na mwisho zilipobakia siku tatu kabla ya ramadhan kuisha, aliswalisha tena swala ya taraweh na ilidumu kwa usiku mzima. Japokua hakuswalisha tena swala ya taraweh kuepusha hatari ya kuchanganya na swala za faradhi. Alishauri kila mmoja aswali taraweh nyumbani kwake.

Utaratibu wa kuswalia taraweh misikitini kwenye mkusanyiko wa watu ulianza katika kipindi cha ukhalifa wa sayyidiya Ummar.





USIKU WA CHEO (LAILAT AL-QADIR) C

C Kama iliyokua mwezi wa ramadhan una nafasi maalum mionganini mwa miezi mingine, usiku wenyewe cheo una nafasi maalumu mionganini mwa usiku nyiningine. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "kwa hakika tumeteremsha ujumbe huu(Quran) katika usiku huu wenyewe cheo kitukufu. Je, ni nini kitakachokujulisha usiku wa cheo ni nini? Usiku wenyewe cheo ni bora kuliko miezi elfu moja. Huteremka malaika na Roho katika huo kwa idhini ya Mola wao Miezi kwa kila jambo. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri!" (Qadr 97; 1-5)

C Usiku wenyewe cheo ni usiku uliobarikiwa. Ni muda ambao rehma na Baraka za Mwenyezi Mungu zinateremka, madhambi ya waislam yanasaamehewa na dua za waumini zinajibowi.

C Mtume alikua akitumia muda mwangi katika kufanya ibada kwa siku kumi za mwisho za Ramadhan. Sababu moja ni kwamba usiku wa Qadr kua "mbora kuliko miezi elfu" ni mionganini mwa masiku haya.

C Tunatakiwa kutumia ipasavyo siku kumi za mwisho za Ramadhan, hususan usiku wa 27. Tunalazimika kujaribu kupata radhi za Mola wetu katika usiku wenyewe cheo inayokadiriwa kua na thamani kuliko maisha yote, ambayo ni miaka 83. Tunalazimika kutambua thamani ya usiku huu ambaa aya za mwanzo kabisa za Quran ziliteremka ndani yake na jua kwa waislam ikaangaza. Tunatakiwa kuutumia kwa;

- ⌘ Kuhudhuria mawaidha misikitini,
- ⌘ Kusoma Quran,
- ⌘ Kuswali swala za faradh,
- ⌘ Kuomba dua,
- ⌘ Kumswalia Mtume wetu
- ⌘ Tunatakiwa kufaidika na usiku huu wenyewe cheo kwa kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kutokana na madhambi yetu na hivyo kutukuza thamani ya usiku huo.



Mtume wetu kipenzi amesema:

"Madhambi yote ya mtu yanasaamehewa ikiwa kautumia ipasanyo usiku wenyewe cheo kwa kuamini katika ubora wake malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee."

(Bukhari, Iman, 25)



"Siku moja mmbora wake Bi Aisha alimuuliza Mtume wetu; "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ikiwa ninajua ni upi usiku wenyewe cheo, ninatakiwa niseme nini wakati huo? Mtume wetu akamfundisha dua ifuatayo, "Ewe Mwenyezi Mungu, wewe ni msamehevu wa wasamehevu na unapenda kusamehe, ninaomba unisamehe."

(Tirmidhi, Daavat, 84)



Dua ya usiku wenyewe cheo(lailat al-qadir)

اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاغْفِرْ عَنِي

Arabic Transliteration:

"Allahumma innaka `afuwun tuhibbul `afwa fa `fu `annil"

"Ewe Mwenyezi Mungu, wewe ni msamehevu wa wasamehevu na unapenda kusamehe, ninaomba unisamehe."



SHEREHE YA KUMALIZA MWEZI WA RAMADHANI (EID AL-FITR)

Uislam umetangaza kua ni faradhi kufunga mwezi wa Ramadhan. Na ikatangaza kua siku ya kwanza ya swawwal ni siku ya sikukuu kwa waislam.

Katika siku za mwisho tunahuzuni kua Ramadhani inakwisha lakini pia tunafurahi kua Eid al-fitr inakuja. Tunatumia siku za mwisho za ramadhani tukijiiliza kama tumeitumia Ramadhan ipasavyo na tunaomba Mwenyezi Mungu atufikishe Ramadhan ijayo na pia tunafanya maandalizi kwa ajili ya sikukuu ya Eid. Asubuhi na mapema tunavaa nguo zetu na kwenda msikitini. Tunaanza sikukuu ya Eid kwa kuswali swala ya Eid na kuonyesha shukran zetu za dhati kwa Allah (SW).

Eid sio siku ya likizo bali ni siku ya Amani na furaha ambayo inasherehekewa pamoja. Katika siku ya Eid, tunashukuru likizo ya wazee wetu na kupata mawaidha yao mazuri. Tunatembelea marafiki na familia zetu. Tunawapa salamu za Eid watu tunaokutana nao.tunaonyesha ukarimu kwa mafukara na mayatima, na kuwajulia hali za afya wagonjwa na wazee. Tunasuluhiha na kupatanisha pande zilizokua zimegombana. Tunadumisha urafiki na udugu katika sherehe hizi. Rehema, huruma na hisia za uaminifu zinajengeka. Miyo yetu inafunguka kwa masikini na wale waliokosa bahati.

MAISHA YA MTUME KATIKA KIPINDA CHA RAMADHANI

Habari njema toka kwa Mtume wetu kuhusu mwezi wa Ramadhan

Mwalimu wetu Mtume alitamani kuurefusha mwezi wa Ramadhan. Alikua furahani pale ilipofikiya miezi mitatu mitakatifu na alikua akiomba dua hii: **"Mola wetulifanye miezi ya Rajab na Shaaban Baraka kwetu, na utujaalie kuifikia Ramadhan."**

Alikua akifunga mwezi wa Rajab na Shaabanbtofauti na kawaida. Alikua akitoa habari njema kuhusu Ramadhan akisema:

"Pindi mwezi wa Ramadhan unaopofika, milango ya pepo inafunguliwa na milango ya

moto inafungwa, na mashetani wanafungwa minyororo."

"Katika pepo ipo milango nane, mionganini mwao upo mlango unaoitwa Al-Rayyan, ambao hawataingia humo isipokua waliofunga. Itatangazwa: wako watu wale walikouwa wakifunga waingie ndani yake? - na pindi mtu wa mwisho atakapoingia milango itafungwa na hakuna mwingine atakayeingia tena humo. Kuna kinywaji watu watakaoingia katika pepo hii watapewa ambacho hawatasikia kiu tena."



SAHUR (DAKU) YA MTUME WETU

Mtume wetu alikua akieleza umuhimu wa kipekee wa muda wa daku (sahur). "Msijilaumu kuamka kwa ajili ya kula daku, kwa sababu chakula cha daku kimebarikiwa." Kwa mfano usiku mmoja alipokua anamuita mmoja kati ya maswahaba masikini, Irbad Ibn Sariyah aliye kua amefanya makazi yake karibu na msikiti wa Mtume na mmoja kati ya waliokua na furaha na wa mwanzo kuingia katika uislam,

"Njoo na ujumuike katika chakula hiki chenye Baraka!"

Mara nyiningine alikua akielezea juu ya kuamka kwa ajili ya chakula cha daku alisema:

"Chakula cha daku kina Baraka, msikipuuzie. Pata chochote walau funda la maji. Mwenyezi Mungu Mtukufu na malaika wake humimina Baraka kwa wale wanaokula daku."

Futari Ya Mtume Wetu

Mola wetu mlezi hufurahishwa sana kuona huruma na heshima za waja wake. Muda wa kufuturu ni muda muafaka wa kuonyesha huruma pamoja na heshima hiyo. Kwa sababu hii Mtume wetu alikua akitilia maanani sana katika muda wa kufuturu.

Alikua anafurahi kama watoto na kusema wazi kua kuwahi kufungua mapema inamfurahisha Mwenyezi Mungu na inaleta kheri na fadhilli:

"Kwa kuwa walikua wanaonyesha jitihada kuwahi kufungua mapema punde tu muda

unapowadia, wafuasi wangu hawatokua mbali na kutoka katika njia ya kheri na fadhilli." (Bukhari, Sawm, 45)

Mtume wa Mwenyezi Mungu, alisema kua dua itakayoombwa kabla ya kufuturu hua hairejeshwi, dua wakati wa kufuturu inasema:

"Ewe Mwenyezi Mungulkwa ajili yako nilifunga na kwa chakula chako ninafungua swaumu yangu." Kisha alikua akifungua swaumu yake kwa tende kama ilikuwepo, ama maji. Alituusia pia tufanye hivyo.



Ukarimu Wa Mtume Wetu Ndani Ya Mwezi Wa Ramadhan

Ukarimu unaojulikana vizuri wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ulikua unaongezeka mara dufu katika mwezi wa Ramadhan. Katika miezi mitatu mitukufu alikua mkarimu Zaidi ya "upepo unaoendelea kuvuma." Alikua anagawa kwa waislam chochote aliichokua nacho. Ikiwa

chochote alichoombwa basi mara moja alitoa, na aikiwa hakua nacho basi alikitafuta kwa marafiki zake. Alikua akiwijibu wale waliokua wakimuuliza ni ipi sadaka iliyokua inakubalika Zaidi: "sadaka ambayo inatolewa katika mwezi wa Ramadhan!"



Matendo Ya Ibada Ya Mtume Wetu Ndani Ya Mwezi Wa Ramadhani

Ongezeko ilikua likionekana kwa matendo ya ibada yaliyokithiri ya Mtume wetu katika Ramadhani. Swala ya tarae hili kua ni moja mwa matendo aliyokithirisha kuyafanya Zaidi.

Katika mwezi huu wa ibada, swala, na kumbukumbu Mtume wetu alikua akisoma Quran Zaidi kuliko miezi mingine yote. Kwa mantiki hii, malaika Jibril alikua akija kwa Mtume wetu kila usiku wa Ramadhan na kusomeana Quran Tukufu kila mmoja. Usomaji huu ambaa ulikua akifanyika mara moja kila mwaka, ulifanyika mara mbili katika Ramadhani ya mwisho ya Mtume wetu.

Kuelekewa mwisho wa Ramadhan, pallionekana ongezeko la matendo ya ibada kwa Mtume wetu. Uwezekano wa kuwa usiku wa cheo(lailat al-qadr) ni katika siku za mwisho za ramadhani , hasahasa katika usiku usio wa kawaida(namba tasaj) kama (usiku wa 21,23,25,27 au 29) ulichangia kuongeza jithhada za kutokuukosa usiku huo. Alikua akisema:

"Yoyote atakayefanya ibada katika usiku wenyewe cheo kwa unyenyekevu wa Imani na kutaraji malipo toka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu(sio kwa kujionyesha) hivyo madhambi yake yote ya nyuma yatasamehewa."

Katika kipindi cha siku kumi za mwisho za Ramadhan, Mtume wetu (Rehma na amani ziwe juu yake) alikua akitafakuru katika Masjid Nabawi (Msikiti wa Mtume). Alijishughulisha Zaidi katika kipindi hiki na matendo ya ibada kama vile swala, dua na maombi. Kama kwamba alikua anasema; "Ewe Mola wangu Mlezii! Ninakuja katika mlango wako na siendi mahali pengine hadi unisamehe."

M. Yaşar Kandemir

FUNGA NA KUSOMA QURAN NI WATETEZI WETU

Kupatikana kwa thawabu maalumu za kiroho na utajiri tutakaupata kutokana na kusoma Quran kipindi cha mwezi wa ramadhani, Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na amani ziwe juu yake) alisema:

"Funga na kusoma Quran ni mkombozi wetu".

Funga itasema:

Ewe Mwenyezi Mungu! Nimemzuilla mja wako huyu kutokana na kula na matamano menginekwa siku nzima. Tafadhali nikubalie mdhamana wangu kwake!

Usomaji wa Quran utasema:

Nilimzuilla mja wako huo kutokana na usingizi wa usiku. Tafadhali nikubalie mdhamana wangu kwake!

Kwahiyo vyote viwili vinamuombea mdhamana mtu huyo.

(Ahmad b. Hanbal, Musnad, VI, 188)

RAMADHANI

Ulimwengu umefurika kwa mwanga,
Jaribio kwa kila mja wa Mwenyezi Mungu,
Kwa wale wanaosema mimi ni muumini,
Mwezi wa funga ya Ramadhan.

Inaathiri nafsi ya mtu,
Unabaki na nguvu kama nafsi,
Funga yetu ya ramadhani,
Ni moja kati ya faradhi kubwa tano

Ramadhani ni mwezi wa Quran,
Ni mwezi wa shukurani kwa waumini,
Mwezi huu kwa waislamu,
Ni mwezi wa msamaha, kutafuta njia iliyo sawa.

Ndani ya mwezi huu, kilakona,
Kila familia, inafurahia,
Ni wajibu kwa kila muislamu,
Kufunga kwa siku thelathini.

Uislamu ni ufunuo,
Imani ni furaha,
Kila muda kwa mja aliyefunga,
Ni ibada.

Funga inatoka kwa Mwenyezi Mungu,
Kuutoa moyo kwa Mola,
Mola mtukufu, ametufanya sisi,
Kuifikia Ramadhani ya mwaka huu.

Enver TUNCALI



MASWALI

Tujipime Maarifa Yetu

Sentensi zifuatazo, tizama jedwali lilio NDIO au HAPANA

1. Funga ni ibada muhimu sana inayotukinga sisi kutoptana na NDIO HAPANA kutofanya maasi katika dunia hii na katika moto huko akhera, na inaongoza kwenye msamaha wa madhambi yetu.
2. Kula na kunywa makusudi bila udhuru wowote wakati wa funga ya NDIO HAPANA Ramadhan inahitajia kulipia vyote Qadha na Kaffara.
3. Wazee ambao hawana nguvu za kufunga katika mwezi wa Ramadhani na wagonjwa ambao hawana matumaini ya kupona wanatoa kiwango Fulani cha chakula kwa kila siku ambayo hawawezi kufunga. NDIO HAPANA
4. Funga ya nadhiri kwa ajili ya Mezyezi Mungu huitwa kaffara NDIO HAPANA
5. Kukaa msikitini au katika nyumba ya ibada kwa muda Fulani inaitwa l'iftar NDIO HAPANA
6. Quran tukufu ilianza kuteremshwa katika usiku aliopaizwa Mtume(usiku wa Mi'raj) NDIO HAPANA
7. Funga za wale wanaokula na kunywa kutoptana na kusahau hubatilika NDIO HAPANA
8. Maneno ya Mtume: "funga ni ngao" inamaanisha kwamba funga inatukinga na kufanya maasi na madhambi NDIO HAPANA

Tujipime Maarifa Yetu

1. Ni lipi kati ya matendo yafuatayo halihusiani na mwezi wa ramadhani?
 - a) Kwenda hija.
 - b) Kufunga.
 - c) Mwanzo wa kushushwa kwa Quran
 - d) Usiku wenye cheo
2. Ni lipi kati matendo yaliyoordheshwa hapa chini si katika faida za funga?
 - a) Kwa kufunga tunapata mapenzi na radhi za Allah (SW).
 - b) Kwa kufunga tunawasaidia maskini.
 - c) Kwa kufunga tunakaa mbali na kufanya maasi na madhambi, amabyo yanatukinga na moto wa jahanam.
 - d) Kwa kufunga tunajifunza kua na uvumilivu



3. Ni lipi kati matendo yaliyoorodheshwa hapa chini ni mionganoni mwa funga ya faradhi?
 - a) kukithirisha sana funga
 - b) kufunga katika mwezi wa Muharram.
 - c) kufunga Ramadhan
 - d) kufunga jumatatu na alhamis.
4. Ni neno gani linatumika kwa wakati ambapo usiku unaisha na mchana unaanza?
 - a) Fajr b) Sahur c) Iftar d) l'tikaf
5. Ni lipi kati matendo yaliyoorodheshwa hapa chini haibatilishi funga?
 - a) Kula kitu ambacho hua si chakula kwa kawaida.
 - b) Kumeza mate yako mwenyewe
 - c) Kumeza chembe ya theluji au kijiwe kwa kudhamiria.
 - d) Kumeza maji bila kukusudia wakati unatia wudhu.
6. Ni lipi kati matendo yaliyoorodheshwa hapa chini inabatilisha funga na inahitaji kulipwa siku nyininge(Qadha)?
 - a) Maji kuingia sikioni bila kudhamiria wakati wa kuoga
 - b) Kuingiwa na moshi au vumbi kooni bila kukusudia
 - c) Kufungua kwa lazima kwa nguvu au kutokana na kutishiwa.
 - d) Kutapika pasina kudhamiria.
7. Ni ipi sababu iliyoorodheshwa hapa chini ni ya muhimu sana kwanini waislam wanafunga mwezi wa Ramadhan?
 - a) Tamaa ya kudhibiti nafsi zao.
 - b) Tamma ya kuishi maisha yenye afya.
 - c) Tamaa ya kujenga mahusiano mazuri na wenzetu.
 - d) Kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
8. Ni lipi kati matendo yaliyoorodheshwa hapa chini haibatilishi funga?
 - a) Kufungua swaumu ukidhania kua muda wa kufungua umewadia na kumbe bado haujawadia
 - b) Kuoga ili kijipooza mwili.
 - c) Kumeza chakula ambacho kilikua kimebaki baina ya meno ambacho ni kikubwa kuliko punji ya choroko.
 - d) Kumeza chembe ya theluji au kipande katika mvua ya mawe au tone la mvua bila kukuksudia.
9. Ipi kati ya sababu iliyoorodheshwa hapo chini haikubaliki kama sababu ya kuvunja funga?
 - a) Kupata mgeni nyumbani
 - b) Kupata tishio la kuuliwa au kujeruhija
 - c) Kua vitani dhidi ya maadui.
 - d) Kua msafiri

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyopo katika mabano.

(cheo/rehma/nisamehe/stini na moja/msamaha wa madhambi/qadha/nadhiri/afya/al-rayyan)

1. Mwezi wa Ramadhan ni mwezi ambao kuna.....mwanzoni, kunakatikati.....na kuna kuongolewa katika adhabu ya moto mwishoni.
2. Fungeni na mpate.....
3. Kaffara kwa kuvunja swaumu ya mwezi wa ramadhan kutokana na kujamiiana ni kufunga siku.....
4. Mtu ambaye anaendelea kula na kunywa kwa kudhani kua funga yake imeharibika baada ya kula au kunywa kitu kutokana na kusahau lazima aliye gunga hii kama funga.....
5. Funga ya nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu inaitwa
6. Mtume wetu aikua akiswali katika usiku wenye.....kama: "Ewe Mwenyezi Mungu!wewe ni msamehevua na unapenda kusamehe,tafadhalli.....mimi!"
7. "Katika pepo ipo milango nane, mionganoni mwao upo mlango unoitwa ambao hawata-ingia humo isipokua waliofunga. Itatangazwa: wako watu wale waliokua wakifunga waingie ndani yake?- na pindi mtu wa mwisho atakapoingia milango itafungwa na hakuna mwingine atakayeingia tena humo. Kuna kinywaji watu watakaoingia katika pepo hii watapewa ambacho hawatasikia kiu tenda".





DARAJA BAINA YA MATAJIRI NA MASIKINI:



ZAKA



- ✿ *Sadaka na zaka*
- ✿ *Maana ya zaka*
- ✿ *Faida ya zaka*
- ✿ *Kanuni zinazohusiana na zaka*
- ✿ *Kwa mambo yapi ambayo tunatakiwa kua*
- ✿ *Wema wa Mtume wetu*



JARIBIO LA SHUKRANI

Mwalimu wetu Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alikua akiwasimulia hadithi za zamani kwa marafiki zake.

Moja kati ya hadithi hiyo ilikua hivi:

"Miongoni mwa wana wa Israel, walikuepo watu watatu; mmoja alikua na ngozi yenye vipele, mmoja allikua na upara na mwingine alikua kipofu. Mwenyezi Mungu alitaka kuwapa mtihani aliwatumia malaika katika umbile la binadamu.

Malaika alikuja kwa yule mmoja mwenye ngozi yenye vipele na kumuuliza:

— Ni kitu gani ambacho unakitaka Zaidi?

Akajibu:

— Rangi nzuri ya ngozi, ngozi nyororo, na kuiondoshaa hii hali ambayo inawafanya watu

wajitenge mbali nami, kutokana na hilo malaika alipapasa ngozi.

Kwa kushikwa na malaika, ngozi ile yenyewe vipele ikapotea. Wakati huu malaika akamuuliza:

— Ni kitu gani unataka kukimiliki Zaidi? Yule mwanaume akajibu:

— Ngamia.


Baada ya kumpa ngamia mwenye mimba, malaika akamuacha na dua hii:

— Mwenyezi Mungu amjaalie huyu ngamia awe na manufaa kwako!

Mwenyezi Mungu amjaalie huyu ngamia awe na manufaa kwako? Kisha malaika akaenda kwa yule mwenye kipara na kumuuliza

— Ni kitu gani ambacho unakitaka Zaidi? Na mwanaume yule akasema:

— "Kuwa na nywele nzuri na kuondokana na hali hii ambayo inawafanya watu wajitenge mbali nami. Malaika akamshika



kichwa chake na upara ukatoweka. Alikua na nywele nzuri za kuvutia.

Malaika akamuuliza:

— Ni kitu gani unataka kukimiliki Zaidi?

— Ng'ombe, yule mwanaume alijibu. Malaika akampatia kundi kubwa la ng'ombe wenyewe mimba kisha akamuombea dua:

— Allah(SW) amjaalie hawa ng'ombe wawe na manufaa kwako. Kisha malaika akaenda kwa yule kipofu na kumuuliza:

— Ni kitu gani ambacho unakitaka Zaidi?

— Na mwanaume yule akasema:

— Ninataka Mwenyezi Mungu anirudishie nuru katika macho yangu ili nipate kuwaona watu. Pindi malaika alipomshika macho akaanza kuona. Malaika akamuuliza:

— Ni kitu gani unataka kukimiliki Zaidi?

— Kundi la kondoo, alijibu. Malaika akampa kundi la kondoo wenyewe mimba.

Ngamia, ng'ombe na kondoo wote wakawa na kizazi chao. Kwa muda wote wakawa wamejilimbikizia utajiri. Mmoja wao akawa nabonde liliojaa ngamiaa na mwingine akawa na bonde liliojaa ng'ombe na mwingine akawa na bonde liliojaa kondoo.

Baadaye malaika akatokea kama mtu mwenye ngozi yenye mapele kwa mwanaume yule aliye kua na tatizo kam ahilo mwanzoni kisha akamwambia.

— "Mimi ni mtu masikini, nimekosa namna ya kuendelea na safari yangu. Ninaweza kuendelea kwanza kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kwanza kisha wewe. Ninahitaji ngamia mmoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu aliye kupa wewe hii ngozi nzuri, nyororo na utajiri wote huu".

Mtu yule alikataa na kusema:

— "Haiwezekani. Kuna watu wengi sana ambaao wana haki na mali hii. Kuna sehemu nyingi sana za kutoa mali hizi hadi ije kufika zamu yako. Baada ya hili malaika akasema:

— Nadhani ninakujua wewe. Wewe si yule mtu masikini uliyekua na mapele na watu walijitenga nawe na ambaye Mwenyezi Mungu amekupa utajiri? Mwenyezi Mungu amekupa afya na mali.

Lakini bwana yule alikataa ukweli ule na akasema:

— Umeongea sana; mali hizi nimezirithi kutoka kwa mababu zangu. Malaika akamlaani na kusema:

— Kama unaongopa Mwenyezi Mungu akurudishe katika hali yako ya mwanzo.

Kisha malaika akajibadilisha na kua mtu mwenye kipara na akaenda kwa bwana yule mwenye kipara mwanzoni na kusema sawasawa na bwana yule aliye kua na kipara akajibu kama yule mwingine. Malaika akamuacha na kusema:

— Kama unaongopa Mwenyezi Mungu akurudishe katika hali yako ya mwanzo.

Kisha malaika akajibadilisha na kua kipofu kisha akaenda kwa bwana yule aliye wahili kua kipofu mwanzoni akamwambia:

— Mimi ni msafiri masikini na sina namna ya kuendelea na safari yangu. Ninaweza kuendelea kwanza kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kisha wako. Ninahitaji kondoo kwaajili ya Mwenyezi Mungu aliye kupa tena nuru ya macho yako. Yule bwana akasema:

— Hapo zamani nimewahi kua kipofu, na Mwenyezi Mungu akanifumbua macho yangu. Niliwahi kua masikini na Mwenyezi Mungu akanfanya tajiri. Chukua chochote unachohitaji na uache kile usichohitaji. Ninaapa kua sitafanya mambo kua magumu kwako. Kwa hili malaika akasema:

— Tufanye kila kitu kua chako. Huu uliku ni mtihani kwako. Mola wako amekuridhia wewe. Wengine wawili wamefeli na wamepata hasira ya Mwenyezi Mungu, na malaika akatoweka. (Bukhari, Anbiya 51; Muslim, Zuhd 10)

NANI NI MMILIKI HALISI WA MALI ZETU?

Uislam unahamasisha watu kufanya kazi na kujipatia kipato kwa njia ambazo ni za halali. Japokua hatutakiwi kusahau uhalisia huu:

Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anayetupa Baraka zote hizi. Ni mmiliki halisi wa mali na vitu vyetu. Ametuamini sisi na Baraka zote hizi kwa kipindi Fulani tu cha muda. Anataka kutupatia majaribio ikiwa tunatumia Baraka hizi katika njia inayomridhisha au isiyomridhisha ametuamrisha kuchangia kiwango Fulani cha mali zetu kilichozidi matumizi na watu masikini na wenyewe uhitaji.

Tunafaaluu jaribio hilo kwa kutumia mali zetu kama ambavyo Mwenyezi Mungu alivyotuamini sisi kutumia katika njia anayotaka tutumie.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

"Sema: Ewe Mwenyezi Mungu uliyemiliki ufalme wote!wewe humpa ufalme umtakaye na humuondolea ufalme umtakaye,humtukuza umtakaye na humwangusha umtakaye.kheri yote iko mikononi mwako. Hakika wewe ni muweza wa kila kitu."

(Ali 'Imran, 3: 26)



SADAKA NA ZAKA

Kutumia neema ambazo Mwenyezi Mungu ameturuzuku katika njia inayompendeza yeye inaitwa "Infaq" katika uislam. Njia bora Zaidi ya infaq ni kutoa sehemu katika neema uliojaaliwa kama zaka na sadaka.

Sadaka ni msaada wa hiyari unaotolewa na muislam kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Tunaposema sadaka, mara nydingi inaeleweka kama msaada wa kifedha unaotolewa kwa maskini. Ingawa, inamaana pana Zaidi ya fedha na msaada wa vitu. Mtume wetu ametuambia kua hata matendo yetu mema yanahesabika kama sadaka. Alitupa mifano mingi ya aina za sadaka ambayo yana thamani kama sadaka kwaajili ya thawabu/malipo yake. Hii ifuatayo ni mifano ya sadaka kwa mujibu wa maelezo ya Mtume wetu:

- ◆ Kuchangia kwa wenge uhitaji ni sadaka
- ◆ Kutoa muda wa ziada kwa mtu unayemda na mwenye ugumu wa kulipa ni sadaka.
- ◆ Kumshauri mtu katika matendo mema na kuwaonya kutokana na matendo maovu ni sadaka.
- ◆ Kuondosha kitu cha hatari katika barabara ni sadaka.
- ◆ Kumuelekeza mtu njia ni sadaka.
- ◆ Kuwasaidia wale wanaojaribu kuvifikia vyombo vyao vya usafiri au kuwasaidia kubeba mizigo yao ni sadaka.
- ◆ Kuwapatanisha watu waliokua hawaelewani ni sadaka.
- ◆ Kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusema "La illaha illallah" na "Alhamdulillah" ni sadaka



- ◆ Kuwa na tabia njema ni sadaka.
- ◆ Kuongea vizuri ni sadaka.
- ◆ Kupata elimu na kuifundisha ni sadaka.
- ◆ Kila hatua kuelekea msikitini kuswali ni sadaka.
- ◆ Kupanda mti ni sadaka.
- ◆ Kila kitu anachokifanya mwanamume kumfurahisha mkewe ni sadaka.
- ◆ Kila kitu anachokifanya mwanamume kumfurahisha mkewe ni sadaka.

Msaada wa mtoto na matendo mema kwa baba,mama na ndugu zake ni sadaka.

Kwa kifupi;

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:


"Enyi mliaoamini! Tumieni (Neema) tulizokupeni..."

(al-Baqara 2: 254)

Kila jambo jema muislam analofanya kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu ni sadaka." (Bukhari, Adab, 33).

Tunaona kuwa sadaka ina maana pan asana katika uislam. Ili muislam atoe sadaka, sio lazima awe tajiri. Kila muislam anaweza kutoa sadaka kwa kuzingatia maana yake au anaweza akapata thawabu za sadaka yake kwa kuwa na muenendo mzuri. Vile vile infaq ina wigo mkubwa pia.

Mola wetu Mlezi amefanya faradhi kwa waislam wenye kiwango fulani cha mali kugawana baadhi yake na wale wenye uhitaji. Tendo hili la ibada, linalofanywa kwa kutoa mali na moja katika nguzo za uislam linaitwa Zakat.



Siku moja mwalimu wetu Mtume(S.A.W):

- Kutoa sadaka ni jukumu la kila muislam.
- Juu ya jambo hili marafiki zake wakasema:
- Ni kipi mtu anaweza akafanya ikiwa hana kitu cha kutoa kama sadaka?
- Mtume wetu akasema:
- Mtu huyo anaweza akafanya kazi na anaweza akawa na manufaa kwake yeye na kutoa kama sadaka.
- Vipi sasa endapo hawesi kufanya kazi au hajapata kazi ya kufanya?
- Anaweza akawasaidia wale wenye uhitaji,
- Vipi kama haswezi kufanya hilo pia?
- Anaweza akashauri kufanya matendo mema.
- Vipi endapo hataweza kufanya hivyo pia?
- Anaweza akajitenga mbali na matendo maovu. Hata hili laweza kua sadaka kwake.

(Bukhari, Zakat 30)



ZAKA NI NINI?

 **Zaka** ni neno linalotumika kuwa ni kiasi Fulani cha pesa kinachotolewa kwa kundi Fulani la watu kutoka katika aina Fulani ya mali ambacho kimefikia kiwango flani.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

"Na shikeni sala na toeni zaka; na kheri mtakazo jitangulizia nafsi zetu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyafanya."

al-Baqara, 2: 110)

Zaka ni aina ya utakaso.

Moja kati ya maana za kifasihi zaka ni "utakaso." Kutoa kiasi fulani katika kipato na mali za mtu kwa wenyewe uhitaji inamtakasa mtu mali yake na hali yake kiroho. Inamtakasa mtu kutohana na madhambi na kughafilika. Inatibu maradhi ya kupenda Zaidi vitu vya kidunia kuliko vya kiroho kwa binadamu.

"Chukua katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehma."

(Tawbah, 9: 103)

FAIDA ZA ZAKA

ZAKA

- Inatusaidi sisi kumshukuru Mwenyezi Mungu ipasavyo kwa mali zetu.
- Inazidisha hisia za wema, rehma na ukarimu
- Inatakasa mali zetu.
- Inatulinda na kughafilika na ubinafsi.
- Inadumisha mshikamano na upendo katika jamii yetu.
- Inafanya mali zetu zibarikiwe na ziongezeke.
- Inalinda mali zetu kutohana na matatizo na ubaya.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

"Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja ilio chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua."

(al-Baqara, 2: 261)

Ni lazima tumshukuru Mola wetu Mlezi kwa neema zote alizotujaalia. Kutumia neema tulizo neemeshwa kama atakavyo Mwenyezi Mungu ni namna nzuri ya kuonyesha shukurani zetu kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kutoa robo ya mali zetu kwa wenge uhitaji, tunafanya ibada na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mali alizotur uzuku. Tusitaraji shukran kwa yoyote yule kutokana na zaka tuliyoitoa. Kwa hiyo, zaka inatufanya tumshukuru Mwenyezi Mungu ipasavyo kwa mali alizotujaalia.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na huwalisha chakula, juu ya kikipenda kwake, masikini na mayatima, na wafungwa. (Husema), "Hakika sisi tunakulisheni kwa wajih wa Mwenyezi Mungu. Pekee. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yeny shida na taabu." Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari za siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha."

al-Insan, 76: 8-11)

Kwa vile watu matajiri wana namna nyangi, wanaweza wasieleewe hali ambayo wanaipitia masikini. Tunapowaangalia watu masikini na wenge uhitaji wa kuwapa zaka, tunaweza kupata wasaa wa kuona kwa namana ya karibu Zaidi. Tunaweza kuona ugumu na matatizo katika maisha yao wanayopitia. Tunapunguza matatizo ya masikini na wenge uhitaji kwa kuwasaidia. Kuchangia tulivyojaaliwa katika njia hii kunadumisha hisia za **wema, huruma na ukarimu.**

Mtume wetu kipenzi amesema:

"Endapo utataka kua na moyo mwepesi, walishe masikini, wajali mayatima....."

(Ahmed b Hambel, II, 263)



Mwenyezi Mungu mtukufu anatufahamisha kuwa masikini na watu wenge uhitaji wana haki katika mali za matajiri alliposema, "na katika mali yao na wanavyovimiliki (Inakumbukwa) ipo haki ya mwenye kuomba na asiyeomba" (Zariyat, 51; 19) ikiwa hatutawapa fungu wenge haki nalo, basi tunaiba haki yao. Na ikiwa imetokea tumeiba haki za watu wengine. Pesa ambayo ni haramu/ iliyokatazwa inachanganyika na mali zetu. Mali iliyochanganyika na haramu haiku twahara. Kwa kuwapa fungu lao masikini na wenge uhitaji, tunajikinga haramu isichanganyike na mali zetu. **Kwa hiyo, zaka inatakasa mali zetu.**

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Chukua katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehma..."

(Tawba, 9: 103)



Zaka na sadaka inadhibiti mapenzi yetu juu ya vitu vya kidunia. Inatudhibiti kuvitumia katika njia isiyokua sahihi. Inatufundisha kua pesa na mali sio kila kitu. Inatufanya tuhisi hisia nzuri ya kuchangia vile tulivyonavyo na wengine. Zaka inatukinga kutokana na **uchoyo na ubinafsi**. Inatufanya tuwe binadamu wenyewe utu ambaو si wabinafsi, tunaowafikiria wengine, na kutumia pesa zake kwa furaha ya watu wengine.

Kipenzi chetu Mtume amesema:

"Yule anayetoa zaka, anayehudumia vizuri wageni wake, na yule anayewasaidia wallopata matatizo anajisaidia kutokana na uchoyo."

(Taberâni, Mu'cemü'l-Kebir, IV, 256)

Zaka ni daraja linalotawanya mali kwa masikini. Inafanya mawasiliano kati ya masikini na matajiri kuwa imara. Inaondosha wivu. **Inadumisha mshikamano na upendo katika jamii zetu**. Matajiri wanahisi wema na huruma kwa masikini na masikini wanaonyesha heshima kwa matajiri. Mshikamano, ushirikiano na muunganikano unakua hai katika jamii. Kwahiyo zaka inatimiza mahitaji ya masikini na inaondosha migongano inayoweza kutokea katika jamii.

Mtume wetu kipenzi anasema:

"Zaka ni daraja katika uislam."

(Heysemi, Medjmau'z-zevaid, I, 480)

Zaka na sadaka **inalinda mali zetu dhidi ya matatizo na uovu**. Msemo maarufu sana mionganoni mwa waturuki, "sadaka kiasi kidogo inaondosha matatizo mengi sana" inaelezea uhalsia huu. Hii ni kwa sababu kupokea habari njema ya masikini na wenyewe uhitaji inaondosha matatizo na maovu. Rehma ya Mwenyezi Mungu inawamiminikia wale wanaotoa sadaka na zaka.

Mtume wetu kipenzi anasema:

"Zilindenî mali zenu na zaka."

(Beyhaki, Şuabü'l-imân, V, 184)

Zaka inahakikisha kua mali zetu zinabaki nyingi. Katika aya, "na mnachokitoa kwa riba ili kiongezeke katika mali ya watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mnachokitoa kwa zaka kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, basi hao ndio watakao zidishiwa." (Rum 30:39) Mola wetu Mtukufu anatufahamisha kua maliza wale wanaotoa zaka na sadaka kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu zitaongezeka. Katika msingi wa ongezeko hili, kuna dua njema za malaika na za wale wenye nyoyo zenye furaha wanaopokea zaka na sadaka. Dua njema ya masikini, mafukara na malaika ni chanzo cha Amani kwa matajiri.

Mtume wetu kipenzi anasema:

"Kila asubuhi malaika wawili wanakuja katika dunia, mmoja wapo anaomba dua, "Mola wangu, ihifadhi mali ya wale wanotumia katika njia nzuri. Na mwagine anasema, "Mola wangu, iteketeze mali ya yule aliyekua mchoyo!"

(Muslim, Zakat, 57)



JE, YUPO MWINGINE ANAYETOA ZAIDI?

Katika kipindi cha ukhalifa kwenye uongozi wake Abu Bakr, ukame uliikumba Madina. Watu hawakuweza kupata ngano ya kuokea mikate. Wafanyabiashara wa Madina walipoiona hali hii wakawekeza pesa katika biashara ya ngano.

Kwa muda fulani, kiongozi wake Uthman alituma msafara wa biashara kwenda Damascus kuleta ngano Madina uliobebwa na ngamia mia moja. Ngano iliyolewa na kiongozi wa umma Uthman ingetosheleza kugawanywa kwa watu wote wenye uhitaji zaidi wa ngano. Ni kwa sababu kwa kipindi hiko mji wa Madina haukua na watu wengi sana.

Baadhi ya wafanyabiashara waliongea na kiongozi wa umma Uthman. Walitaka kununua ngano iliyokua imenunuliwa kutoka Damascus. Walikua wako tayari kununua kwa dau la dirham 4 kwa kila kilo moja ya ngano. Hata hivyo, kiongozi wa umma Uthman aliona thamani hii haitoshi. "yupo mwengine anayetoea zaidi!" alisema. Hakutaka kuza ngano yake kwa mtu yoyote. Kwa namna hii, wafanyabiashara wakaongeza dau Zaidi. Lakini matokeo yake wakapata majibu yale yale kutoka kwa kiongozi wa umma: "Yupo mwengine anayetoea zaidi!" mwishoni wakapanda dau hadi kufikia dirham 7 kwa kilo moja ya ngano. Hii ilikua ni kiwango cha juu zaidi ambacho wangeweza kutoa. Lakini kiongozi wa umma Uthman hakua

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Ambao hutoa wanapokua na wasaa na wanapokua na dhiki....."

Ali 'Imran, 3: 134)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Mfano wa wanaotumia mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni mfano wa punji moja iliyochipuza katika mashuke saba. Katika kila shuke zimo punji mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa na mwenye kujua."

al-Baqara, 2: 261)

akisema chochote isipokua; "yupo mwengine anayetoea zaidi!"



Baadhi ya wafanyabiashara walifikiri kua tabia yake ni kutaka kujaribu kupata faida katika hali hii na kujipatia pesa nydingi sana. Walikatishwa tamaa na jinsi alivyojionyesha hali ya kua watu walikua na uhitaji.

Mwishihi walikata shauri kumwambia kiongozi wa umma wa wakati huo khalifa Abu Bakr. Walipanga kumuuliza khalifa kutafuta njia ya makubaliano kati yake na kiongozi wa umma Uthman.

Walimwambia hasa kile kilochotokea khalifa Abu Bakr na aliwasikiliza hadi mwisho na kuwaambia:

"Kuna kitu kilikua hakija fahamika katika hili. Nadhani hamkuelewa ni kitu gani kiongozi wa umma Uthman alikikusudia. Ni mkwe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni rafiki yake peponi. Si mtu wa kutaka kupata faida kutoka kwa watu wenye uhitaji na kupata faida kwa hillo. Lazima kutakua na sababu kwanini alijionyesha hivyo. Twendeni pamoja na tujifunze ni kitu gani alikua yeye amekimaanisha."

Walikwenda kwa pamoja kwa kiongozi Uthman. Kiongozi wa umma khalifa Abu Bakr

akamuuliza kiongozi Uthman kwanini hakuza ngano yake kwa thamani iliyopendekezwa.

Jibu la kiongozi Uthman kwa swali hili lilikua na maana na lenye mashiko:

"Ewe khalifa wa Mwenyezi Mungu! Walitaka kununua kilo moja ya ngano kwa dirham 7. Kwa maneno mengine wangenipa saba kwa moja. Ninataka kuza kwa yule anayeweza kunipa mia saba kwa moja. Je, si Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetuhidi kutupatia thawabu mia saba kwa jambo jema moja? Kwanini niwauzie wao ngano yangu hali ya kua kuna biashara yenye faida kupitiliza?"

Kwa jibu hili wafanyabiashara walipigwa na butwaa. Waligundua makosa yao waliyofanya kwa kudhania mawazo mabaya dhidi yake.

Kiongozi wa umma alitoa ngano yote iliyobebwa na ngamia mia moja kwa watu wa mji wa Madina kama sadaqa. Aliwafanya masikini na wenye uhitaji wafurahi. Kwa hiyo ukame katika mji wa Madina ukapata suluhisho.



Nani anayewajibika kutoa zaka?

* Kila muislam ambaye

ana mali kwa
misingi ya vipimo
vya dini

ni wajibu
kwake kutoa
zaka

mara moja kwa
kila mwaka.


Ni kipimo gani cha kuwa na tajiri kwa katika Uislam?

Mtu ambaye anauwezo wa kutoa zaka kiwango cha chini cha mali (Nisab) mbali na matumizi yake ya lazima anahesabika kama tajiri katika uislam.

Kiwango cha Nisab ni cha chini cha kua tajiri katika uislam. Japokua, kwa zaka kua wajib (Faradhi), kiwango hiki cha mali kinatakiwa kiwe kinamilikiwa na muhusika kwa takribani mwaka mmoja (siku 354)

Yapi ni mahitaji ya lazima?

Vitu vifuatavyo kama si vya biashara vinajumuishwa kama mahitaji ya lazima:

- ➲ Nyumba
- ➲ Samani za ndani,
- ➲ Mavazi,
- ➲ Usafiri (Gari),
- ➲ Vitabu,
- ➲ Vitu vinavyohitajika kwenye kazi
- ➲ Akiba ambayo inatosheleza matumizi ya familia kwa muda wa mwaka mzima.



Ni kiwango cha Nisab (kiwango cha kulinwa zaka) na kiasi cha zaka.

-  Wale ambao ni matajiri kwa mujibu wa vipimo vya uislam na ambao viwango vyao vya mali havijatetereka kwa mwaka mzima au zaidi ni lazima watoe zaka.
-  Kiwango cha nisab kinahesabiwa baada ya kutoa mahitaji ya lazima.
-  Kiwango cha nisab na zaka kinabadilika kutegemeana na aina ya bidhaa.

Kiwango cha nisab na kiasi cha zaka kwa wafanyabiashara.

Aina ya bidhaa	Kiwango cha nisab	Kiwango cha zaka
Dhahabu	Gramu 80,18 (Miskal 20)	Robo (2.5%)
Fedha	Gramu 561 (dirham 200)	
Bidhaa za biashara	Kiasi ambacho ni sawa na gramu 80,18 ya dhahabu	
Fedha taslim	Kiasi ambacho kipo sawa na gramu 96 za dhahabu	

 Hakuna hitajio la zaka katika mapambo ya wanawake ya dhahabu na fedha. Ikiwa jumla ya thamani yake ni chini ya gramu 80,18 ya dhahabu.



Kiwango cha nisab na kiasi cha zaka kwa wanyama.

Kiwango cha zaka kwa wanyama kinabadilika kutohata na aina ya wanyama na idadi ya wanyama:

- * **Kondoo na mbuzi:** kwa kondoo na mbuzi inakadiriwa kufikia 40 hadi 120 bila shaka, kiwango cha zaka cha kutoa aidha kondoo wa mwaka mmoja au mbuzi wa miaka miwili.



- ✎ Kiwango cha zaka kwa kondoo, mbuzi, ng'ombe na ngamia Zaidi ya kiwango kilichotajwa hapo juu inaweza kujifunza kutoka katika vitabu vya sharia.
- ✎ Ili ikidhi kua kitu cha kulipia zaka wanyama wanatakiwa kua wamelishwa katika malisho yaliyowazi, kwa Zaidi ya nusu mwaka. Hakuna zaka kwa wanyama wenye kufanya kazi, mfano wale waliofunzwa kulima au kubeba mizigo.
- ✎ Zaka ya wanyama ni lazima ilipwe kwa kutumia wanyama. Hairuhusiwi kulipa fedha kama mbadala wa zaka.

* **Ng'ombe:** kwa ng'ombe inakadiriwa kufikia kati ya 30 hadi 39 bila shaka., kiwango cha zaka ni ndama wa miaka miwili.

* **Ngamia:** kwa ngamia inakadiriwa kufikia kati ya 5 hadi 9 bila shaka. Kiwango cha zaka aidha kondoo mmoja au mbuzi mmoja.





Kiwango cha Nisab na Kiasi cha Zaka kwa mazao.

⦿ Zaka kwa bidhaa za mazao inaitwa pia "ushur" au (Moja ya kumi).

❖ Nisab kwa mazao ni kama kilogram 610 ya uzito wa mazao makavu, pasipo na madanda ya juu au makapi baada ya kutoa mbegu.

❖ Zaka ya mazao ambayo yamenyeshewa bila ya jitihada kama mvua na mfano wake, ni asilimia kumi ya mazao.

❖ Zaka ya mazao ambayo yamenyeshewa kwa jitihada ni asilimia tano ya mazao.

↗ Hakuna zaka kwa nafaka au mboga isipokua aina ya kawaida ambayo watu hulima, hukausha na kuitunza katika maghala kama vile ngano, shayiri, mtama, mchele na mazao jamii ya kunde n.k

↗ Kwa bidhaa za mazao, hailazimiki kusuburi kwa mwaka mzima. Baada ya mazao kua yameshavunwa, zaka yake inatakiwa itolewe.

• • •

"Endapo mmoja hupanda, na ghalani kwake hakuna mbegu, lakini muda wa mavuno unapofika, huwaza kua ni mara ngapi anapata katika shamba lake kuliko mbegu anazozipanda.

Ni maghala kiasi anapata kwa matokeo yake baada ya kutumia ghala moja.

Endapo ataacha mbegu zake ndani ya ghala na kuzitunza badala ya kuzipanda wadudu na panya na majanga ya muda na uozo ukaliteketeza.

(Jalaladdin Rumi, Mathnawi, I, 2239-2240)

BUSTANI ILIYOHARIKBIKA

Palikua na mwanaume mkarimu mwenye mashamba na bustani za mitende. Mtu huyu alikua anatekeleza dini na alikua akitoa zaka kipindi cha mavuno. Baada ya kifo chake, watoto wake walirithishwa mashamba haya mazuri. Watoto wake walitekwa na tamaa za anasa za kidunia na wakawa wachoyo.

Kwa uhalisia, kutoa zaka kwa ukarimu na kwa muda aliokua anatoa baba yao na kupokea dua njema toka kwa masikini viliifanya mashamba yawe na baraka na neema. Masikini na mafukara walikua wanapata faida pia kuitia mashamba hayo. Ingawa, zaka ambayo baba yao alikua akiigawa ilionekana kubwa sana kwa watoato wale na hawakutaka kuigawa. Walifikiri kwamba kutoa zaka kutafanya mali zao zipungue. Hawakujua ni wapi rutuba katika mashamba yale ambayo Mwenyezi Mungu alikua amewaruzuku ilitoka. Hiyo ni kwa sababu ya uzembe na tamaa za kidunia zilipofua nyoyo zao.

Wakafuta sababu za kutotoa zaka.

Walisema, "Familia zetu zina watu wengi, lakini mali zetu si nyingi. Tusiwape chochote masikini. Twende asubuhi na mapema katika bustani yetu na tuvune kabla maskini hawajaja!"

Walipokua wanasema haya hawakufikiria kuhusu Mwenyezi Mungu. Mmiliki halisi wa mali zao na haki ya masikini katika mali zao...

Kwasababu hiyo, walipokua wamelala, maafa yalitokea kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Moto uliibuka toka bondeni mahali yalipokua mashamba na kuunguza shamba lote.


Asubuhi bila kujua nini kilichotokea, walitana kila mmoja kwa furaha:

— Twendeni, kama mnataka kuvuna matunda, ni lazima mfanye haraka!

Wakaanza safari. Wakiwa njiani walikua wanamong'onezaka kila mmoja:

— Kumbukeni! Hakuna ombaomba atakayetukaribia leo hii. Tusiwape nafazi ya kuja katika shamba letu.

Japokua walistaajabu walipofika shambani. Hawakuamini macho yao, walisema: "Tupo katika



eneo sahihi?" walitizama eneo lote. Lilikua ni shamba lao, lakini shamba halikua sawasawa. Kila kitu kilibadilika cheusi kama mkaa.

Mmoja kati yao aliona mbali zaidi na kugundua hali halisi haraka na kusema:

— Hapana, hapana! Hatukuja katika eneo ambalo si sahihi, hili ni shamba letu. Toka tumeumbwa katika dunia hii na kuamua kutowasaidia masikini, Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupa matatizo, ameunguza shamba hili kwa maafa haya.

Walibadilika rangi kutokana na huzuni na majonzi. Kile walichokipanga usiku na kile walichokumbana nacho asubuhi! Kutokana nahili walianza kulumbana na kushitakiana kila mmoja kwa kusema, "Ulitupa wewe lile wazo baya." Yule aliyeona mbali akawashauri wenzake:

Ndugu zangu! Hakuna
faida ya kushitakiana baina
yetu kama hivi. Tumucombe
Mwenyezi Mungu
atusamehe.

Kutoka hapo walielewa makosa yao. Mwenyezi Mungu ni mmiliki halisi wa tunavyovimiliki. Wangetumia mali alizowapa Mwenyezi Mungu kama Mwenyezi Mungu anavyotaka. Mali inayotumiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu inaongezeka na kutufanya tuipate pepo.

Mwishoni walitibu na kusema:

— "Aibu iwe juu yetu! Kwakweli tumefanya makosa makubwa sana. Ni kosa letu kabisa. Mola wetu kwa upande mwagine, hana mapungufu yoyote. Kwahiyo, tusikate tamaa isipokua tumkabili Mola wetu. Mola wetu mtukufu amechukua shamba letu kutokana na makosa yetu, lakini akituona kua tumeomba msamaha wa kweli kwa kile tulichokifanya, anaweza akatupa kitu kingine bora Zaidi kuliko hili. Tunaomba kwa Mola wetu Baraka na kumrejea yeche."

(kwa aya zinazoendana katika Quran tizama al-Kalam, 68: 17-33)



NI NANI ANAYESTAHILI KUPEWA ZAKA?

Watu ambao zaka inaweza kutolewa kwao ni:-

☞ **Masikini:**

Yule ambaye hana
kiasi cha kumtosha
mwenyewe au yule
ambaye anachokimiliki
hakikidhi hata nusu ya
matumizi yake kama
chakula na mavazi.

☞ **Mwenye uhitaji:**

Ni yule ambaye
anamiliki baadhi
ya mali ambayo
inatosha kukidhi
mahitaji yake Zaidi ya
nusu na sio mahitaji yote. Hawa wanaweza kuitwa wale wenye uhaba
wa fedha. Kwa maneno mengine wana fedha lakini hazitoshelezi.

☞ **Wale wenye madeni:** Hawa ni watu ambao hawawezi kulipa madeni yao kwa fedha
taslimu walizonazo mikononi. Inaruhusika kuwapa zaka kiasi cha
kuweza kulipa madeni yao. Ingawa wanatakiwa kuwa na madeni kwa
sababu za kisheria.

☞ **Wasafiri:**

Ni wasafiri ambao wana fedha katika miji yao lakini wametoka bora
fedha njiani na wanahitaji msaada wa watu wengine. Wanapewa
zaka inayotosheleza kuwafikisha katika miji yao. Ingawa, kwa watu hao
ni bora kwao kuazima pesa badala ya kuchukua zaka.

☞ **Wale wanaopigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu:** Hawa ni wale wanotaka kupigana
kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lakini wanashindwa kwa kukosa chakula,
silaha na vifaa vingine muhimu. Zaka inaweza kutolewa kwao kwaajili
kuhudumikia mahitaji yao. Kwa mantiki hii, zaka inaweza kutolewa kwa
wale wenye kueneza dini ya Mwenyezi Mungu na wale wanaotafuta
elimu na kusoma kwa njia hii.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na katika mali zao na vile wanavyovimiliki
(walikumbuka) haki ya (wenye uhitaji)
wale wanaomuomba, na wale ambao
(kwa namna moja au nyingine) walijizua
(Kuomba)."

az-Zariyat, 51: 19)

✿ Katika aya ya sitini(60) sura ya tisa(9) inayoitwa At-Tawbah, orodha ya wale ambao zaka inaweza kutolewa kwao inajumuisha makundi mengine matatu zaidi tofauti na hayo matano yaliyoorodheshwa hapo juu: watumwa, wale ambao mioyo yao hivi (karibuni) imerudia (kwenye ukweli), na wale ambao wameajiriwa kusimamia zaka(mfuko). Kwa hiyo, kwa mujibu wa aya hii, orodha ya wale ambao zaka inatakiwa kutolewa kwao inajumuisha makundi nane.

✿ Kama mtu anaweza kutoa zaka kwa moja kati ya makundi hayo, mmoja anaweza pia akagawa zaka kwa baadhi au kwa makundi yote.

✿ Tunapotoa zaka,kuanza na watu wa karibu zaidi inaleta thawabu kubwa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na shikeni Sala na toeni Zaka; na kheri mtakazo jitangulizia nafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yafanya."

al-Baqara, 2:110)

NI NANI ASIYESTAHILI KUPEWA ZAKA?

Zaka haitakiwi
kupewa kwa:-



- ✖ Mwenye mali,
- ✖ Asiyekua muislam,
- ✖ Wategemezi (Mama, Baba, Bibi, Babu, Watoto na wajukuu)
- ✖ Taasisi kama Shuleni, Hospitalini, Misikitini, wajengaji wa visima na madaraja n.k.

- Wanawake wanaweza wakatoa zaka kwa waume zao masikini na watoto. Kwa sababu yeye hausiki na maisha yao.
- Mmoja anaweza akatoa zaka kwa ndugu wengine kama baba wakubwa na wadogo na wajomba, mashangazi na wapwa.



KUTOA KATIKA VITU TUNAVYOVIPENDA

Abu Taliha alikua ni mmoja kati ya marafiki wependwa sana wa bwana Mtume na mmoja kati ya matajiri wasomi wa Madina. Alikua na viwanja vingi sana, mabustani, mashamba na ng'ombe. Alikua pia na bustani kubwa na ya thamani karibu na msikit wa Mtume (Masjid Nabawi) na ilikua ni bustani yake yenye thamani Zaidi katika bustani zake. Abu Taliha alikua akiipenda sana bustani yake hii ya mitende ambapo palikua na kisima cha maji matamu.

Alikua akiwaalika mara kwa mara Mtume na marafiki zake wengine katika bustani yake na kuwahudumia. Palikua panakua na majadiliano mazuri chini ya vivuli nya mitende. Siku moja Mtume alikua na majadiliano na maswahaba zake ndani ya msikit. Alisoma ayah ii wakati wa mazungumzo yao:

"Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnachokitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua." (Al-i Imran , 3: 92)

Abu Taliha alipoiskia aya hii aliyathirika nayo sana na alisema kwa Mtume wetu:

— Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! bustani iliyokaribu na msikit ni ya thamani sana kwangu na sehemu ninayoipenda zaidi

katika mali zangu. Kuanzia sasa na kuendelea, ninaitoa bustani hii kwa wenyewe uhitaji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Basi masikini waislamu wanufaika kutohana matunda na maji katika bustani hiyo.

Baadaye, Abu Taliha alienda katika bustani yake ya mitende na kutekeleza maamuzi yake. alipofika katika bustani yake alimuona mke wake Ummu Suleym amekaa katika kivuli cha mti wa mtende. Akamuomba aondoke katika bustani. Ummu Suleym akamuuliza:

— Abu Taliha! Kwanini tunaiacha bustani? Tunaenda sehemu? Abu Taliha akamjibu:

— Hapana, hatuendi sehemu yoyote. Bustani hii yetu tena; inamilikiwa na masikini wa Madina.

Kisha, akamwambia tukio lilitoteka msikitini. Juu ya hili Ummu Suleym akauliza:

— Je, umeitoa kwa niaba yetu sisi sote au kwa ajili yako pekee? Abu Taliha akajibu:

— Kwa niaba yetu sote. Kisha Ummu Suleym akasema:

— Mwenyezi Mungu awe radhi nawe Abu Taliha. Nilikua nafikiria sawasawa na wewe nilipokua nawaona masikini wanaotuzunguka, lakini nilikua ninaogopa kukwambia. Mwenyezi Mungu akubali sadaka yetu.



Khalifa Umar Ibn Abdulaziz alikua akinunua mifuko ya pipi na kuigawanya kwa masikini. Aliulizwa Umar;

- "Haitakua bora kuwapa pesa kuliko kugawa pipi?"

Umar Ibn Abdulaziz akajibu:

- "Ninapenda pipi kwahiyo ninawapa kile ninachokipenda Zaidi."



KIPI TUNATAKIWA KUZINGATIA TUNAPOTOA ZAKA?


Tunatakiwa tuwe na huruma tunapotoa zaka.

Pindi tunapokua tunatoa zaka na sadaka tunatakiwa kutoa kwa huruma na upole na kujifikiria wenyewe katika nafasi ya masikini kwa hisia kua tunaweza kua mmoja wao.



Tunapotoa zaka zetu, tunatakiwa tuisahau kua tunafanya tendo la ibada.

Pindi tunatoa zaka na sadaka, hatutakiwi kusahau kwamba tuna tekeleza moja katika amri ya Mwenyezi Mungu inamaanisha kuwa tunafanya jambo la ibada. Kwa sababu hii, tunatakiwa kuwa wenyewe kushukuru na kuona heshima kwa masikini ambao wanatufanya sisi tuweze kutekeleza tendo hili la ibada.



Tunatakiwa kua na adabu tunapotoa zaka

Tunatakiwa kutosahau kua tunatoa zaka na sadaka zetu ili kupata thawabu. Kama tunavyokua makini na kifurushi na kua wema tunapotoa zawadi au kurudisha uaminifu, tunatakiwa kufanya hivyo hivyo kwenye kutoa zaka na sadaka. Tunatakiwa kujionyesha kutokana na tabasamu na ishara nzuri kwa watu ambao tunawapa zaka.

Hatutakiwi kutegermea chochote Zaidi kutoka kwa kuliko matamano ya kumridhisha Mwenyezi Mungu. Tunapotoa zaka zetu, hatutakiwi kumkosea mtu anayepokea zaka ile kwa kusema; "Hii ni zaka yangu" kwa sababu kitu cha muhimu ni mchango ule uwafikie masikini. Sio muhimu kuwa anapokea mchango ule kufahamu kua ni zaka au sio.



"Ninapopokea zawadi,
ninapenda kupewa kwa uso
wa tabasamu na kifurushi
chenye kuvutia."



Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mliaoamini! Msharibu sadaka zenu kwa masimilizi na maudhi, kama anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho..."

(al-Baqara, 2; 264)

Ninapopokea zawadi, ninapenda kupewa kwa uso wenye tabasamu na katika kifurushi chenye kuvutia.

Kwa zaka zetu kukubalika, tunatakiwa kufanya utafiti wa kina kwa watu tunaowapatia zaka. Kilichokua muhimu ni kwamba sio kua vitu vimetuondokea mikononi mwetu, lakini pia vimewafikia walengwa. Kwasababu kilichokua muhimu katika zaka ni kumpa mtu anayestahiki. Ikiwa itapewa kwa mtu bila kufanyiwa utafiti wa kina, zaka inatakiwa itolewe tena.

Tunatakiwa kujaribu kuwatafuta wale watu hasa wenye kuona aibu kusema kua wanauhitaji. Hatutakiwi pia kusahau kua ni masikini kwelikweli, kwa hiyo zaka zetu zifike katika maeneo husika.

"Ni kwa namna gani
nitatambua masikini
wa kweli?"



Mtume wetu kipenzi amesema:

"Mtu masikini si yule anayezunguka kwa watu na kuwaomba mafunda au (milo miwili) au tende lakini masikini ni yule ambaye hana fedha za kutosha kukidhi mahitaji yake ya lazima na ambaye hali yake haijulikani kwa wengine, ambao wengine wanaweza kumpa kitu kama sadaka, na asiyeombaomba kwa watu."

(Bukhari, Zakat, 53)

KUTAFUTA MAISHA KWA KUFANYA KAZI ZA MIKONO NI BORA ZAIDI KULIKO KUOMBA



Mtume alikuwa hapendi watu wanaoomba na alikuwa akisema: "Hapana shaka, ni bora kwa mtu kuchukua Kamba na kwenda asubuhi milimani kukata kuni kisha kuziuza, na kula katika kipato na kutoa sadaka kutoka katika kipato hicho kuliko kuwaomba watu vitu."

(Bukhari, Zakat, 54)



Mtume wetu kipenzi amesema:

"Mkono unaotoa ni bora Zaidi kuliko mkono unaopokea."

(Bukhari, Zakat, 18)



Mtu alikuja kwa Mtume wetu na kumuomba sadaka. Mtume wetu akamuuliza:

— "Unachochote nyumbani?" yule bwana akasema:

— "Ndio, tunalo zulia, ninalala juu ya nusu yake na nusu nyagine ninajifunika mwenyewe. Baada ya hili ninacho kikombe ambacho ninakitumia kunywa vinywaji. Mtume wetu akasema:

— "Twende, nyanyuka na ukavilete." Yule bwana akanyanyuka na kuvileta vile vitu. Mtume wetu akavinyanya na kusema:

— "Je, yupo mmoja wenu anayeweza kuvinunua hivi?" yule bwana akasema:

— "Nitavinunua kwa dirham moja." Mtume wetu akasema mara mbili au mara tatu:

— "Hakuna yoyote atakayetoo Zaidi?"

Pindi mwengine aliposema; "Nitavinunua kwa dirham mbili." Mtume wetu akaviuza vile vitu kwa mtu yule kwa dirham mbili na akasema:

— "kwa dirham moja utanunua chakula kwa ajili ya watoto wako na kwa hii utanunua Kamba na kujipatia kipato chako kwa kukusanya na kuuza kuni."

Yule bwana alifanya kama ambavyo Mtume aliviyosema, na alikuja baada ya siku kumi na tano na kusema kua amepata dirham kumi, na amenunua kwa baadhi yake mavazi na chakula. Juu ya hili Mtume wetu akasema:

— "Ni bora kuishi kwa hivi(kuishi kwa kufanya kazi za mikono) au kumkabili Mwenyezi Mungu siku ya hukumu ukiwa na muhuri wa uombaomba?"

(Abu Dawud, Zakat, 26)

UKARIMU NA UTU WA BWANA MTUME (s.a.w)

Utu, kujali mahitaji ya watu na kuwatizama masikini, ni moja kati ya tabia za bwana wetu Mtume. Yoyote aliye pata tatizo alikua akikimbilia kwa Mtume wetu na kumwambia matatizo yake, matokeo yake, alikua akijaribu kuyatekeleza matamano ya kila mmoja na hakua akiwaacha watu waliomuomba kitu waondoke mikono mitupu. Alikua hajawahi kusema "hapana" au "sina kitu hicho."


Alikua akitoa hata kama kitu hicho si kikubwa. Pindi alipokua hana kitu cha kutoa alikua mwema kwa masikini na alikua akiwafariji.

Bwana wetu Mtume alikua mtu mwema Zaidi. hakuwahi kusahau kua mmiliki halisi wa mali na vitu ni Mwenyezi Mungu. Alikua akiwafikiria sana masikini na watu wenye uhitaji kuliko alivyokua

akijifikiria yeye mwenyewe na kuwalisha wenye njaa. Alikua akiwasaidia wale waliokua wanataka kukopa, na wakati mwengine alikua akitoa katika mali zake mwenyewe.

Moja ya hitajio la kua mkarimu ni kutoa zawadi kwa watu tunaowapenda na kuwafanya wafurahi. Bwana wetu Mtume wa Mwenyezi Mungu alikua akipendekeza zawadi na kusema: "Peaneni zawani baina yenu ili ikuze mapenzi kati yenu." Alikua akiwafurahisha marafiki zake kwa kuwapa zawadi mbalimbali. Alikua akipokea zawadi, na kujibu kwa nzuri Zaidi ya ile. Wakati mwengine alikua akirudisha bidhaa aliyo inunua kwa , muuzaji kama zawadi. Mara moja alinunua ngamia toka kwa Jabir Ibn Abdullah aliye kua katika mtikisiko wa uchumi na akamlipa pesa. Kisha akamrudisha kwake tena kama zawadi.

Mtume wetu kipenzi alikua akiwa alika waislam katika ukarimu na kujali mahitaji ya watu wenye uhitaji. Alikua akinadi kua matendo haya yanamfurahisha Mwenyezi Mungu kwa maneno yake haya mazuri: "Mtu anayejali mahitaji ya mmoja katika umma wangu ananifurahisha mimi. Na yoyote anayenifurahisha mimi anamfurahisha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi



Mungu kwa matokeo yake, humuweka mtu katika pepo yule ambaye amemfurahisha."

Alikua akiwapa watu habari njema kuwa watu wanaochangia wanapata furaha hapa duniani na huko akhera na watu wachoyo huwa hawana furaha. Kwa kuongezea ukarimu unamuweka mtu karibu na Mwenyezi Mungu, pepo na watu na alikua akiongezea:

"Mtu mkarimu hua karibu na Mwenyezi Mungu, na pepo na watu. Na mtu mchoyo huwa mbali na Mwenyezi Mungu, na pepo na watu na karibu na moto wa jahanam."

Hii ni jinsi ukarimu wa Mtume wetu kipenzi uliviyokua, ambaye moyo wake ulikua umejazwa mapenzi ya watu, huruma na utu, na ulikua hivyo siku zote za maisha yake.



"Mmoja anatakiwa (vyema) na tamaa ya watu wa aina mbili: moja, mtu anayetumia mali alizopewa na Mwenyezi Mungu katika njia ya haki, na mtu mwiningine anayetoa hukumu kwa elimu aliojaaliwa na Mwenyezi Mungu na kuifundisha kwa wengine"

(Bukhari, Ilim 15)



Siku moja, mmoja kati ya wasichana wa kiislam alitoa kama zawadi shati aliloliunganisha kwa mikono yake mwenyewe. Mtume wetu aliyeihitaji shati hiyo aliichukua na kwenda nyumbani. Baada ya kuivaa, alirudi msikitini. Mmoja wa maswahaba zake aliipenda sana na kushawishika na ukarimu wa bwana Mtume akasema:

— "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni shati zuri kiasi gani! Unaweza ukani pa mimi kama zawadi?"

Japokua hakua na sweta jingine, Mtume wetu kipenzi hakupinga hitajio la rafiki yake na akalivua na kumpatia haraka sana kama zawadi.

Rafiki wa yule swahaba aliyeomba shati kwa Mtume wetu akamuuliza:

"Kwanini umeomba shati hilo? Kwa kweli, Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) alilitaka sana shati lile. Hukujua kua hawesi kumkatalia mtu yoyote atakayemuomba kitu? Alijibu:

— "Sikulitaka shati lile kwa ajili ya kulivaa, nililitaka ili kulifanya sanda yangu."

Pindi swahaba huyu alipofariki alivalishwa shati lile alilopewa na Mtume kama sanda.

(Bukhari, Adab, 39; Janaiz, 29)



MBINGU NANE ZIKO TAYARI

Unahitaji pia huruma, ewe rafiki yangu
Usiwe mwiba katika uwaridi, kuwa umandel
Yoyote unayemuona kavunjika ubawa,
Kuwa zeri lake pasina kuumiza kidonda chake!

Kuna mikono ambayo haiwezi kukamata lesu kavu,
Kuna ndimi ambazo haziwezi kuyasema matatizo yake,
Kuna mafunzo mengi amba ni masikini na wasiojiweza,
Nenda kawe mkarimu utakayewafanya wafurahi!

Kuna ufahamu na mwenye moyo kwa mayatima,
Wasaidie wale walioachwa kilimani kuifikia tambarare,
Kwa uso uliochomeka katika jangwa lisilokua na kitu,
Kua upepo mwanana kwa uwepo wako!

Ulimwengu ni kwamba una mafukara wengi,
Baadhi yao hawana nguo, wala pesa,
Huyu hana miguu, yule pale hana mikono,
Hua na huruma ya moyo, kuna mkarimu mwana wa Adam.!

Yoyote anayekunywa sumu ya uchoyo,
Ah mto wa ufukara unamzamisha,
Nenda katika kila kona ya kijiji na mji,
Kua maji ya Zamzam kwa mwenye njaa, mwenye kiu.!

Unalazimika kuaendelea kufanya matendo mazuri rafiki yangu,
Hata kama baadhi yao hawatakuelewa,
Muumba anatosha kuwa msiri wako,
Mbingu nane zipo tayari, wewe tu kuwa mkarimu.!

Wote masikini na matajiri wako sawa mbele za Mwenyezi Mungu,
Si tamaa wala dharau, hii ni amri ya Mwenyezi Mungu,
Mwenyezi Mungu huwataka wale walio wema,
Wewe pia ni SEYRI, kua msiri wa pendo hili.

Muhammed Ali Eşmeli



MASWALI

Tujaribu uelewa wetu.

Oanisha sentensi zifuatazo.

- Wale wanaomiliki mali nyingi kiasi cha nisab
- Tunatoa robo ya dhahabu au fedha
- Mtu asiyeweza kutoa zaka
- Wakati unatoa zaka,
- Taasisi kama msikiti, shule, hospitali
- Zaka inahudumia kama daraja ambalo
- Mchango wa muislam anaotoa katika mali yake
- Mkono unaotoa
- Kiwango cha nisab kwa dhahabu
- Kiwango cha chini za zakat al-fitr ni
- Milo miwili kwa mtu mwenye kipato cha kati au kiwango cha fedha kinachohusiana.
- Wapokeaji waliyeamrishwa na dini yetu wanaitwa "Zaka."
- Ni mbora kuliko mkono unaopokea.
- Kwa maneno mengine 2.5% yake kama zaka.
- Ni gramu 80.18
- Wajukuu wake.
- na kwa wakandarasi wa barabara, visima, na madaraja zaka haiwezi kutolewa.
- Tusinghau kuwa tunafanya tendo la ibada.
- Inabeba njia ya matajiri kwa masikini.
- Wanahesabika matajiri kwa mujibu wa dini.

Tujipime maarifa yetu.

1. **Kwa yupi kati ya hawa zaka haitakiwi kutolewa kwake?**
 - a) Kwa msafiri
 - b) Kwa masikini
 - c) Kwa wale wenye madeni
 - d) Kwa wazazi
2. **Ni ipi tabia ya kawaida kwa matendo ya ibada kama zaka, sadaka, kuchinja na fitr?**
 - a) Utu na mshikamano
 - b) Haki na usawa
 - c) Kazi kwa bidi na furaha
 - d) Subira na wingi



3. Kipi kati ya vitu vifuatavyo hapo chini sio mionganini mwa mahitaji ya muhimu?
 - a) Nyumba
 - b) Gari
 - c) Bidhaa za biashara
 - d) Vifaa vya Sanaa na kazi
4. Ni kiwango gani cha nisab ya kondoo na mbuzi?
 - a) 40
 - b) 30
 - c) 20
 - d) 100
5. Ni sharti gani za kutoa zakat al-fitr?
 - a) Mubah
 - b) Faradh
 - c) Sunna
 - d) Mustahab
6. Ni sentensi gani hapa chini si sahihi?
 - a) Zaka inatakasa kutokana na mapenzi ya kupenda vitu vya kidunia yaliyopitiliza na uchoyo.
 - b) Zaka inasababisha mali kubarikiwa na kua nyingi na kuongezeka.
 - c) Zaka inaongeza mapenzi ya watu na ukaribu.
 - d) Zaka inafanya walio matajiri kuwa matajiri na walio masikini kua masikini.
7. Kutoka katika hivi vifuatavyo hapo chini haviwezi kutolewa kama zaka?
 - a) Fedha taslim
 - b) Kondoo
 - c) Vyombo vya nyumbani
 - d) Ng'ombe
8. Kipi ya vifuatavyo hakiwezi kusemwa kuhusu zaka?
 - a) Zaka ni lazima kwa matajiri
 - b) Zaka inatolewa mara moja kwa mwaka
 - c) Moja ya nne(robo) inatolewa kama zaka.
 - d) Wagonjwa hawatoi zaka.

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyowekwa kwenye mabano.

(katika mali, mbegu, haombiombi, takasa, moyo wako)

- ✿ "Mtu masikini wa kweli ni mtu ambaye hana vitu vya kumtosha mwenyewe, ambaye hapewi sadaka hata kama inajulikana kua ana uhitaji na ambaye.....kila mmoja."
- ✿ "...ya muislam tajiri ipo haki kwa masikini anayeomba na asiyeomba."
- ✿ "Kipimo cha wale wanaotoa sadaka katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama.....inayotoa mashuke saba ya nafaka ambapo kuna mbegu 700."
- ✿ "Ikiwa unataka.....kua laini, lisha masikini, papasa kichwa cha yatima."
- ✿ "Chukua zaka kutoka kwenye mali ya mwenye mali. Zaka.....mali zao na kuwatakasa kutokana na madhambi."



NINAJIFUNZA KUHUSU MTUME WANGU




SIRA



- ✿ *Vita ya Uhud (mwaka 625)*
- ✿ *Tukio la Raji na maafa ya kisima cha Maunab)*
- ✿ *Pombe na kamari: Shughuli za shetani*
- ✿ *Kijana aliyechunguzza uchaguzi wa Mtume wa mwisho*
- ✿ *Nguo inayokinga kutokana na aibu na madhabbi*
- ✿ *Vita ya Handaq(mwaka 627)*

- ✿ *Sulubu ya Hudaibbiya(mwaka 628)*
- ✿ *Kuwatuma wajumbe na barua za mialiko ya uislam(mwaka 629 -628)*
- ✿ *Ushindi wa khaibar (mwaka 628)*
- ✿ *Miaka ya mbeleni kuitembelea Kaaba (mwaka 629)*
- ✿ *Vita ya Mutah(mwaka 629)*




1- VITA YA UHUD (MWAKA 625)

a) Washirikina wakiugulia matamano ya kisasi.

Washirikina walipoteza watu 70 katika vita ya Badr. Miongoni mwao walikua watu mashuhuri katika kabilia la Maqraysh wakiwemo Abu Jahl, Uqbah, Utbal, Shaybah, na Umayyah. Ndio maana hawakusahau hasara walipata katika vita ya Badr na walikua wakiungulia kwa matamano ya kulipiza kisasi. Walikuwepo watu wengi walipoteza baba zao, kaka, watoto wao na wengine watu wao wa karibu sana katika viwanja vya Badr. Kwa hiyo washirikina wa kiquarashi wakafanya mukutano chini ya kiongozi wao Abu Sufyan na wakakubaliana kukusanya jeshi kubwa na kuivamia Madina. Kwa njia hii walikua wanakwenda kulipiza kisasi.

Baadhi ya washirikina ambao walikua wanaungulia moto wa kisasi, walishushwa na watu wa Makka kwa kusoma mashairi na uvumi katika kumbukumbu za wale waliouawa katika vita ya Badr. Kwa malipo ya fedha, waliweza kuwafundusha mamluki 2000 kutoka katika makabila ya wakazi wa Makka. Pamoja na watu wa Makka 1000, Abu Sufyan aliku anaenda na jumla ya maaskari 3000 chini ya amri: 700 kati yao walikua kivita na 200 kati yao walikua askari ya farasi. Jeshi lilikua na ngamia 300, walikua



na pombe ya kutosha pamoja na wanawake wakuwaimbia katika sherehe yao ya ushindi. Walikua na uhakika kua watakuwa washindi. Hata baadhi ya wake wa watu mashuhuri wa Makka waliungana na kampeni, mtu mashuhuri hasa Hindu mke wa Abu Sufyan.

b) Adui alipokua anakaribia

Maswahaba walituma wapelelezi na punde walikuwa na habari kua washirikina wameukaribia sana mji wa Madina. Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) walikua na kawaida ya kujadili mambo yaliyokua hayajafafanuliwa na wahyi na maswahaba zake. Kwa jambo hili alitumia pia njia hii. Alikusanyika na maswahaba zake, anawauliza:

— Tunaweza kukabiliana na adui nje ya Madina au tufanye njia ya kujilinda tukiwa na Madina? alikua na mapendekezo kua itakua bora wakifanya njia ya kujilinda ndani bila kuondoka Madina. Maswahaba waliokua viongozi kama Abu Bakr na Sa'd Ibn Muadh (Mwenyezi Mungu awe radhi nao) walikua na mapendekezo sawa na hayo. Lakini maswahaba wengi hasahasa vijana ambaa hawakuepo katika vita ya Badr walisisitiza:

— Tulikua tunasubiria sana siku hii ifike.... twendeni tukapambane na maadui zetu katika uwanja nje ya Madina! Mtume wetu (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikubaliana na pendekizo la wengi. Akavaa nguo mbili juu ya nyininge maalum kwa ajili ya vita pamoja na kofia, akatoka nje ya nyumba yake. Muda mfupi baadaye wale waliokua wakisitisiza kupigana nje ya Madina wakagundua dosari ya kopinga mapendekezo ya Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) wakabadilisha mawazo yao. Wakasema:

— Tulikua tumekosea, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hatuwezi kwenda kinyume na mapendekezo yako. Tafadhalii, fanya kama uliviyotaka!

Lakini Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akasema:

— Mtume hawezi kuvua mavazi yake ya vita akishavaa bila ya kupigana. Ikiwa mtakua wavumilivu na kufata majukumu yenu, ushindi na upendo wa Mwenyezi Mungu, utakua wetu.

Jeshi la washirikina walikua wamepiga kambi katika mlima Uhud, kama kilometra 5 kaskazini mwa Madina. Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alimuacha Abdullah Ibn Maqtum(radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) kusimamia Madina. baada ya kuswali swala ya Ijumaa, alitoka mji wa madina na wapiganaji 1000. Alitumia usiku katika maeneo karibu na Uhud. Siku iliyofuata katika mapambazuko, aliwasili Uhud na kuchagua eneo zuri kabisa kwa ajili vita.

c) Usaliti wa wanafiq.

Kitu ambacho hakikutarajiwa kiltokea nji-ani. Abdullah Ibn Ubayy alitafuta sababu ya kutokwenda akasema, "...Muhammad haku-tusikiliza watu wazima kama sisi ila alichagua mapendekezo ya vijana. Sikutaka uwanja huu wa vita wa kuanza nao." Kwa hiyo pamoja na watu wengine 300 wakatelekeza jeshi zima. Hawa walikua wanafiq ambaa alama zao hazikujulikana wakati huo. Walijionyesha kuwa waislam kwa nje, hali ya kuwa kwa uhalisia, ha-wakumuamini Mtume wala dini. Idadi ya wais-lam kulikabili jeshi la washirikina 3000 liliipungua kufikia 700. Hii ilimaanisha kua kila swahaba alikua anatakiwa kupambana na washirikina wanne.

**Unadhani waislam waliogopa kwasababu idadi ilikua ndogo
ukilinganisha na maadui? Na kwanini?**

Mtukufu Mtume(s.a.w) aliwapanga jeshi la waislam kuupa mgongo mlima Uhud. Katika kilima cha Ainayn kwa upande wake wa kushoto, aliwaweka wapiga mishale 50 chini ya uongozi Abdullah Ibn Jubayr (r.a) kisha akawashauri kwa msisitizo sana kua;

—bakini katika kilima hata kama tumeshinda au tumeshindwa na msiziache nafasi zenu hadi mtakaposikia amri yangu ya kufanya hivyo...maadui wanaweza kuwazunguka kwa kutumia njia ya mchepuo kupitia katika bonde lile na kutuzingira. Tumieni pinde na mishale yenu msiwaruhusu kuvuka katika bonde lile.

Ukubwa wa jeshi la maqraishi ulikua mara nne Zaidi kwa ukubwa kuliko lile la waislam. Ingwa, 700 kati yao walikua na silaha za kivita na 200 walikua askari wa farasi. Waislam kwa upande mwingine walikua na watu 100 na silaha za kivita na watu 2 tu askari wa farasi. Mtukufu Mtume(s.a.w) alitoa amri upande wa kulia kwa Uqqasha na upande wa kushoto kwa Abu Muslama(r.a).

Vita ilianza kwa pande mbili kutoa mtu kwenye mashindano kama ilivyokua desturi ya siku hizo. Katika mashindano hayo, jumla ya washirikina 9 waliuwawa, mmoja baada ya mwingine, na waislam walioshindana nao.

Kwa hamasa dhidi ya hatua za swahaba shupavu kama Hamza, Ali, Sa'd Ibn Abi Waqqas na Abu Junadah(r.a) washirikina walipoteza watu wengine 20 mwanzoni kabisa mwa vita. Watu wa Makka wakawa wameshindwa ghafla. Pande zao zote mbili ya kulia na kushoto wakaanza kurejea nyuma, hata wanawake waliokua wakipiga ngoma na kuwashawishi washirikina kupambana wakaanza kukimbilia uelekeo wa mlimani huku kukiwa na vilio na kelele. Walikutana na sura ya nguvu ya Imani na ushujaa wa waumini, idadi kubwa ya wanaume na vifaa washirikina

vilithibitika katika mpambano kua havina matumizi. Walikua wakikimbia haraka iwezekanavyo.

d) Wapiga upinde walivunja amri ya Mtume.

Hivyo waislam walikua washindi wa wazi katika hatua ya kwanza ya vita. Lakini walitakiwa kuwafuata maadui waliokimbia hadi mbali kabisa. Badala yake, waislam walichagua kutawanyika katika uwanja wa vita na kuanza kukusanya vitu vilivyoachwa na washirikina walivyoivacha nyuma. Muda mfupi baadaye, baadhi ya wapiga upinde walikua wanaangalia eneo la tukio kutoka katika kilima cha Ainayn wakaanza kusema,

— Tunasubiri nini hapa? Hali ya kua vita imeisha na ushindi ni wetu, twende nasisi tukakusanye vitu!"

Kamanda Abdullah Ibn Jubayr(r.a) alijaribu kuwakataza na kuwaambia;

— "Mmesahau amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu? Hatuwezi kuacha nafasi yetu hadi pale atakapoturuhusu kufanya hivyo!"

Hawakumsilikiza. Walibaki wapiga upinde 8 tu waliobaki naye wakati wenginne wote walikua wakiteremka chini ya mlima kwenda kukusanya vitu.



**Je, unafanya nini ingekua wewe ni mpiga upinde katika kilima
cha Ainayn siku hiyo?**




Khalid Ibn Walid, mmoja wa makamanda wa jeshi la watu wa Makka, alilazimisha njia yake kuititia katika bonde liliokua linalindwaa na wapiga upinde wa kiislam na kwenda kuwazingira jeshi la waislam kuwakamata walinzi, lakini walishindwa kwa kua wapiga upinde walikua wamelidhibiti bonde vilivyo. Lakini baada ya kuona wapiga upinde wengi wamekiacha kilima, Khalid Ibn Walid alizindua shambulio jingine akiwa na wafuasi wake. Haraka sana wakamuua Abdullah Ibn Jubayr na wapiga mishale wengine nane pamoja naye(radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao). Kisha akawavamia waislam waliobaki kwa upande wa nyuma waliokuwa wameshughulishwa na kukusanya vitu vilivyoachwa na washirikina. Washirikina wengine waliokua wanakimbia, wakaona vita imeanza upya na wakazindua shambulio jingine kwa upande wa mbele. Maswahaba walikua wamewekwa chini ya mpambano mkali. Ushindi wa waislam ulibadilika na kushindwa ndani ya muda mfupi. Kwa sababu waislam walipatwa na tatariki walitawanyika katika uwanja wa vita na wakatengana baina yao, wakaanza kuhofia maisha yao.

e) Kuuwawa kwa mjomba wake Mtume Hamza(r.a)

Hindu mke wa Abu Sufyan, aliyempoteza baba yake Utbah, kaka yake Walid na mjomba

wake Shaibah katika vita ya Badr, alitaka mno kulipiza kisasi kutoka kwa Hamza(r.a) aliyemuua baba yake katika mpambano. Likini alikua ana-jua kua hakuna anayeweza kumshinda shujaa mkubwa Hamza uso kwa uso. Kwa hiyo alimu-hidi Wahshi, mlenga shabaha mashuhuri, uhuru wake na zawadi zenyeh gherama, endapo atafanikisha kumuua Hamza. Wakati wa vita ya Uhud, Wahshi hakupata uwezo wa kumk-abili Hamza uso kwa uso. Alijificha nyuma ya jabali kubwa na kusubiria Hamza apite mbele yake. wakati huo huo, Hamza alikua akikimbia huku na huku katika uwanja wa vita, akiwa na upanga wake akikata shingo za washirikina waliokuwa wankatisha mbele yake. muda huu, alikuja na kusimama mbele kabisa ya Wahshi, akiwa amempa mgongo. Wahshi hakutaka kupoteza muda. Alirusha mkuki kidogo kutoka upande wa juu wa jabali alilokua amejificha nyuma yake. mkuki ulimchoma kuititia katika kinena cha Hamza. Na muda mfupi baadaye Hamza (r.a) alikua amaelala katika uwanja wa vita amekufa (Shahidi)

Kuuwawa kwa Hamza katika kipindi vita imepamba moto ilikua ni upotetu mkubwa kwa waumini. Maswahaba wakawa wanau-liwa mmoja baada ya mwingine. Namba ya waumini mashujaa waliokuwa wamemzunguka Mtume(S.a.w) pia waliuwawa.



f) Je, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuwa-wa?

Mshirikina mmoja alimuua Musab Ibn Umayr(r.a) mbeba bendera wa jeshi la waislam, akidhani amemuua Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake). Akaanza kupiga kelele:

— Nimemuua Muhammad.....nimemuua Muhammad.

Mwangwi (Sauti ikijirudia) eneo lote la uwanja wa vita, maneno haya yalitia hofu kwa madaraja ya waislam. Muda mfupi baadaye, Mtukufu Mtume (S.a.w) alianza kuita kutoka kule alipokuwepo:

— Enyi watumishi wa Mwenyezi Mungu! Nipo hapa! Njooni na mkusanyike kwangu!

Lakini hakuna aliyemsikia. Waislam walijikuta wakigawanyika makundi matatu. Kila kundi ,ilikua halitambui juu ya kundi jingine.

Washirikina walijaribu kuitumia hali ile ya mkanganyiko wa waislam. Walikua ndani ya urefu wa mikono ya Mtukufu Mtume (S.a.w). Jiwe lilirushwa na wao iliasikamana na midomo yake na likavunja jino lake. Alipigwa na upanga wa Ibn Kamiah. Duara mbili kutoka katika kofia yake zilivunjika na kumchoma shavi la Mtume na akapata jeraha katika uso wake.

Nini ungefanya endapo ungekuwepo pembezoni mwa Mtume (S.a.w) wakati huo?

Baada ya muda, maswahaba mwishoni wakamtambua Mtukufu Mtume(S.a.w) katika uwanja wa vita. Haraka sana wakajikusanya kumzunguka. Wakaanza kupambana tena na washirikina.

Haraka sana, washirikina wakaanza kutoweka katika viwanja vya Uhud, wakifkiria kuwa nafasi ya udhibiti waliyoipata ilikua imetosha. Lakini kabla ya muda mrefu, walijutia uamuzi wao na kufikiria kuhusu kushambulia mji wa Madina; kwa sababu hata kama wame tokea washindi hawakua na ushahidi juu ya hilo, hawakua na ngawira wala wafungwa wa vita. Kufanya hali kuwa si shwari waislam hawakua wameondoka katika uwanja wa vita.

Waislam walikusanyika tena. Walikua wakivifunga vidonda vyao na waliokua wamekuwa mashahidi walikua wanawsaliwa swalat jeneza na kuzikwa. Mashahidi tisa kwa wakati huo waliletwa pembezoni mwa mwili wa Hamza(r.a) na kuzikwa baada ya kuswaliwa swalat jeneza, hali ya kuwa mwili wa Hamza(r.a) ulibaki kwa wengine tisa kuletwta tena. Kwa namna hiyo, Mtukufu Mtume(S.a.w) aliongoza swala nyangi za jeneza kwa mjomba wake

kipenzi ambaye pia alijulikana kama "Bwana wa mashahidi".

Tunapokumbuka mashahidi wa Uhud baadaye, Mtukufu Mtume(S.a.w) alisema kwa kuelezea fadhila zao

— Naapa kwa Mwenyezi Mungu, nilitamani kua shahidi na kutumia usiku wangu chini ya mlima Uhud pamoja na maswahaba zangu.

Baada ya kurudi Madina, Mtukufu Mtume (S.a.w) aliwakusanya maswahaba zake na kuwafuata washirikina. Katika sehemu inayoitwa Khamra al-Asad, walijenga mahema 500.

Washirikina kujua kwamba wanafuatwa, wakaanza kupata hofu.

— Waislam walikua hawawezi hata kunyanya vidole vyao, inawezekana vipi haya kutokea kwa ghafla kiasi hiki? Wakaanza kushutumiana kati yao. Halikua muda mrefu toka wameanza kuambizana:

— Twendeni.....tutokeni hapa kabla kitu kibaya hakijatokea!


Na haraka wakarudi Makka.

2- TUKIO LA RAJI NA MAAFA YA KISIMA CHA MAUNAH (MWAKA 625)

a) Waislamu waliojitoa kufundisha Uislam

Washirikina walipata ujasiri Zaidi baada ya vita ya Uhud. Waislam hawa kua salama Madina. Kwa upande mwingine, Mtukufu Mtume (S.a.w) alikua anafanya tahadhari ya ulinzi dhidi ya uvamizi wa watu wa Makka, hali ya kua na upande mwingine alikua akitumia ipasavyo kila nafasi aliyokua akiipata kuutangaza uislam. Alikua akiwatuma walimu katika makabila ya jirani yaliyokua yameukubali uislam, ili wajifunze kuhusu uislmu na Quran.

Mjumbe kutoka katika kabilia la Adal na Qara alikuja kwa Mtukufu Mtume(S.a.w). Walimuomba walimu waislam watumwe kwenye kabilia lao ili wakawafundishe uislam na Quran. Mtukufu Mtume (S.a.w) akawatumia kundi la maswahaba kumi chini ya uongozi wa Asim Ibn Thabit(r.a). Wakiwa njiani walimu wakavamiwa na kundi la wahuni wapatao wanaume 100 kutoka katika kabilia la Huzail, karibu na eneo linaloitwa maji ya Raji baina ya Usfan na Makka. Walimu nane kati yao





walipambana na wavamizi hadi mwisho kabisa na wakauwawa. Wakabaki wawili ambaao ni Zaid Ibn Dasina na Hubaib Ibn Adiyy, walichukuliwa kama wafungwa wa vita na watu wa Huzail na kuwauza kwa watu wa Makka. Zaid alinunuliwa na Safwan Ibn Umayya, aliyetaka kulipiza kisasi

toka kwake kwa kumuua baba yake katika vita ya Badr. Hubaib pia alitiwa gerezani na kisha kunyongwa. Watu wote mashuhuri wa mji wa Makka walikuwepo kuangalia utekelezaji wa adhabu huyo ya kunyongwa kwa wote wawili.

Unafikiri Hubaib alijibu nini kwa swali hilo?

Muda kabla ya kunyongwa, Abu Sufyan alikuja kwa Hubaib (r.a) na kumuuliza:

— Basi, hebu niambie.....Ungependa Mtume kua katika nafasi yako mbadala wa maisha yako?

Hubaib (r.a) akasema bila hofu yoyote:

— Haiwezekani.....! Sitaweza hata kustahmili mawazo yay eye kuchomwa japo na mwiba katika mguu wake Madina, basi pekee atumaini yeeye kuwa katika nafasi yangu wakati huu!

— Alishangazwa na majibu, Abu Sufyan hakuweza kusaidia ila alikiri,

— Naapa, sijawahi kuona mtu mwingine anayependwa na marafiki zake kuliko Muhammad!

Majibu ya Zaid (r.a), aliyeahidiwa uhuru endapo angeukana Uislam, yalikua yanafanana:

— Kufa nikiwa muislam ni bora mara elfu moja kuliko kuishi kama msaliti..! hakupepesa hata jicho tayari wakawa wamemnyonga.

Mtukufu Mtume (S.a.w) alikua amefadhaika sana na kile kilichowatoka maswahaba zake, waliouwawa kwa mapenzi ya kufundisha Uislam. Akasema:

— Mwenyezi Mungu ashughulike na wajeuri hao kama anavyotaka na akamuachia Mwenyezi Mungu kisasi hicho kukitekeleza.

b) Usaliti mmoja baada ya mwingine

Katika kipindi cha siku hizo hizo, abu Bara, mtu mashuhuru katika mji wa Najd, alikuja Madina na kumuomba Mtukufu Mtume (S.a.w) kuwatuma baadhi ya maswahaba kuwfundisha Uislam. Maumivu ya tukio la Raji

lilikua bado halijapoa. Mtukufu Mtume (S.a.w) akamwambia Abu Bara,

— Siwaamini watu wa Najd. Ninahofia kitu kitawatoka walimu wangu endapo nitawatuma huko.

Abu Bara akaahidi kuwalinda walimu. Kisha Mtukufu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake) akawatuma maswahaba sabini pamoja na Abu Bara. Lakini mjambe alipofika katika kisima cha Maunah, walilalitiwa vibaya mno. Kundi kubwa la watu wadanganyifu wa Najd waliwaua wajumbe wote wa maswahaba. Umayya Ibn Amr (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) ndiye mmoja pekee aliyesurika na mauaji.

Mtukufu Mtume (S.a.w) alikua nahuzuni ya hali ya juu kutokana na mfululizo wa majanga. Mtukufu Mtume (S.a.w) aliwapenda sana maswahaba wale waliouwawa. Wote walikua wamefundishwa na Mtume mwenyewe. Waumini wa Madina walitokwa na machozi ya huzuni. Wanafiki na mayahudi kwa upande mwingine hawakuweza kuficha furaha yao.

Mtukufu Mtume (S.a.w) alikuwa amefadhaika mno kuliko kipindi kingine chochote. Baada ya swala ya asubuhi kila siku kwa mwezi uliofuata, aliomba dua akisema:

— "Ewe Mola wangu! Walaani kabilia hili ambao wameasi dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake!

3- POMBE NA KAMARI: MATENDO YA SHETANI

Kisha aya ifuatayo ya Quran ikateremshwa “**Enyi mliaoamini!msiikaribie swala hali ya kua mmelewa mpaka mtakapoolewa kitu gani mnachokisema...**” (an-Nisa, 4:43). Baada ya hapo, namba ya waislam waliokua wanalewa ikapungua. Kabla ya swala, swahaba alikua akinadi: “**Wale waliolewa wakae mbali na swala!**” Hatimaye, waislam wengi wakaacha kunywa pombe. Wengi hawakua huru kutoekana na matukio yasiyokua ya lazima yanayotokana

sababu ya kunywa pombe. Umar(radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) alikua akiomba dua:

— Mola wangu..... tutumie amri iliyokua bayana kuhusiana na ulevi!

Mwishoni, ugomvi uliotokea baada ya sherehe za unywaji wa pombe ulileta hatari ya ulevi wa pombe bayana kwa kila mmoja. Hitajio la kupiga marufuku unywaji wa pombe likawa wazi.

**Unafikiri nini sababu ya kwanini unywaji wa pombe haukupigwa
marufuku kwa mara moja?**

Na ilikuja kuzuiliwa na aya ifuatayo:

“**Enyi mliaoamini!bila shaka ulevi na Kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi za shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpare kufanikiwa. Hakika shet'ani anatraka kutia kat i yenu uadui na chuki kwa ulevi na Kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mtaacha?**” (al-Maida, 90-91)

Mtukufu Mtume (S.a.w) alitumwa kwa Umar(r.a) na kumsomea wahyi huu. Aliofika kipande kilichosema “**Basi je, mtaacha...?**” Umar (r.a.) akatangaza:

— Ewe Mwenyezi Mungu! Ndio, tutaacha; tutaacha! Maneno halisi yaliwaingia hasa maswahaba wote.

Baada ya ufunuo huu pamoja na amri ya Mtukufu Mtume (S.a.w), swahaba akanadi habari hii katika mitaa yote ya Makka kwamba:

— Kutoka sasa ulevi umekatazwa!

Katika mitaa ya Madina palitengenezeka mifereji ya pombe iliyomwagua kutoka mitungi

na vibuyu nya ngozi ambavyo mwanzo zilikua zimetunzia na sasa kinywaji kimekatazwa.

Waislam ambao mwanzoni walikua wanakunywa pombe, kwa hiyari na heshima wakajikabidhi katika amri hii na kuharibu akiba ya pombe waliokua nayo bila kipinga kitu chochote na hawakunywa tena.

Mtukufu Mtume (S.a.w) baadaye alisema:

— Hakika Mwenyezi Mungu amerlaani mnywaji wa pombe, mtengenezaji, mbebaji, mnunuaji na yule anayeishi kwa kutumia faida inayopatikana kwayo. (Ahmed, I, 53; II, 351; Nasai, Ashriba, 1-2; Hakim, II, 305)

Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) pia alisema maneno yafuatayo:

“Kila ulevi umekatazwa. Kidogo katika kitu kinacholewesha kikitumika sana pia kimekatazwa.” (Ibn Majah, Ashriba, 10; Nasai, Ashribah, 24, 48)

“Pombe ni mama wa madhambi yote.” (Ahmad, V, 238)

ALIDHALILISHWA!

Ali (r.a.) anasimulia:

"Katika watu wote wa familia yao, aliye kua mpendwa Zaidi kwa baba yake alikua Fatimah. Mikono yake ilipata makovu kutokana na kusaga na shingo yake kutokana na kubeba mkoba wa ngozi wa maji. Kufagia kuzunguka nyumba kulimuacha na mavumbi. Baadhi ya watumwa waliletwa mara moja kwa Mtukufu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake) .

— Unatakiwa kuomba mtumwa kutoka kwa baba yako, nilimshauri.

Hivyo Fatimah alikwenda nyumbani, aliona baba yake ana ongea na watu wengine, akarudi. Siku iliyofuata, Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) akaenda kumtembelea. Akamuuliza:-

— Ni kitu hicho ulichokua unakihitaji? Fatimah alikaa kimya na hakujibu.

— Naomba mimi nielezee, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu...nilivunja ukimya na kuanza kuelezea juu ya jambo lenyewe.

— Muogope Mwenyezi Mungu Fatimah na tekeleza yale aliyokuamrisha. Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) kisha akasema:

— Shughulikia familia yako na kabla hujaeda kulala sema , **Subhanallah mara 33, Alhamdulillah mara 33 na Allah-u Akbar mara 33;** vyote hivi unaweza kuongeza idadi yake na kufikia mia moja (100). Hizo ni bora kwako kuliko mtumishi.

— Niko radhi na Mwenyezi Mungu na Mtumewa Mwenyezi Mungu, alisema Fatimah. Kwa hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) hakumpa mtumishi." (Abu Dawud, Kharaj, 19-20/2988)




4- KIJANA ALIYEFANYA UTAFITI KUHUSU UCHAGUZI WA MTUME WA MWISHO

Salman Farisi (r.a.), aliye kua mtumwa wa myahudi mmoja wa Madina, anasimulia kwa Ibn Abbas (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) aliyechochea safari ambayo ilikua katika kilele cha kuingia kwake katika sehemu salama ya Uislam:

a) Tulikuwa tukiabudu moto

- Nilikua nikiishi Jayy, kijiji katika mji wa Isfahan. Baba yangu alikua mtu tajiri katika kijiji chetu. Nilikua ni mtoto wake wa pekee. Nilikua ni ktu alichokipenda sana katika maisha yake. alinipenda mimi mno. Hakuniacha niwe mbali ya upeo wa macho yake. hakua hata akiniruhusu kuondoka nyumbani akihofia kua kitu kibaya kinaweza kunikuta.

B a b a
yangu aliamini
k a t i k a
Uzoroasta.
K w a



maneno mengine alikua akiabudu moto. Alinifundisha na mimi Imani yake. kwa nafasi kubwa nilishika Imani ya baba yangu ambayo nilijipa mwenyewe majukumu ya kuuwashaa na kuchochea moto mtakatifu katika hekalu la ibada. Sikuruhusu moto kusinzia hata muda kidogo.

Baba yangu pia alikua na shamba. Siku moja, alipokua kashughulishwa na ujenzi aliniambia.,

— Mwanangu kazi hii inanichukua siku nzima ya leo, kwa hiyo sitaweza kwenda shambani....ni vema ukaenda wewe leo.

Kisha akanielekeza vitu vinavyotakiwa kwenda navyo shambani, akaongezea,

— Mwanangu nitakapokufa, utakua mmilikia wa ardhi hii. Kwahiyo toka nenda kaone ardhi yako, lakini usikae sana huko kuliko kawaida ukani pa mashaka juu yako, kisha nikashindwa hata kuwa makini na kumalizia kitu ninachokifanya!

b) Nilishangazwa

Hivyo nikatoka kuelekea shambani. Nikiwa njiani, nikaona kanisa la wakristo. Nikalisogelea karibu na kusikia sauti za wakristo zikitokea ndani. Walisikika kama wanasali. Lakini pia sikua na uhakika walikua wanafanya nini hasa, kwa kua baba yangu hakuniruhusu kutoka nyumbani karibia maisha yangu yote. Kwa hiyo sikua na hakika ni nini hasa watu walikua wanafanya ndani ya kanisa. Nikiwa nataka kudadisi, nililingia

kanisani ili kujionea mwenyewe. Niliwatazama kwa muda. Na mwishoni, nikafikiria:

— Hakika dini yao inaonekana tofauti na ya kwetu.

Sikuondoka kanisani hadi juu lilipokuu linazama. Lakini kwa upande wa shambani sikuenda tena. Nilitaka kufahamu Zaidi, nikawauliza:

— Wapi nitapata namna halisi kabisa ya dini yenu? Wakajibu

— Huko Damascus. Nikaendelea:

— Nikienda huko je watanipokea katika dini hii? Wakajibu:

— Ndio. Nikaauliza tena:

— Je, kuna mmoja mionganii mwenu anaweza kwenda huko hivi karibuni? Wakasema:

— Upo msafara unatarajia kwenda Damascus siku chache zijazo.

Jua lilikua limeshazama kabisa muda mimi ninaenda nyumbani kwa baba yangu, ambaye nilielewa mapema kua aliacha kazi

zake zote na kawatuma watu watoke kunitafuta. Aliponiona tu, akaniuliza,

— Ulikua wapi? Je sikikukwambia nini cha kufanya?

— “Baba, nilikwenda leo kutizama ardhi yetu, lakini nilikuta kanisa na kuingia ndani. Nilikuta watu Fulani wanaabudu ndani yake.” nilianza kuelezea, “nilichukuliwa sana na kitu walichokua wanakifanya..... kiasi kwamba nilikuja kugutuka juu linazama muda ninaachana nao!”

— “Hakuna chochote utafaidika nacho katika dini yao,” alinikemea. Ulichonacho wewe, kilichotoka kwa mababu zako, ndio njia bora!”

Alihofia ninaweza nikawakimbia, baba yangu alinitia pingu kuzunguka miguu yangu na akanifungia ndani ya nyumba. Lakini yote nilikua ninawaza kuhusu msafara ambaao utaondoka kuelekea Damascus ndani ya siku chache zijazo.

Unafikiri Salman atakwenda Damascus? Kwanini?

c) Njiani kuelekea Damascus

Hata hivyo, kupitia rafiki niliweza kutuma ujumbe kwa mabwana wa kanisani, niliwasisitiza “Kunipa habari mapema sana endapo msafara utakua tayari kwa ajili ya safari ya Damascus.” Muda mfupi baadaye nilipata habari kua msafara wa wakristo kuelekea Damascus ulikua tayari. Angalau nilikuwa huru kutokana na pingu za chuma na kukimbia kanisani, ambapo nilijungu na msafara kuelekea Damascus. Baada ya muda Fulani tulifika Damascus.

Huko nilitafuta msomi zaidi katika mji ule. Wakazi wa pale walinielekeza kwa askofu mmoja wa kanisa. Nilienda upesi nilipopata habari. Wakati huo askofu alikua nje ya kanisa.

— Ninataka kuingia katika dini hii, nilimsihi askofu.

— Ninatamani nibaki na wewe, nitoe huduma kanisani, njifunze ukristo kutoka kwako na niabudu pembezoni mwako.

— Njoo ndani! Alisema.

Niliingia kanisani pamoja naye. Siku zangu pale zilianza. Ndani muda, nilijikuta nikiona kua askofu wa Damascus hakua mtu mzuri kama wengi walivyodhani. Aliwaamrisha watu wanaokuja kanisani kuwapa sadaka masikini, lakini aliihifadhi. Niligundua pia, siku moja, alikusanya jumla ya mitungi saba ya dhahabu na fedha katika sadaka. Hasira yangu ilikua siku hiyo. Lakini muda mfupi, alijeruhiwa na kufariki. Wafuasi wa kanisa walikusanyika ili kumtolea huduma ya mwisho. Hapo ndipo nilipokuja kua wazi kua maaskofu wote wanakosea kidogo.

— Alikua mtu mbaya, nilimwambia mtazamaji.

— Kweli, alikua anawashawishi nyinyi kutoa sadaka, lakini mar azote alikua anahifadhi vitu mlivokua mnatoa kwa matumizi yake binafsi na hakua akitoa hata kidogo kwa masikini!

— Umeyajuaje yote hayo? Waliniuliza kwa tuhuma.

— Ninaweza kuwaonyesha mahali alipoficha hazina yake, niliwajibu.

Kishawakachukua mitungi sabaya dhahabu na fedha kutoka katika eneo nililioanya.

— Hatutamzika, tunaapa! Waligomba huku wakilaumu. Walikua wakweli katika ahadi yao; badala yake wallitupa maiti yake katika shimo na kufunika kwa mawe. Katika eneo lake, walimleta msomi mwингine. Alikua tofauti, toka siku hiyo, tofauti na wale waliokua wakiswali swala tano, sikumbuki kama nimewahi kumuona mtu mwингine aliyekua anajishughulisha na dunia walau kidogo, aliyekua na hamu na akhera na aliyekua anafanya ibada mchana na usiku. Muda mwингine baadaye, yeze pia alikua katika kitanda chake cha kifo, anapumua pumzi yake ya mwisho, nilimwambia,

— Nimekua na wewe kwa muda wote huu na sijawahi kumpenda sana mtu yoyote mwингine kama nilivyokupenda wewe. Sasa unaona muda wako umewadia. Ni kitu gani unanishauri nikifanye baada yako? Nitaenda kwa nani?

— Simfahamu yoyote ambaye anaifuata njia kama ninayoifuata mimi, mpPENDWA WANGU, ALINONG'ONA.

— Wema wanao wote lakini wamekuwa. Wale walioko hai wameharibu ukweli wa milele wa dini na wamezuia mambo mengi sana. Lakini fikiria, yupo bwana huko Masul, anaifuata njia kama yangu. Ni vema ukaenda kwake.

Baada ya huyu mzee mwenye heshima kufariki, nilikwenda Mosul na kukutana na rafiki yake. Yeye pia alifariki dunia, baada ya kumuuliza, nilikwenda Nusaybin na baadaye Ummariya(karibu na Eskishehir ilipo Uturuki leo) Kule nilijipatia mali kiasi pia kwa kua na ng'ombe na kondoo. Hatimaye, kifo kilifika katika mlango wa yule bwana wa Ummariya pia. Nilipomtaka ushauri alisema:

— Kiukweli kabisa, mpPENDWA WANGU, SIFIKIRI kama yupo anayefuata njia kama hii ninayeweza kukushauri umfuate baada yangu....hakuna aliyeo katika njia kama yetu. Lakini nyakati za Mtume wa mwisho ziko karibu; ninakihisi kivuli chake kimetulia juu yetu. Mtume huyo atatumwa katika dini ya Ibrahim (r.a). atatokea katika ardhi ya waarab na atahamia katika nchi yenyemashamba ya mitende, sehemu yenyemajabali. Atakubali zawadi lakini hatagusa sadaka. Atakua na muhuri wa utume katikati ya mabega yake. ikiwa utapata uwezekano sasa hivi nenda katika ardhi hiyo na usisubirie hadi wakati huo!

d) Katika uchaguzi wa Mtume wa mwisho

Hatimaye, naye alifariki dunia. Kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu nilikaa pale kwa muda mrefu kidogo. Kisha nikakutana na baadhi ya wafanyabiashara kutoka katika ukoo wa Kalb. Nilitoa ng'ombe na kondoo wangu kwa sharti kuwa nitakwenda nao Uarabuni. Walinikubalia na wakaondoka na mimi. Baada ya kufika katika bonde la Qura, walinigeuka na kuniiza kama mtumwa kwa myahudi. Nilibaki kwa myahudi kwa muda. Bonde la Qura liliku na miti mingi ya mitende, sikusaidia ila nilikua nimestaajabu endapo nimewadnia, baada ya yote yale, katika mji amba bwana wangu alinielezea kama sehemu ambayo Mtume wa nyakati za mwisho atahamia. Hata hivyo, ado nilikua nmejenga matumaini makuu, moyo wangu hauku umeshawishika kikamilifu.

Mara moja katika kuishi kwangu bonde la Qura, binamu wa myahudi, aliyetokea katika kabilia la Quraya, alininunua na kuja na mimi Madina. naapa kwa Mwenyezi Mungu mara baada ya kuwasili Madina nilijua, kua ni pale na kisha, huu ndio mji amba bwana wangu alinielezea nilipokua Ummariya. Moyo wangu sasa ukapata utulivu, nikaanza kumsubiri sasa Mtume wa nyakati za mwisho. Kidogo nilichokua ninafahamu ni kua Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) ameshakuja na amebaki kwa muda katika mji wa Makka. Mahusiano ya majukumu kuwa amekuja kuwa mtumwa, japokua, sikuwahi kusikia chochote kinachohusiana. Nikaanza kuvumilia na kuwa na matumaini nikisubiria muda wa kukutana naye.

e) Habari za Mtume wa mwisho

Siku moja, nikiwa juu ya mtende, nikifanya kazi na bwana wangu alikua amekaa chini ya kivuli cha mti akiwa na mtu mwininge. Kisha

binamu yake akaja, akipiga kelele kwa sauti kubwa,

— Wamepata hasara hawa Aws na Khazraj! Wamekusanyika katika kijiji cha Quba kumzunguka mtu ambaye wanamuita Mtume!

Ni vipi Salman alijisikia katika wakati ule?

Nikaanza kutetemeka kwa vujo baada ya kusikia maneno yake kiasi kwamba nilikaribia kumwangukia mmiliki wangu.

— Umesema nini? Umesema nini? Nilimuuliza kwa kurudiarudia, nilipokua nateremka haraka mtini. Alikasirishwa, japoqua, bwana wangu alinipiga kofi la nguvu na akasema,

— Ni kitu gani kwako? Hofia mambo yako!

— Hakuna cha kuhofia. Nilikua ninataka tu kupata uhakika kama kweli nilisikia sawasawa. Nilisema.

Njoo jioni ninaweza kukupeleka Quba, kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w), ubebe vitu vichache vya kula pamoja nami nilivyokua nimevitunza. Maneno yangu ya kwanza kwake yalikua,

— Nimesikia wewe ni mtu mwema na uko na marafiki wengi wenye uhitaji. Niko na chakula kidogo nilichokitunza kwa ajili ya sadaka. Niliposikia kuhusu hali yako, nikahisi unaweza kua na uhitaji Zaidi kuliko mimi.

Kwa hiyo nikatoa kile nilichokua nacho kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w). Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akawaambia maswahaba zake:

— Haya, chukueni wenyewe, na hakusogea hata mkono wake juu yake.

“Jambo la kwanza hilo” nilifikiria mwenyewe. Kisha nikaondoka kwenye uwepo wake na kurejea Madina. Nikaweka tena vitu vingine. Muda si mrefu Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akawasili Madina. nikaenda kwake tena na kumwambia

— Niligundua kuwa hukugusa kabisa sadaka yangu lakini hii ni zawadi nimekuandalia. Mara hii Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alikula na kuwaambia maswahaba zake wafanye kama yeye. “Jambo la pili hilo” Nilifikiria mwenyewe.

Baada ya hapo nilimtembelea Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) ambaye alikua katika makaburi ya Baqi Al-Gharqad kwa wakati huo, katika tukio la mazishi ya swahaba. Alikuameketi katikati ya maswahaba zake, akiwa amevaa sanda mbili ambazo zilikua zimemfunika wote sawasawa. Nikamsabahi, kabla sijazunguka upande wa nyuma, kwa matumaini huenda nikaona muhuri wa utume nilioelezewa na bwana wangu huko Ummariya. Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) akahisi nini ilikua kipaumbele changu, kwa hiyo alivuta kidogo sanda yake kutoka katika mgongo wake. Nikagundua ule muhuri na nikauona. Nikamdkondokea, nikamkumbatia na kuanza kulia. Kutoka pale na kuendelea nikawa muislam.

5- NGUO INAYOKINGA KUTOKANA NA AIBU NA MADHAMBI

Kabla dini ya kiislam haijazaliwa, waaarabu walikua wanavaa hijabu. Japokuwa hawakuwa na desturi ya kufunika mwili wote. Wanawake hawakua makini na kufunika miili yao yote pia, hatimaye aya ya 30 na 31 ya surat Nur zilipoteremka.

"Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari kwa wanayoyafanya. Na waambie waumuni wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao wala wasionyeshe uzuri wao isipokua kwa unao dhihirika. Na washushe shungi zao juu ya vifua vyao..." (Surat Al-Nur 24: 30-31)

Kwa aya hizi hadhi na heshima ya wanawake iliongezeka katika jamii. Kwa kujisitiri ipasavyo, wanawake wa kiislam walitunza heshima yao na sifa njema ya akina mama. Walidhihirishahisla za umaridadi na usafi wa nyoyo kupitia mavazi yao ya stara amabayo yalikua yanafunika miili yote. ilibatilisha nadhari ya kuwa kivutio na matamanio ya kimwili, lakini walibadiilika na kuwa mabinti waliokua alama ya usafi na adabu. Amri ya kujistiri haikua kwa wanawake tu ila na kwa wanaume pia.

Mtume wetu (S.a.w) alikua aktilia mkazo juu ya stara kwa wanawake. Mara moja asma, binti wa Abu Bakr, aliingia kwa Mtume wa Mwenyezi

Mungu(S.a.w) alikua amevaa nguo nyepesi. Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) akahamisha umakini wake na kumgeukia kisha akasema:

— Ewe Asma, endapo mwanamke akifika umri wa kuvunja ungo, haipendezi kwake kuonyesha maungo yake hususani hili na hili na akanyooshea uso na mikono. (Abu Dawud, Libas, 31/4104)

Abdullah Al Muhibbi (r.a.) alielezea: Asubuhi moja, nilimuona Mtume wetu (S.a.w) sokoni. Alikua akinadi:

— Enyi watu! Semeni "lailaha illallah" ili mpate wokovu.

Baadhi ya watu walikua wakimtemea mate usoni na wengine walikua wakimmwagia uchafu kichwani. Wakati wengine walikua wakimlaani. Hali hii iliendelea hadi mchana. Kisha akaja binti ambaye shingo yake ilikuwa wazi na maji na les. Alikua Analia. Mtume wetu (S.a.w) alichukua kikombe akanywa maji na aliosha uso na mikono yake. kisha akanyanya kichwa chake na kumwambia:

— Binti yangu mpendwa! Funika shingo yako na lesi yako. Usiogope kua baba yako atakamatwa, kuuwawa na kudhalilishwa. Tulipouliza msichana huyo alikua nani tuliambiwa.

— Alikua ni binti yake Zaynab. (Haythami, VI, 21)



6- VITA YA HANDAQ (MWAKA 627)

a) Angamizo kwa waislam

Vita ya Handaq ilikua ni katika vita mbaya sana na ngumu ambayo washirikina waliiizindua dhidi ya waislam. Washirikina walikua na tamaa ya kuwaangamiza na kuuondosha kabisa dola ya kiislam iliyoanzishwa Madina na Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w). Japokua walionekana kuibuka washindi katika vita ya Uhud, siku baada ya siku Waislam walikua wakiongezeka nguvu na idadi.

Muda mfupi baadhi ya makabila ya waarab yakawasaliti na kuwazunguka waislam. Wakachukulia faida juu ya hali hii, washirikina wakaanza kuijandaa kuivamia Madina. washirikina wa Makka walifanikiwa kuunda jeshi kubwa la watu elfu kumi kutoka Makka na makabila ya jirani. Wakati huu kazi ilikua kweli kweli kwa upande wa waislam.

Pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alipopata habari kuhusu maandalizi ya washirikina, alishauriana na maswahaba zake kuhusu njia gani itumike katika vita hii. Alipokea tamko mahiri kabisa lilloimarisha matumaini na msisimko kutoka kwa maswahaba zake. Yeye Mtume wetu(S.a.w) aliwaahidi pia kupata msaada wa Mwenyezi Mungu ikiwa hawatakiuka amri za Mwenyezi Mungu na kuvumilia ugumu katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu alimuongoza Mtume wetu(rehma na Amani ziwe juu yake) kuchimba mahandaki kuzunguka Madina. lakini bado Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) aliwaliliza maswahaba zake kama watataka kupigana nje ya Madina au kuchimba mahandaki kuzunguka mji ili kuulinda. Salman Al-Farisi akasema:

— Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Persia ilikua ni desturi yetu kuchimba mahandaki kuzunguka miji pindi tulipokua na mashaka ya uvamizi wa maadui

wapanda farasi. Tunaweza tukafanya hivyo pia. Jambo la kweli, pande tatu za Madina zimezungukwa na kuta ndefu na madhubuti za nyumba, miteremko mikali na kijisitu kizito cha mitende. Ni upande mmoja wa kaskazini mwa mji uko wazi kwa maadui kuvamia. Ikiwa watachimba mahandaki katika upande huu wa mji ambayo ni lazima maadui wapitie hapo, tutakua tumeulinda mji.

Mchango wa mawazo wa Salman uliwashawishi waislam. Njia hii ilikua haijulikani mionganoni mwa waarab ilionyesha kua sahihi kwenye ulinzi wa mji.

b) Mahandaki yanajengwa

Upopo uvumao ulikua unafanya mikono na miguu ya wafanyakazi kuganda ndani ya mahandaki. Hata hivyo, Madina ilikua inakabiliwa na njaa. Waislam walifanya kazi bila kula kwa siku tatu. Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alifunga jiwe katika tumbo lake ili kupunguza makali ya njaa kama waislam wengine walivyofanya. Alikua akichimba ardhi pamoja na maswahaba zake. Alikua akiwapa hotuba zilizowatia nguvu na kuwahamasisha dhidi ya njaa, baridi na uchovu.

Walipokua wanachimba mahandaki, wakaona jiwe kubwa na gumu. Hakuna hata mmoja aliyeweza kulivunja na kuliondoa. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alikwenda chini katika handaki, alilipiga jiwe lile mara tatu na kulivunja vipande vipande. Baada ya pigo la kwanza akawapa habari njema kua kipande kikubwa cha mji wa Damascus kitachukuliwa na waislam. Baada ya pigo la pili akatangaza kua Persia itachukuliwa na waislam hivi karibuni. Na baada ya pigo la tatu, akawapa habari ya kufunguliwa kwa Yemen kwa waislam. Habari hizi za kupendeza zillijaza mioyo ya waislam chini na ugumu wa baridi na njaa kwa matumaini na furaha.

Licha ya kero zote na ugumu, handaki kubwa lenye urefu wa takriban mita 5500 lilichimbwa. Handaki ilikua na pana kiasi cha farasi kukatisha, na urefu wa kutosha kwa yejote atakayedondokea ndani yake asiweze kutoka. Lilikua tayari kabla ya ujio wa maadui. Anayesimilia hapa chini ni Jabir (r.a.):

"Tulipokua tunachimba mahandaki kueleka katika vita ya Handaq, tulikumbana na jabali kubwa. Maswahaba wachache walim-uendea Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) na kumwambia kuwa wamekumbana na jiwe gumu ambalo ha-wakuweza kulivunja.

'Nitakwenda chini ya handaki mimi mwenye Mtume wa Mwenyezi Mungu aliowaambia. Kisha akashuka chini. Alikua kajifunga jiwe katika tumbo lake kutokana na njaa. Ililiku ni siku tatu tukiwa hatujala chochote. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alinyanya shoka na kuligonga jiwe lile, ambalo ililunjika vunjika na kugeuka kua mithili ya changarawe.

'Niruhusu niende nyumbani, Mtume wa Mwenyezi Mungu, niliomba baadaye. Umepewa ruhusa, nilikwenda nyumbani na kumwambia mke wangu kitu nilichokiona.... Mtume wa Mwenyezi Mungu yupo katika wakati mgumu. Tuna chochote cha kula?'

Ngano kiasi na mbuzi mdogo, alisema.

Hivyo nilimchinja yule mbuzi na kuandaan ngano. Tuliweka nyama katika chungu. Wakati mkate unakaribia kuiva na nyama ilikua linachemka jikoni katika mafiga chungu lilipokuwepo, nilikimbia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumwambia:

'Nina chakula kidogo, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Tafadhalii tutunuku sisi na watu wengine baadhi...'

"Kuna chakula kiasi gani?" aliuliza.

Nilimwambia kile tulichokua nacho. Kisha akasema, "Vizuri na kinatosha.....mwambie mke wako atoe nyama kwenye moto na aache mkate katika tanuri hadi nitakapowasili!"

Kisha akawageukia maswahaba zake na akapaza sauti, "watu wa mahandaki; njoo-ni.....Jabir ameandaa karamu kwa ajili yetu! Kila mmoja aliyejukwepo akatoka.

Kwa wasiwasi, nilikimbia nyumbani na kumwambia mke wangu, "Tizama kinachotokea sasa..... Mtume wa Mwenyezi Mungu anakuja na ansari wote, na muhajirina na watu wengne kama wao!

'Je, Mtume wa Mwenyezi Mungu ameuliza kuna chakula kiasi gani?' aliniuliza.'Ndio' nilim-jibu.

'Sasa usiwe na wasiwasi.' Alisema kwa utuliu, "anajua Zaidi kuliko unavyojua!"

Waliwasili muda mfupi baadaye. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akaawaambia waingie bila kujazana ndani. Liliingia kundi la maswahaba kumi kumi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alianza kugawanya mkate, akiweka nyama ndani yake na kuwapa maswahaba wote waliokua wana-subiria, mara zote alikua akifunika mfuniko wa chungu na tanuri kila alipomaliza. Hadi pale kila na maswahaba wote, takribani elfu moja walikula nan yoyo zao ziliridhika. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alirudia tena utaratibu huu. Palikua na chakula ambacho kilibakia hadi kufikia mwisho. Kisha akamgeukia mke wangu na kumwambia, "Kula hiki na wape baadhi majirani zako kwa hakika njaa hii imeteketeza kila mtu!' (Bukhari, Maghazi, 29; Muslim, Ashribah, 141; Waqidi, II, 452)

c) Siku ngumu

Pindi washirikina walipokuja mbele ya Madina, walikumbana na handaki. Mshangao wao ulionekana katika nyuso zao. Hata hivyo, walifikiria kuwa jeshi wa watu elfu kumi litaiteketeza Madina na kuwaondoha kabisa waislam wote.


Walikwenda juu na chini ya mahandaki, lakini hawakupata njia ya kukatisha. Kwahiyio wakaanzisha

makao yao makuu mbele ya Madina na kuizingira. Dhidi ya jeshi la washirikina elfu kumi, idadi ya waislam ilikadiriwa kufikia elfu

tatu. Kuzingira kule kulichukua takribani siku ishirini na saba.

Mgongano ukaanza kwa kurusha mishale na mawe.

Waislam walikua wanajitahidi kusimama dhidi ya jeshi la washirikina mbele ya handaki. Usaliti wa kwanza kwa waislam, ambao tayari ulikua katika hatua mbaya, ultoka katika kabilia la mayahudi la Banu Qurayza, japokua walikua wamesaini mkataba wa Amani na mshikamano na waislam. Walipoona ya kua kuna jeshi kubwa na lenye nguvu la washirikina limeizingira Madina, wakavunja makuballiano yao ghafla na kujuinga na jeshi la washirikina. Hawakumsikiliza Sa'd Ibn Muadh(radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) aliyekua ametumwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) kuwaonya na kuwapa ushauri. Wakadhihirisha uadui wao. Usaliti huu wa wayahudi ulisababisha hali kua tete kwa waislam. Kwa wanaume waliokua na silaha walikua wanapambana mstari wa mbele. Walikuwepo wanawake, watoto, wazee na wagonjwa waliobaki katika mji. Ilikua rahisi kwa mayahudi kuivamia Madina na kuchinja wanawake



wote na watoto wakati wanaume wa kiislam wakipambana na maadui mbele ya mahandaki. Usaliti mwininge ultokea kwa wanafiq. Walianza kufanya ujisadi. Waliacha kupambana na kuanza kusema kua waislam watashindwa katika vita ile.

Kwa upande mwininge, washirikina walikua wamechoshwa na kushindwa kuvuka handaki kwa muda mrefu toka wamezingira. Ukizingatia ilikua ni msimu wa winta na hali ya hewa ilikua ni ya baridi. Kile washirikina na askari mamluki wao walitarajia ingekua ni ushindi mwepesi wangeufikia ndani ya muda mfupi.

Washirikina walifanya shambulio kubwa ili kuwashinda waislam. Mishale ilikua ikidondoka chini ya waislam. Askari wa farasi walikua wanajitahidi kukatisha handaki. Wale waliofanikiwa kukatisha waliangamizwa na viongozi wa kiislam. Na wale waliodumbukia katika handaki wanajitahidi kutoka ili kuwasaidia wenzao. Washirikina majasiri na wenye


nguvu waliofanikiwa kuvuka upande wa pili wa handaki waliuliwa mara moja na Ali (r.a) na watu wake.

Siku iliyofuata ilikua ni siku ngumu zaidi katika vita. Kwa upande mmoja washirikina na kwa upande mwininge wayahudi kutoka katika kabile la Banu Qurayza walifanya mashambulizi. Mvua ya mishale kwa waislam ilikua haizuiliki hadi usiku. Waislam walijisikia wamekabwa. Siku hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) na maswahaba zake hawakupata hata muda wa kuswali sala zao. Waliziswali baadaye.

d) Mwisho wa kuzingira

Katika siku hizo ngumu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alinyanya mikono yake na kuomba, "Ewe Mwenyezi Mungu! Mola wangu Mlezi uliyeteremsha Quran na uliyeteleta Hukumu! Tawanya haya makabila ya waarab, vunja muungano wao na tikisa uwezo na nguvu zao."

Alipormaliza kuomba dua, palikua na nuru katika uso wa bwana Mtume (S.a.w) aliwapa bishara njema maswahaba zake kuhusu ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kutoa msaada.



Unadhani habari hii ilirudisha upya nguvu na msisimko wa maswahaba?

Nini unafikiri zilikua athari za habari hii njema?



Muda mfupi badaye, mpelelezi wa kiislam chakubimbi akaingia kwa wayahudi na washirikina na kusababisha ufa mionganini mwao. Licha ya kuwa upande mmoja, washirikina na wayahudi wakaanza kutizamana kama vile walikua maadui, pindi utegemezei mionganini mwao ulipovunjika, matamanio ya kupigana na waislam yaliondoka.

Usiku upepo ukaanza kuvuma. Upepo ambaao baadaye ulibadilika na kuwa dhoruba kubwa ulinyanya mahema na kuyatupa mbali. Vyombo wyo kupikia vilitupwa tupwa na matanuri yalibomoka, makundi ya ngamia na farasi yalitawanyika. Midomo, pua na masikio ya washirikina vilijaa mavumbi. Makao yao makuu yalipinduliwa juu chini. Hofu ilijaa miyoni mwao. Walikua katika mshangao wa hali ya juu, nyoyo zao zilizama katika huzuni; walipoteza matumaini na kuanza kupata hofu. Kutopata mafanikio kwa kuizingira Madina kwa muda mrefu kuliwachosha.

Washirikina wakaanza kutishika. Walikimbia bila kubeba mabomu yao, chakula na mali zao zingine. Asubuhi, waislam walikusanya vitu

viliyoachwa na maadui zao ikiwa ni pamoja na chakula na ngamia waliokua wamezagaa hovyo. Kwa namna hii, walinusurika na kuzingirwa na ugumu wa njaa.

Katika Quran tukufu tukio hili limeelezewa kama ifuatavyo: **“Na Mwenyezi Mungu akawageuza wasioamini katika hasira yao; hawakupata faida yoyote, na Mwenyezi Mungu amewatosheleza walioamni katika mapigano, Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mkuu.”** (al-Ahzab 33: 25)

Katika vita hii, watu wanne katika washirikina walikufa. Kwa waislam watu watano walikufa mashahidi. Baada ya vita, Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) alitoa habari njema nyingine. Alisema:

— Sasa ni zamu yetu.....washirikina hawatatuvalamia tena sisi ila tutawavamia wao.

Punde baada ya vita ya Handaq, wayahudi wa kabile la Banu Qurayza waliitwa na kuhojiwa kwa yale waliyoyafanya. Jeshi la waislam lilitoa adhabu stahiki kwa usaliti uliofanywa na kabile hili la kiyahudi.

7- SULUHU YA HUDAYBIIYAH (MWAKA 628)

a) Waislam walikua wanaihitaji sana Ka'bah

Imekua miaka sita tangu Mtume (S.a.w) na waislam kufukuzwa kutoka katika mji wao wa Makka na kulazimika kuhamia Madina. katika kipindi hiki, walikua wakijilinda wenyewe dhidi ya uvamizi wa washirikina kuwauwa na kuwapoteza katika vita ya Badr, Uhud na katika vita ya Handaq.

Hata hivyo, Imani mpya ya kiuslam, ambayo inathamini utu wa watu bila kubagua mtu wala kumkweza mtu. Ulikua unaendelea kuenea. Ingawa, waislam kuingia vitani na watu wao wenyewe wa Makka ilisababisha makabila ya karibu yasiyokua ya kiuslam kutoelewa juu ya uislam. Kutoekana na hili, Mtume wetu kipenzi (S.a.w) alitamani kusuluhiha na washirikina wa Makka. Kwa njia hii, Amani itakuwepo ndani ya jamii na makabila mengine wataenda kuufahamu uislam.

Kwa upande mwengine, wahamiaji wa Makka walikua wamekumbuka mji ambao walizaliwa, wakakua, lakini hatimaye wanalazimishwa kuondoka, na kuacha kila kitu nyuma. Kwa miaka sita iliopita hawakuweza kuitembelea Ka'bah takatifu ambayo mara kwa mara walikua wakienda kwa ajili ya kufanya ibada.

Katika moja ya masiku Mtume wetu (S.a.w) aliota ndoto. Aliwapa maswahaba zake bis-hara njema kuwa watakwenda kuitembelea Ka'bah mwaka huo. Maandalizi yalifanyika.


Watu wapatao 1400 waliondoka Madina kuele-ke Makka bila kuchukua silaha yoyote ya kivita kama mikuki n.k. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) hakutaka kuwatisha watu wa Makka au kuwafanya wahofie kua waislam wamekwenda kwa ajili ya vita. Nia ya waumini ilikua ni kwenda kutembelea Ka'bah tu na kuondoka. Walikua na ngamia 70 kwa ajili ya sadaka ya kuchinjia amabo wangechinja baada ya kumaliza hija yao ndogo (umrah).

b) Hofu ya watu wa Makka

Watu wa Makka waliingiwa hofu baada ya kusikia waislam wanakuja kutembelea Ka'bah. Wakakubaliana wasiwaruhusu kuingia ndani ya Makka. Mara moja walituma kundi la watu wa farasi mia mbili. Wakati huo waislam pamoja na mahujaj wengine walikua wamekaribia kabisa mji wa Makka eneo lilioitwa Hudaybiyyah. Japokua, ngamia wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) aliyeitwa Kaswa alipiga magoti pale. Hakuna aliyeweza kumfanya ngamia anyanyuke.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alisema hivi:

- Nguvu ya Mwenyezi Mungu iliyowafanya tembo wa Abraha washindwe kuingia Makka sasa haimruhusu Kaswa kusogea. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu nitawakubalia chochote ambacho wataniambia watu wa Makka niki-fanye nionyeshe heshima kwa vitu ambavyo Mwenyezi Mungu amenibariki. Hata kama ni ngumu kiasi gani mapendekezo yao yatakua, nitaridhia.





c) Mzungumzo ya Amani

Baada haya muda watu kutoka Makka wakaja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w). Akawaambia kuwa hawakuja na lendo la kupigana, ila kwa lengo la kufanya ibada. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akawaambia:


— Kama mtataka tunaweza tukasaini suluhu ya muda. Kabilalenu la kiquirayshi halitakiwi kuingilia mahusiano yetu na makabila mengine.- Ikiwa makabila haya mengine ya kiarab yataukubali uislam, wanatakiwa wawe huru kuufuata. Watu wa Makka hawatakiwi kuazuia. Kama wakiwa hawataki kuufuata uislam, ina maana kwamba kitatokea kama kilewatu wa Makka wanachotaka kitokee. Lakini

kama watajaribu kuzuia hili kutokea, naapa kwa Mwenyezi Mungu, nitapambana katika njia ya Mwenyezi Mungu hadi nitakapokufa. Mwenyezi Mungu atatumaa msaada wake kuhakikisha dini hii inakuwa na nguvu.

Baada ya hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) akamtuma Uthman (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) kwenda Makka. Alijadiliana pale na Abu Sufyan na watu wengine mashuhuri katika washirikina. Akawaambia kuwa lengo lao pekee lilikua ni kutembelea Ka'bah. Watu wa Makka wakasema:

— Ikiwa tutawaruhusu nyie nyote muingie Makka waarab watasema "Watu wa Makka wameewaogopa wiaslam." Unawenza

Ni kipi Uthman(r.a) alikifanya katika hali hii?



ukaizunguka Ka'bah ila hatuvezi kuwaruhusu wengine kuingia Makka.

Kwa Uthman (r.a.), alilikataa pendekezo hilo kwa kusema:

— Isipokua Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) azunguke Ka'bah, nami sitazunguka.

Tabia ya Uthman ilionyesha upendo na heshima kwa Mtume (S.a.w) iliwafanya watu wa Makka wapate hasira. Kwahiyo, hawakumruhusu aende tena na kumlazimisha abaki Makka.

d) Utii wa Ridwan

Waislam walipata mashaka kutokana na kucheleva kwa Uthman. zilikua zimeenea fununu kuwa ameuwawa. Ikiwa hili ni kweli, itamaanisha kuwa washirikina wametangaza vita dhidi ya waislam. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akasema:

— Inaonekana kuwa hatutaondoka bila mapigano.

Kisha kama tihadhari, aliwaita maswahaba zake na kutii juu ya "kutoogopa kuyatoa maisha yetu kupambana katika njia ya Mwenyezi Mungu." Maswahaba ambao walikua tayari kufa na kutoa mali zao katika njia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu walishikana mikono. Wakaahidi uaminifu wao kwa kusema:

— Tunaahidi kutekeleza matakwa ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) atakayo tutuma kuyafanya, kupigana kwa njia ya Mwenyezi Mungu hadi kifo, na kutowakimbia maadui.

Juu ya hili, Mwenyezi Mungu akashusha aya ifuatayo:

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu radhi waumini waliofungamana nawe chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao, basi akateremsaha utulivu juu yao, na akawalipa kwa ushindi wa karibu. Na ngawira nyingo watakazozichukua. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hekima." (al-Fath 48:18-19)

Kuishuhudia uaminifu wa waislam kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) na Imani yao madhubuti, watu wa Makka walipata wasiwasi wa kuanzisha vita. Haraka sana wakamuacha huru Uthman (r.a) na wakatuma mjumbe kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) kuzungumzia kuhusu masharti ya mkataba.

e) Kusainiwa kwa makubaliano ya Suluhu

Baada ya mzozo wa muda mrefu kati ya washirikina wa Makka na waislam, walifikia mapatano chini ya haya:

1. Waislam watarudi bila kutembelea Ka'bah mwaka huo. Wataitembelea Ka'abah mwaka utakaofuata lakini hawataruhusiwa kukaa Zaidi ya siku tatu na hawatabeba silaha yoyote.

2. Kipindi waislam wanatembelea Ka'bah, watu wa Makka watatoka katika mji wa Makka na hawatawaona waislam.

3. Patakuwepo na mkataba wa upande mmoja; watu wa Makka wakitaka kimbilio kwa Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake) watakabidhiwa juu la hitajio kwa maqraysh. Lakini kwa waislam kujikabidhi/kutaka ulinzi kwa maqraysh hawatakubaliwa.

4. Kabila lolote litakalotaka kuingia mkataba na watu wa Makka au makurayshi, wanawenza kufanya hivyo.

5. Patakuwa na Amani kwa kipindi cha miaka kumi, waislam watakuja Makka na maqrayshi watakwenda Syria kupitia maeneo ya waislam. Hapatakuwa na uvamizi au vita baina ya washirikina wa Makka na waislam.

f) Tukio la kuhuzunisha

Punde baaada ya kumaliza kuandika mkataba, Abu Jandal (r.a) alionyesha minyororo iliyokua ikitikotwa na kufungwa katika vifundo ya miguu yake. Aliku amebadilisha dini na kuukubali uislam muda mfupi uliopita. Baba yake alijaribu kumzuia kutohana na dini hii, lakini aliposhindwa alimfunga pingu na kumuweka gerezani. Abu Jandal alipata njia ya kutokea na kutafuta hifandi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alijiunga na jamii ya waumini.

Baba yake sahal alimtaka kijana wake kwake. Kutohana na vipengele vya mkataba, mtu aliyekua muislam na kutoroka kutoka Makka kwenda Madina na kutaka hifadhi kwa waislam huko Madina walitakiwa kurudishwa tena.

Licha ya maombi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) baba yake Abu Jandal hakubadilisha msimamo wake wa kumtaka kijana wake tena. Kwa Abu Jandal aliku akizungumzia mateso aliyoyapitia na alilaombwa waumini wasimrudishe tena.

Bila matumaini, Abu Jandal alirejeshwa kwa washirikina ili wasivunje mkataba. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alimtazama kwa macho ya huruma na kumwambia maneno ya kumfariji:



Endapo ungekuwepo pale, ungesema nini kwa Abu Jandal?

— Ewe Abu Jandal, kuwa na subra kidogo Zaidi. Mwenyezi Mungu atafungua njia ya wokovu kwako na kwa wale waliopata tabu kwa sababu ya Imani zao!

Kwa tukio hili la kusikitisha, maswahaba wakapata masikitiko na machozi yakawadondoka toka katika macho yao. Lakini hawakua na namna, kwa kua mkataba uliku tarayi umeshasainiwa!

Hadi wakati huo, watu wa Makka walikua wanawachukulia waislam kama jamii ambayo wangeigawanya na kuiharibu. Kwa suluhi ya

Hudaybiyyah, walikua wamehalilisha waislam kama dola. Suluhu hii ilikua ni hatua muhimu sana kwa kueneza uislam nje ya Madina, kwa sababu itaongeza mahusiano kati ya waislam na makabila ya jirani yasiyokua ya kiislam. Uislam ulianza kusambaa kwa uhuru bila kupata pingamizi lolote. Idadi ya waislam ikaanza kuongezeka pia.

UFUNGUO WA KWENDA MBINGUNI

Usiku ule Rabia hakupepesa macho akisubiri mbele ya mlango wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) hadi jua lilipochomoza. Rabia alimpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) kuliko alivyojipenda yeye mwenyewe na ilikua akijawa na furaha ya ajabu alipokua anamhudumia. Kwakuwa alikua anajua kua Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) ataamka na ataswali swala ya Tahajjud (swala kabla ya mapambazuko) alianda maji yake kwa ajili ya kuchukulia wudhu, taulo na mswaki na zulia la kuswalia jioni. Hatimaye akamuona Mtume (S.a.w) mlangoni. Akantabasamia Rabia alipomuona na kumsalimia.

Kila kitu kilienda vile Rabia alivyokua anataka. Ule, usiku mtulivu na mtukufu! Bwana wa walimwengu alikua anachukua wudhu mbele yake, na Rabia alikua anammwigilizia maji. Huu ulikua muda ambaa ni wa thamani sana kwa maisha yake yote. katika mawazo haya mazuri, alimwaga maji. Wudhu ulipokamilika, alimpatia taulo. Muda mfupi baadaye hakupata macho ya Mtume. Alikua amefedheheka na alikua akitizama chini. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akamuuliza:

— Rabia! Unatamani nini kwa mrejesho kutoka kwangu kwa huduma yako? Hii ilikua ni nafasi yake kubwa katika maisha yake.

— Ninatamani kua na wewe mbinguni. Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) aliuliza tena:

— Hauhitaji chochote cha kidunia?

— Ninatamani kua na wewe mbinguni.

Hili ilikua kweli tamano kubwa. Rabia alikua anataka nafasi kubwa mbinguni iliyokua inaitwa Maqam Mahmood(Nafasi tukufu) na kua jirani kabisa na Mtume kipenzi hasa cha Mwenyezi Mungu pale. Mtume wetu akamuuliza:

— Umeniomba kitu kikubwa sana kutoka kwangu. Hauwezi kuomba kitu kingine Zaidi ya hiki? Lakini Rabia akasema:

— Bwana wangu! ninahitaji kuwa na wewe mbinguni.

— Rabia! Nisaidie kwa kuswali na kusujudu sana.

Kutoka siku ile na kuendelea, Rabia alikua akiswali mara kwa mara. Aliswali sana. Rabia alipata ufunguo wa mbinguni, aliokua akiutamani. Alikua anaushililikilia ufunguo huo kwa makini mno ambaa hakuuacha hata alipofariki dunia.



8- KUWATUMA WAWAKILISHI NA BARUA ZA MWALIKO WA UISLAM

Uislam ulikua ni dini ya mwisho kushushwa kwa wanadamu. Ilikua ni dini halisi ambayo imebaki bila kubadilika. Kwahiyo, uislam ulikuia unatakiwa kutangazwa si tu ndani ya nchi za kiarabu bali ulimwengu mzima. Kwa mujibu wa vipengele vyta suluhu ya Hudaybiyyah, washirikina wa Makka hawataweza tena kuzuia uislam kuenea. Hivyo ilikua ni wakati wa uislam kueneza ujumbe wake katika miji ya mabali ghafla.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) aliifikisha mada hii kwa maswahaba zake baada ya kurudi Madina kutoka Hudaybiyyah. Wakaamu kutuma wajumbe na barua kwa viongozi wa dola za jirani na waarabu wa enzi hizo. Ili kutumia muhuri, pete ya fedha iliyokua

imeandikwa "Muhammad Ar-Rasul Allah" (Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu) ilitengenezwa.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alandika na kutuma barua kwa wafalme na viongozi wa dola za jirani mmoja baada ya mwengine. Maswahaba mashujaa walizifikisha barua hizi wakikatiza jangwa, milima na bahari, walipikua wanafanya haya, hawakua wakiogopa mapanga yenye kumeremeta ya wanyongaji au magereza zisizokua na juu za wafalme. Ilikua ni heshima ya hali ya juu kwa wao kupeleka barua za Mtume wa Mwenyezi Mungu zilizokua zimewakaribisha katika uislam.

Hizi ni baadhi...



a) Kumualika mtawala wa Byzantine Heraclius katika Uislam

Alikua Halifa kijana wa Dihya Al-Kalbi aliyepokea barua ya mualiko ya uislam kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) kwa Heraclius. Wakati huo Heraclius alikuwa Jerusalem. Mtawala aliyemkaribisha Dihya aliwaamuru wafanyabiashara wa kiarabu katika eneo hilo wampeleke kwake ili apate kujua habari zaidi juu ya Mtume wetu (S.a.w). Msafara wa biashara kutoka Makka ulikua katika mji huo kwa wakati huo. Abu Sufyan, kiongozi wa washirikina wa Makka, alikuwepo katika msafara pia. Heraclius alimuuiliza maswali kadhaa na kusikiliza majibu yake. muda mfupi baadaye Heraclius aliambatana na mapadri na wachungaji kutoka katika watu wake.

— Uko vipi ukoo wa Muhammad (S.a.w)?

— Ni kutoka katika familia tukufu.

— Je, wale waliofauta dini yake ni kutoka katika wenye yleo na matajiri au wanyonge katika jamii?

— Wengi wao ni watu masikini na wanyonge katika jamii.

— Je, idadi ya waumini wake inaongezeka au inapungua kila siku?

— Idadi inaongezeka.

— Je, kuna watu wanaoingia katika dini yake na kutoka kwa kuwa hawajaipenda?

— Hakuna hata mmoja.

— Je, amewahi kusema uongo?


— Hajjawahi kutokea.

— Je, amewahi kuvunja ahadi?

— Hapana hajjawahi kuvunja ahadi.

— Nini alichokutuma wewe kuja kukifanya?

— Amesema: "muabuduni Mwenyezi Mungu pekee. Msimshirikishe yeye na kitu



chochote." Ametutaka kuyaacha masanamu ambayo mababu zetu walikua wakiyaabudu. Ametuamrisha kuswali, wachamungu na tusijikweze.

Heraclius, alipata majibu ya maswali aliokua akiyahitaji. Aliongea kutoka moyoni:

Ikiwa ulichoniambia ni cha kweli, ardhi hii ambayo tunaishi sisi sasa hivi itachukuliwa nayeye muda si mrefu. Nilikua ninajua kua mtume atakuja, lakini sikutarajia kua atakuja tokea kwa waarabu. Endapo ningekua ninajua ningejitahidi kumfikia, ningevumilia mateso yote na ugumu. Ningeosha miguu yake na kumhudumia endapo ningekua karibu yake.

Baadaye, aliisoma barua kwa namna ambayo kila mmoja angeisikia.

"Bismillah al-rahman al-rahim... kutoka kwa mijumbe wa Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad kwenda kwa kiongozi Heraclius kiongozi wa Roma. Amani iwe juu ya waumini wanofuata njia iliyonyooka ya wokovu! Naanza: ninawalika kuupokea uislam na kusaidia kuueneza. Pokea uislam ili upate ukombozi. Hivyo Mwenyezi Mungu ataongeza ujira wako. Endapo hautakubali, jukumu la kutowafanya watu wako kuikubali dini ya kweli liko juu yako..."

Hotuba hii ya mfalme na barua viliwakasirisha sana mapadri. Wakati barua inasomwa ghasia na miguno ilianza ukumbini. Heraclius aliogopa mambo kutowezakana kudhibitiwa. Aliwataka Dihya na wafanyabiashara wa kiarabu watolewe nje. Alibadilisha mawazo yake na kuwaambia watu wake kua anataka kupima kiwango ya uaminifu katika dini yao. Kwa hiyo hofu yake ya kupoteza madaraka kulimfanya ashindwe kuukubali uislam. Japokua alimkari bisha Dihya kwa ukarimu na heshima kubwa.

Alimpa zawadi na maneno mazuri ya kukataa pendekeso la kuikubali dini mpya.

b) Kumualika mfalme wa Persia Husraw Parwiz katika uislam.

Barua ya Mtume ya kumualika mfalme wa Persia Husraw Parwiz katika uislam ilipelekwa na kijana wa Hudhaifa Abdullah. Katika barua iliandikwa hivi:

"Bismillah al-rahman al-rahim...kutoka kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad kwenda kwa mfalme wa Persia Husraw! Amani iwe juu ya wale walioukubali hikma, kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ambao wamekiri kua hakuna mungu ila Mungu mmoja na Muhammad ni mjumbe na Mtume. Ewe mfalme! Ninakualika wewe katika dini sahihi ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu nimetumwa kama muonyaji wa adhabu za Mwenyezi Mungu kwa viumbe na muongozo kwa watu wote. Ewe mfalme! Kua muislam ili ufikie ukombozi. Ikiwa hautaukubali mwaliko wangu, dhambi za wazorostria wate ziwe juu yako."

Pindi kiongozi wa Sasanian aliposoma barua hii, aliichana kwa hasira. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alipopata habari hii akasema:

— Ninawaombea wao na dola yao wagawanyike vipande vipande kama barua hiyo.

Sio muda mrefu baada ya hili, mfalme Husraw Parwiz aliuwawa na tumbo lake likachomwachomwa na kijana wake Shirwahy. Katika miaka iliyofuata, ardhi yote ya Persia ilitwaliwa na waislam.

c) Kwa Najashi Ashama Mfalme wa Abyssinia.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alimtumia barua Najashi Ashama aliye kua mkristo kwa asili yake kupitia Amr kijana Umayyah. Ashama aliwahudumia vizuri

waislam waliohamia Abyssinia na kwa Jaffar, kijana wa mjomba wake Mtume hapo mwanzoni. Aliwalinda wasidhuriwe na yeyote na kuwawekea mazingira mazuri yao kuishi kwa mujibu wa Imani yao. Katika barua iliandikwa:

Bismillah al-rahman al-rahim. kutoka kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Najashi, Mfalme wa Abyssinia. Ewe Mfalme, ukubali uislam. Ninafuraha kuhusu barka ulizopewa na Mwenyezi Mungu na ninamtukaza yeye kwa niaba yako. Ninakiri kuwa Yesu mwana wa Mariam, ni mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alimleta katika ulimwengu bila kua na baba, toka kwa mwanamke msafi na asiyekua na hatia Mariam ambaye hakuwahi kuolewa. Wakristo walimuabudu kama mungu. Ewe mfalme! Ninakualika ujikurubishe kwa Mwenyezi Mungu, ambaye ni wa pekee hana anayewiana naye na kunitii mimi na kitabu nilichokuja nacho. Kwa kua ni mtume wa Mwenyezi Mungu. Ninakuita wewe na watu wako kwenye dini ya Mwenyezi Mungu. Fuata ushauri wangu. Amani iwe juu ya wale wanaofuata njia iliyonyooka!

Mfalme wa Abyssinia akaandika barua ya kujibu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alimtaarifu kua amekua muislam.

Bismillah al-rahman al-rahim, kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu...kutoka kwa Najashi Ashama. Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Amani ya Mwenyezi Mungu, rehma na radhi ziwe juu yako. Mtume wa Mwenyezi Mungu, barua yako imenifikasi, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu na ardhi, ulichokisema kuhusu Yesu ni cha kweli. Allichotuambla ndicho unachotuambla wewe. Ninakiri kuwa wewe ni Mjumbe mwaminifu wa Mwenyezi Mungu ulyekuja kuthibitisha mitume wallotangulia. Ninaapa nitakutii wewe. Ninaamini kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu na nimekua muislam.

Unafikiri Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) alifurahi kiasi gani kwa kiongozi wa dola kuutukuza uislam?

9-USHINDI WA KHAIBAR (MWAKA 628)

a) Wayahudi wa khaibar wanataka kugana

Khaibar ulikuwa mji wa kiyahudi kilomita 170 kutoka Madina. ulikuwa na ngome saba. Na palikua na vijisitu vizuri vyatende na ardhi yenye rutuba.

Wayahudi ambao mwanzoni walikua wamaefukuzwa kutoka Madina, walianzisha makazi pale. Walikua wanawahimiza washirikina wa makabila ya kiarabu wawachukulie waislam kama maaadui. Moja ya sababu za vita ya Handaq ilichoche wa wayahudi hawa.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alitaka kufikia mkataba wa Amani na watu wa Khaibar. Alipokua njiani akitokea Hudaybbiyah, alituma ujumbe Khaibar akianza na kua anataka kuwe na mazungumzo ya Amani. Ingawa wayahudi wa Khaibar walikataa kusaini. Kwa upande mwengine watu wa Khaibar walijipanga kwa uvamizi wa Madina kwa msaada wa kabile la jirani, Gatafan. Kwa sababu, Japokua waislam walikubaliana na vipengele vizito vyatende ya Hudaybbiyah, walikua wanafikiria kua waislam ni dhaifu na wenye kukata tamaa. Japokua hili halikua tattizo. Wanafiq walikua wanawashawishi watu wa Khaibar kupigana. Kabilo la Gatafan lilikubali kushirikiana na wayahudi kuwavamia waislam.

Kwa hali hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) aliamua kuchukua hatua kabla ya kuaruhusu maadui kufanya maandalizi yao na kukatisha katika mipaka ya kabilo la Gatafan. Walipanga wapanda farasi 2000 na askari wa miguu 1600 kuelekea Khaibar.

b) Ngome za Khaibar zinashindwa

Baada ya kuswali swala ya alfajir, Mtume (S.a.w) alitangulia kuelekea Khaibar. Asubuhi,

wayahudi waliokuwa wameacha nyumba zao na makazi yao na makasia yao kuelekea kwenye kazi zao, walishangaa kuona jeshi la waislam mbele yao. Walipiga mayowe: "Muhammad, kwa jina mungu, Muhammad na askari wake...." Na wakakimbilia katika ngome zao. Miiongoni mwa ngome saba ndani Khaibar, ngome iliyokua imejitosheleza na kuandaliwa dhidi ya vita iliitwa Kamus. Palikua na vyakula pamoja na silaha nyingi ndani yake. Wayahudi walikua warmejiandaa kikamilifu kwa ajili ya mapambano. Matokeo yake, hawakukubaliana na pendekezo la Mtume (S.a.w) la Amani.

Mwisho wa kuzingira kwa takribani siku ishirini, kila ngome ilishikiliwa moja baada ya nyingine isipokuwa Kamus. Waislam hawakua na matokeo kutohuna na uvamizi wao uliofanywa chini ya viongozi wa makamanda wa kiislam. Ngome yaya Kamus haiwezekani kutekwa.

Mwisho, Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akaongea:

— Kesho nitampa bendera mtu ambaye mikono yake Mwenyezi Mungu atajaalia ushindi dhidi ya Khaibar. Ni mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda pia.

Bila kujua heshima hii anakwenda kupewa nani, kila mmoja alisubiria hadi asubuhi kwa matumaini kuwa atakua yeze ndiye mtu mwenye bahati hiyo. Asubuhi Mtume (S.a.w) akasema:

— Yuko wapi Ali? Niitieni!.

Ali alikuwa anasumbuliwa na maumivu makali ya macho. Kwahiyo, hakuna aliyedhani kua bendera atapewa yeze. Maswahaba:

— Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Ali anamaumivu makali sana ya macho. Walimleta Ali wakiwa wamemshikilia mikono. Mtume wetu

Endapo ungekuwa katika viatu vyatende ya Ali, ungewaza nini?

(rehma na Amani ziwe juu yake) aliomba dua na kupulizia machoni kwa Ali. Macho yalipona ghafla. Ilikua kana kwamba hakuwahi kuwa na maumivu hata kidogo. Kisha Mtume akampa bendera Ali.

Ali mwanzoni aliwaalika wayahudi katika uislam. Hata hivyo hawakuukubali. Hawakukubali kwa Amani isipokua waliendelea kupigana. Zaidi ya hapo, walisoma aya za kishujaa, walileta changamoto dhidi ya waislam. Baadaye, mpiganaji hodari kushinda wote wa kiyahudi, Mahrab alitoka nje ya ngome na kusema:

— Yupo mwanaume shujaa wa kuja kunikabili mimi?

Ali mwenyewe akamkabili, mpambano wa kishujaa. Ali alimuangusha mpiganaji huyu shujaa wa kiyahudi. Mahrab alipokufa wayahudi wakakosa hamasa na wakapoteza upinzani. Hawakupinga tena zaidi. Kwa kukata tamaa waliacha ngome. Kwahiyio Khaibar ilikua chini ya utawala wa kiislam kabisa. Na Ali akawa ndio mshindi wa Khaibar. Wakati wa mapigano wayahusi 93 walikufa. Kwa upande mwingine, waislam walikufa mashahidi 15.



c) Njama ya kumuua Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kisasi

Mtume (S.a.w) alikaa siku chache Khaibar. Licha ya huduma za kibinadamu walizozionyesha wayahudi walipanga kumuua Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w).

Binti immoja wakiongozi wa kiyahudi aliyeitwa Zainab aliandaa karamu. Kisha akamualika Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na marafiki zake wengine. Aliweka kipande cha nyama yenye sumu mezani. Punde baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) kukata kipande kidogo na kukitia mdomoni, ghafla akakitema na kusema: "Nyama hii imeniambia kua imetiwa sumu, rafiki zangu msile. Lakini Bishr kijana wa Bara alikua maekula kiasi kidogo, hivyo akadhirika na sumu na akafariki pale pale.

Pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alipowauliza wayahudi kwanini wamefanya vile, wakasema:

— Tulifikiria endapo ni muongo, tukufukuze, lakini umekua mtume wa kweli, sumu hii isingekudhuru wewe.

Pengine walitoa jibu lenye werevu. Mwanamke aliyetia sumu katika nyama hata hivyo hakupinga kua alifanya hivyo. Alisema:

— Baba yangu, mjomba wangu, mume wangu na kaka zangu, wote wamekufa katika vita. Nilifanya hivyo ili kutekeleza kisasi changu.




10- MWAKA MMOJA BAADYE WALITEMBELEA KA'BAH

Kama ilivyoelezwa katika suluhu ya Haudaybiyyah, mwaka mmoja baadaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) pamoja na maswahaba Zaidi ya 2000 walikuja Makka wakitokea Madina.

Washirikina waliondoka Makka waliposikia waislam wanakuja, kama walivyokubaliana mwaka mmoja uliopita. Waliwatazama waislam kuititia mahema waliyoyajenga katika vilima kuzunguka mji.

Unafikiri waislam walitembelea Ka'bah baada ya kusubiria

muda mrefu walivyojisikia? Unafikiri walifanya nini?



Kuingia kwa waislam Makka kulikua kunahofisha kwelikweli. Mtume (S.a.w) aliku mbele na ngamia wake Kaswa. Maneno ya "Allahu Akbar... Labbayk Allahumma Labbayk..." yalitoka katika nyoyo za waislam zilirindima katioka anga ya Makka. Ka'bah ambayo walikua wanaitamani kwa muda mrefu sasa ilikua mbele yao.

Walifanya Umra yao kwa kuchelewa mwaka mmoja Zaidi, ambayo hawakuweza kuitekeleza mwaka mmoja uliopita.

Waislam walikaa Ka'bah kwa siku tatu. Muda mfupi baadaye, washirikina kwa udadisi na tamaa walifuatisha ibada yao na tabia zao kwa mbali. Walikua wakisemezana wao kwa wao juu ya waislam kuwa:

— Ni wakarimu na wastaarabu hawa waislam walivyo!

— Wanawali pamoja, kwa Amani na heshima kwa kila mmoja!

— Hawalewi wala hawalaaniani baina yao kama tufanyavyo sis!


— Ndio, ni wa kawaida na watu wenye akili safi na tabia njema!

— Wanaposwali au kuongea baina yao, wanapendana na kujaliana kwa uadilifu mionganoni mwao. Sio makatili baina yao kama sis!

— Tizama, pia ni wanyenyekevu na kumuabudu Mwenyezi Mungu muda wote. Wako na Amani na utulivu!

— Hata hiyo, ni watu wazuri namna gani walivyo!

Washirikina wa Makka walikua wameathirika vilivyo na tabia njema za waislam na ufanuzi katika ibada zao. Walipokua wakijulishana kwa ukaribu kwa waislam amba walikua maadui mwanzoni, watu wa Makka wakaanza kuwatamani. Palikuwepo na watu mionganoni mwao amba hata walianza kufikria kuhusu kubadiilisha dini na kuufuata uislam.



11-VITA YA MUTAH (MWAKA 629)

- a) Pindi mjumbe wa Mtume alipokufa kwa kuulingania Uislamu.

Alipokua anatuma wajumbe kwa viongozi wa nchi za jirani ili kuwakaribisha katika uislam,

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alituma barua kwa Shurahbil, gavana wa Busra ndani ya Syria pia. Alikua Harith Ibn Umayr aliyefikisha barua kwa Shurahbil aliye kua Mkristo chini





ya uongozi wa Byzantine. Harith alikwenda kwa Shurahbil na kumkuta katika mji unaoitwa Mu'tah. Alianza kua alikua mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, akampatia barua.

Alipoisoma barua, Shurahbil kwa fakhari na kiburi alimuua Mjumbe wa waislam Harith. Hii ilimaanisha kudharau sharia za ndani na heshima. Ilikua pia ni dhihaka na changamoto kwa aliyemtuma mjumbe.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alikua na jeshi la watu 3000 liliojianda ili kulinda heshima ya uislam. Alituma jeshi lake chini ya kamanda Zaid Ibn Harith kwa mtu katili Shurahbil. Aliwaambia makamanda:

— Mkaribisheni katika uislam. Lakini asipokubali piganeni naye! Msihadhuru watoto, wanawake na wazee! Msiharibu nyumba za watu wasiokua na hatia au kuua

wanyama au kukata miti.

Baadaye,
aliendelea na
hotuba yake kwa
kusema:

— Endapo Zaid
atakuwa shahidi,
Jaffar atakuwa
kamanda. Ikiwa
Jaffar atakuwa shahidi,
Abdullah Ibn Rawaha atakuwa
kamanda. Na ikiwa naye atakuwa
shahidi, basi waislam watachagua
yoyote mionganini mwao na atakuwa
kamanda wao!

b) Nguvu ya maadui na hamasa waliyokua nayo waislam.

Baada tu ya kuingia katika ardhi ya Syria, waislam waligundua kua kuna jeshi la watu wapatao 100,000 hivi likiwasibiri. Maadui pia walikua limejitosheleza kwa silaha na vifaa vingine vya mapigano. Kwa upande mwingine, idadi ya waislam ilikua ni 3000 tu.

Zaid kamanda wa jeshi alikusanya baadhi ya mashujaa wake na kuzungumzia hali halisi pamoja nao.

Nini majemedari 3000 wakiwa na silaha hafifu wakifanye kwa jeshi madhubuti la watu 100,000? Wanatakiwa wamuarifu Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusiana na hali na wapambane kwa mujibu wa mujibu yake?lakini kwani hawakua hapa kwa ajili ya mapigano? Hawawezi kurudi bila kupambana.Abdullah Ibn Rawaha alisawazisha hofu yote.

— Ndugu zangu! Tumekuja kutoka tutokako na ni lengo letu kuu,ambalo ni kufa mashahidi. Tupambane ili kutetea dini yetu. Tutakua mashahidi au kuchukuliwa kama wateka wa vita....je, yote sio mazuri?

Hotuba ya Abdullah ilitia nguvu Imani ya waumini mashujaa na kuamsha hisia zao za jihad. Walisema wote kwa pamoja:

— Kijana wa Rawaha yuko sahihi! tupambane!

c) Zamu ya kuheshimika kwa kuuawa mashahidi

Majeshi mawili yalikutana katika eneo linaitwa Mutah. Zaid kwa kujiamini akapita mbele alikwa na bendera mkononi mwake.

Alipambana kishujaa akionyesha kua hakua akiogopa kifo. Japokua aliyatoa maisha yake kwa ajili ya uislam chini ya mikuki ya maadui.

Baada ya Zaid kufa shahidi. Ja'far haraka sana alichukua bendera yake. Yeye pia alipambana kishujaa. Pindi mkono wake ulipokatwa, alichukua bendera kwa mkono wa kushoto. Pindi mkono wake wa kushoto nao ulipokatwa, alishika bendera kwa vipingu vya mikono. Hata hivyo alijeruhiwa vibaya sana. Hakuiacha bendera hadi pumzi yake ya mwisho. Mwishoni, aliuwawa pia. Baada ya Ja'far, Abdullah Ibn Rawaha alichukua bendera. Akisoma shairi, alipambana kishujaa pia. Alipambana hadi mwili wake ulipokuwa umejawa na majeraha ya mapanga na mishale.

Muda ambaa Abdullah Ibn Rawaha anauliwa, askari walibaki bila kamanda. Baada ya tukio hili, waislam walikosa matumaini dhidi ya jeshi la maadui zao ambalo lilikua na watu mara 40 zaidi ya wao. Iakini Khalid Ibn Walid aliyekua mtaalam wa vita aliwakusanya wanajeshi waliokua karibia watawanyike. Japokua alikua ndio ameukubali uislam muda mfupi uliopita, waislam walijikusanya kumzunguka yeye tena. Khalid alichukua ukamanda na kupambana hadi jioni akiwa na bendera mkononi mwake. Kutoka siku hiyo Khalid alilijikana kama "Sayfullah", yaani "**Upanga wa Mwenyezi Mungu.**"


Wakati wa usiku Khalid alilipanga jeshi lake. Aliwaweka wale waliokua nyuma safu ya mbele, na wale waliokua mbele safu ya nyuma. Alibadilisha nafasi ya wale waliokuwepo upande wa upande wa kulia na

Unadhani mpangilio uliopangwa na Khalid uliathiri vipi kiini cha vita?

wale waliokuwepo upande wa kushoto na wale wa kushoto upande wa kulia.

Katika siku iliofuata, maadui walidhani kua waislam wengine wallikuja kwa ajili ya kutoa msaada kwa waislam walipoona maaskari tofauti mbele yao. Kwa shambulio la ghafla na

lenye nguvu lililotoamriwa na Khalid asubuhi na mapema, maadui walilazimika kukimbia. kwa kutumia fursa hii, Khalid kwa umakini mkubwa akawarudisha nyuma askari wake. Walirudi Madina pasipo kuhesabika kupoteza vita. Katika vita hii kali dhidi ya watu 200,000, waislam 12 tu walikufa mashahidi vitani.



MAYATIMA WA JA'FAR

Mke wa Ja'far, Umays Bint Asma alisimulia:

Siku hizo zilikua ni siku za karibuni kwa jeshi kurudi kutoka katika vita ya Mu'tah. Tukiwa na familia nzima, tulikuwa tunatizamia Ja'far akirejea. Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuja kwetu. Siku hiyo, baada ya kua nmemaliza kukanda unga kwa ajili ya kupika mkate, nilizikosha nyuso za watoto wangu na kuwachana nywele zao. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akaniuliza:

— Ewe Asma! Watoto wa Ja'far wako wapi?

Aliwafariji na kuwabusu mmoja baada ya mwingine. Wakati huo huo, machozi yalikua yakimtiririka mashavuni mwake. Nikamuuliza:

— Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwanini unalia? Kwanini unawachukulia

watoto wangu kana kwamba ni yatima? Je, kuna taarifa za majonzi kumuhusu Ja'far na wenzake?

Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w):

— Ndio!wameuwawa leo!

Nilianza kulia na kusema: "O bwana wangu! O Ja'far wangu!"

Kisha Mtume akaenda kwa Fatima na kumwambia:

— Pika chakula kwa ajili ya familia ya Ja'far. Wana huzuni leo.

Tuliletewa chakula kwa siku tatu. Katika siku ya mwisho ya tatu, Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alikuja kwetu na kutuambia:

— Msilimlilie kaka yangu zaidi ya hapa. Kutoka saivi na kuendelea, ninajukumu la kuangalia watoto wa ndugu zangu.



MASWALI

NIMEJIFUNZA KIASI GANI?

1. Ni kitu gani Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alikitaka kabla ya vita ya Uhud? Ni yapi yalikua majibu baada ya kuwashirikisha maswahaba zake?
.....
.....
2. Kwanini wapiga upinde wa kilim cha Ainayn waliondoka katika nafasi zao?
.....
.....
3. Unafikiri nini yangekua matokeo ya wapiga upinde wasingeondoka kuacha nafasi zao katika vita ya Uhud?
.....
.....
4. Ni mapenzi kiasi gani Mtume (S.a.w) aliyonyesha katika mazishi ya mjomba wake Hamza kwa waliokufa mashahidi katika vita ya Uhud?
.....
.....
5. Alipopewa pendekezo la kuwekwa Mtume (S.a.w) badala yake ili kuyanusuru maisha yake dhidi ya kunyongwa, jibu gani Zaid aliwapa?
.....
.....
6. Ni vitu gani vingine vilikatazwa pamoja na pombe na kusema kama kazi ya shetani latika aya?
.....
.....
7. Ni alama gani alizofundishwa Salman Farisi ili kumtambua Mtume wa kweli aliyekua amemfanya utafiti tangu muda mrefu?
.....
.....
8. Katika mwaka gani ambao vita ya Handaq ilitokea kwa mujibu wa kalenda zote mbili ya juu nay a mwezi?
.....
.....

9. Wakati waislam walikua karibu kushindwa katika vita ya Handaq, ni jinsi matokeo yalibadilika na kua ushindi?
-
.....

10. Vipi vilikua vipengele vikuu katika mkataba wa Hudaybbiyah?
-
.....

11. Kwanini Abu Jandal aliyekua ameukubali uislam na kwenda kwa Mtume(S.a.w) punde tu baada ya mkataba wa Hudaybbiyah alirudishwa tena?
-
.....

12. Ni kitu ambacho Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) aliomba kutoka kwa wafalme wa nchi za jirani katika barua zake za mwaliko wa Uislam?
-
.....

13. Ni udhuru gani wayahudi waliutoa kutokana na kujaribu kutaka kuumua kwa sumu Mtume (S.a.w)?
-
.....

14. Ni kitu washirikina walikifiria kuhusu waislam waliotembelea Ka'bah mwaka mmoja baada ya mkataba wa Hudaybbiyah?
-
.....

15. Ni maswahaba gani watatu walioongoza kama makamanda wa jeshi katika vita ya Mu'tah? Baada ya makamanda hawa watatu, ni nani alichukua ukamanda?
-
.....

Lipi Hapa ni Jibu Sahih?

- 1) Ni lini vita ya Uhud iliteke kwa mujibu wa kalenda ya jua?
 - A) 623
 - B) 624
 - C) 625
 - D) 626
- 2) Katika kuamua mfumo wa vita, katika jambo gani Mtume alikua akilitilia maanani sana?
 - A) Ujasiri
 - B) Uaminifu
 - C) Ushauri
 - D) Ushujaa
- 3) Ni nani Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) aliemuacha Madina kama wakala alipokua anakwenda katika msafara wa kijeshi?
 - A) Ali
 - B) Uthman
 - C) Abdullah ibn Ummi Maktum
 - D) Zaid ibn Thabit
- 4) Ni jambo gani ambalo Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) aliona na kusisitiza wapiga upinde alioaweweza katika mlima wa Ainayn?
 - A) Kuilinda bendera
 - B) Kutoondoka sehemu yao hadi atakapowapa maelekezo ya kuondoka yatakapowajia
 - C) Kumlinda Hamza
 - D) Kushuka chini ya mlima katika uwanja wa vita ili kumsaidia Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) ikiwa wataona jeshi la waislam lipo matatizoni
- 5) Kwa sababu gani wapiga upinde katika kilima cha Ainayn waliacha eneo lao?
 - A) Kwasababu hawakuweza kuvumilia kuona jino la Mtume likiwa limevunjika
 - B) Ili kuwasaidia marafiki zao
 - C) Kukusanya ngawira kwa kudhani kuwa wameshapata ushindi
 - D) Kwa kuwa mbinu za vita zilikua zimeamuliwa kwa namna hii
- 6) Ipi moja kati haya hayakua maafa yaliyomtokea Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w)?
 - A) Midomo yake mitukufu ilipasuka
 - B) Jino lake tukufu lilivunjika
 - C) Kucha zake tukufu zilivunjika
 - D) Pete mbili zilivunjika kutoka katika kofia yake na kumtoboa shavu lake
- 7) Ni vita gani ambayo Mtume (S.a.w) alitamani kufa shahidi pamoja na maswahaba wengine?
 - A) Vita ya Mu'tah
 - B) Vita ya Uhud
 - C) Vita ya Handaq
 - D) Vita ya Badr

- 8) Jinsi gani Abu Sufyan, aliyejua kiongozi wa washirikina wa zama hizo, alitoa maoni juu ya majibu yenyé kipaji ya Hubaib aliyotoa kujibu pendekezo alilopewa alipokua katika kitanzí?**
- A) Mtume wao lazima awakamate watu waliowateka
 - B) Waislam hawa walikuawamerukwa na akili
 - C) Sijawahi kuona mtu anayependwa sana na marafiki zake
 - D) Nadhani unatakiwa kuifikiria nafsi yako kwanza, tumia akili yako
- 9) Kitu gani ambacho hakikukatazwa katika aya inayohusiana na ulevi?**
- A) Kamari
 - B) Kupiga ramlii
 - C) Kuabudu masanamu
 - D) Zinaa
- 10) Wapi kati ya watu hawa wanaohusiana na pombe wamelaaniwa na Mtume (S.a.w)?**
- I. Mnywaji
 - II. Yule anayesaidia wengine wanywe pombe
 - III. Yule aliyebeba
 - IV. Yule anayeliona
 - V. Yule anayenunua na kuuza
- A) I, II na III B) I, II, III na V
 - C) I, IV, V D) I, II, III, IV, V
- 11) Muhuri wa utume ulikua wapi katika mwili wa Mtume (S.a.w)?**
- A) Bainya nyusi zake
 - B) Katika kiganja chake kitukufu
 - C) Katika mashavu yake matukufu
 - D) Katika mgongo wake, baina ya mabega mawili
- 12) Ni sura gani katika Quran inayoongelea Zaidi juu ya matukio yaliyotokea katika vita ya Handaq?**
- A) Surah al-Baqara B) Surah al-Ahzab
 - C) Surah Yasin D) Surah al-Rahman
- 13) Ni makundi gani mawili yaliwasaliti waislam katika vita ya Handaq?**
- A) Wayahudi na wakristo
 - B) Wakristo na washirikina
 - C) Wanafiq na wakristo
 - D) Wanafiq na wayahudi
- 14) Munafiq ni mtu gani?**
- A) Mtu anayejua muislam kwa nguvu
 - B) Mtu anayekataa kua muislam kwa ulimi wake
 - C) Mtu anayeshirikiana na wasioamini dhidi ya waislam
 - D) Mtu anayesema kua yeye ni muislam hata kama haamini katika uislam
- 15) Kwa miaka mingapi mkataba wa Hudaybbiyah ulikubaliwa kuwa halali?**
- A) 16 B) 14
 - C) 10 D) Hajaelezwa

16) Ipi kati ya aya zifuatazo inahusiana kabisa na mkataba wa Hudaybbiyah?

- A) "Na endapo utazihesabu neema za Mwenyezi Mungu, hautaweza kuzuhesabu"
- B) "Amri yake, anapotaka kitu chochote, husema: Kua, nalo hua."
- C) "Lakini kuna uwezekano wa kulichukia jambo kumbe lina kheri na wewe"
- D) "Lakini wale watakaofanikiwa ni waliojisafisha, na kulitkuza jina la Mola wao Mlezi, na (kuzituliza nyoyo zao) katika swala."

17) Ni yapi kati ya yafuatayo ni matokeo chanya ya mkataba wa Hudaybbiyah?

- I. Washirikina wallidhinisha waislam kama dola.
 - II. Uenezaji wa uislam uliongezeka.
 - III. Uhusiano na mazungumzo kati ya waislam na makabila na dola za jirani uliongezeka.
 - IV. Waislam waliweza kutembelea Ka'bah mwaka ule.
- A) I, IV
 - B) I, II, IV
 - C) I, III
 - D) I, II, III

18) Ni kiongozi gani wa dola alijibu kwa kukubali barua ya mwaliko wa Mtume wa Mwenyezi Mungu alipomualika katika dini ya kweli ya Allah(Sw)?

- A) Heraclius mfalme wa Byzantine
- B) Husraw Parwiz mfalme wa Iran
- C) Ashama mfalme wa Abyssinia
- D) Shurahbil gavana wa Busra


19) Katika siku ya kuivamia Khaibar, Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa swahaba gani bendera?

- A) Zaid
- B) Umar
- C) Ali
- D) Sa'd

20) Ipi ilikua idadi ya waislam dhidi ya jeshi la watu 100,000 katika vita ya Mu'tah?

- A) Elfu tano
- B) Elfu hamsini
- C) Elfu kumi
- D) Elfu tatu

FUMBO

**Kwenda kulia**

2. Kabilo la kuyahudi lillowasaliti waislam; wana wa Quraya
5. Mtu anayeabudu moto; muabudu moto.
8. Mtu anayejifanya kua ni muislam, ingawa haamini haswa katika dini na Mtume; mnaifiq
9. Msomi wa dini ya kikristo.
11. Swahaba wa Mtume aliyeleshimika aliyechukua bendera baada ya Zaid na baadaye kufa shahidi katika vita ya Mu'tah
13. Tukio ambalo Mtume (S.a.w) aliwalaani wasaliti baada ya kuswali swala ya alfajr kwa siku arobaini: Maafa ya kisima cha Maunah
16. Mtu aliyetoa maisha yake katika njia ya Mwenyezi Mungu; shahidi
17. Jina la utani alilopewa Khalid Ibn Walid kutokana na mafanikio aliyoypata katika vita ya Mu'tah.
18. Mtu anayeabudu masanamu tofauti na Mwenyezi Mungu
19. Jina la vita ambalo washirikina waliwaalika watu wa makabila ya jirani na kuunda jeshi la watu 100000; vita ya Handaq
20. Jina la utii alilopewa Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na Amani ziwe juu yake) juu ya kuchelewa kwa Uthman na kuzagaa kwa fununu za kuuliwa kwake.

Kushuka chini

1. Mjomba wake kipenzi na Mtume aliyeuawa katika vita ya Uhud.
3. Jina la ngamia wa Mtume.
4. Jina la mkataba uliosainiwa kati ya waislam na washirikina wa Makka.
6. Jina la kilima ambacho wapiga upinde walikaa katika vita ya Uhud
7. Cheo alichopewa kiongozi wa Abyssinia.
10. Mmoja wa maswahaba shujaa ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu alimteua kua mbebaji wa bendera katika siku ya kuishinda Khaibar.
12. Mmoja wa maswahaba wa Mtume. Salman alikua na asili ya Persia na alizaliwa katika familia za wazorostria. Baada ya kufuatilia kwa muda mrefu njia iliyonyooka alimpata Mtume wa dini ya kweli.
14. Jina la kilima ambacho wapiga upinde walikaa katika vita ya Uhud
15. Kitu kinachotambulika kama kiongozi wa madhambi yote, na kilichokatazwa kutumika.

“Bismillah al-rahman al-rahim...
kutoka kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu na
Mtume Muhammad kwenda kwa mfalme wa Persia
Husraw! Amani iwe juu ya wale walioukubali hikma,
kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ambao
wamekiri kua hakuna mungu ila Mungu mmoja na
Muhammad ni mjumbe na Mtume. Ewe mfalme!
Ninakualika wewe katika dini sahihi ya Mwenyezi
Mungu, kwa sababu nimetumwa kama muonyaji
wa adhabu za Mwenyezi Mungu kwa viumbwe na
muongozo kwa watu wote. Ewe mfalme! Kua muislam
ili ufikie ukombozi. Ikiwa hautaukubali mwaliko wangu,
dhambi za wazorostria wate ziwe juu yako.”





TABIA ZINAZOMFANYA MTU KUWA MUISLAM MZURI



ADABU



- ✿ *Adabu katika udugu*
- ✿ *Kuonyesha heshima kwa wakubwa*
- ✿ *Adabu ya kuingia na kutoka nyumbani*
- ✿ *Adabu ya kutoa na kupokea zawadi*



ADABU KATIKA UDUGU

Waumini tu ni ndugu!

Kabla ya uislam, watu waliokua wanagawanyika katika makabila walikua katika hali ya vita. Hitilafu ndogo ilikua inatosha kuanza vita kudumisha heshima ya kabila. Mshikamano wa ukoo ulikua unakuja kabla ya mshikamano wa kidini na Imani. Kwa mujibu wa amri tukufu, "Hakika waumini si chochote ila ndugu. Kwahiyopatanisheni baina yenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe." (al-Hujurat 49:10), Mtume Mtukufu (Rehma na Amani ziwe juu yake) alitangaza udugu mionganoni mwa waumini. Baadaye, hisia za udugu wa kidini uliushinda ule wa kiukoo; mfano katika vita ya Badr waislam walilazimishwa kuingia, muumini alipigana dhidi ya mjomba wake, kaka yake hata baba yake. katikati ya vita mathalani, Abu Bakr(Mwenyezi Mungu awe radhi naye) alikutana uso kwa uso na kijana wake na Abu Ubayda ibn Jarrah (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) dhidi ya baba yake na Hamza (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) dhidii ya kaka yake.

Hivyo kwa undani kabisa Ansar wa Madina waliichukua dhana hii ya udugu kufuatia Hijra iliyofanya na Muhajirun usawa katika umiliki wa

majumba yao. Walionyesha tukio ambalo halija-wahi kutokea la kutokua na ubinafsi na ukarimu.

NDUGU ZETU WANAHITAJI HUDUMA BORA NA KUJALIWA

Mtume Mtukufu(rehma na Amani ziwe juu yake) alitia ushauri ufuatao katika kundi la maswahaba zake, kabla hajwajatembelea kundi jingine la ndugu:

"Mnakuja kwa ndugu zenu; kwa hiyo safisheni nyendo zenu na safisheni mavazi yenu, hadi mtakapokua kama baka mionganoni mwa watu.Mwenyezi Mungu hapendi maneno au matendo tupu, au fanyeni mambo machafu ya kimataifa." (Tizama , Abu Dawud, Libas, 70)

**KUFIKA KWA MPENDWA WENU
INATAKIWA IWE KAMA KARAMU.
KUMBUKA KUA MUISLAM NI MTU
ANAYETOA FURAHA NA RAHA KWA
WANAOMZUNGUKA.**



Ndugu wana majukumu kwa kila mmoja! Ndugu wana haki kwa kila mmoja!

- ✿ Ndugu hukimbilia kwenye msaada wa ndugu yake, huona mahitaji yake; kwa yoyote anayeyajali mahitajio ya ndugu yake katika maisha haya zitakua kwa Mwenyezi Mungu, utukufu juu yake, na kujali mahitajio yake akhera (Bukhari, Mazalim, 3)
- ✿ Ndugu hayaweki wazi aibu ya ndugu yake. Yoyote atakayeficha aibu ya ndugu yake katika maisha haya, utukufu wa Mwenyezi Mungu juu yake, ataficha aibu yake akhera (Muslim, Birr, 58)

Hasan Basri -(rehma ya Mwenyezi Mungu iwe uu yake) aliwahi kujiliwa na mtu na kuambiwa,

"Nilikwenda kwenye nyumba ya mtu huyu na huyu na amesema maneno ya uvumi kuhusu wewe."

"Kwanini umeenda kwanza katika nyumba?" aliuliza Hasan Basri.

"Nilialikwa pale kwa ajili ya chakula." Alijibu.

"Ni kitu gani alichokuandalia wewe?"

"Vitu vingi tu.....supu, nyama za kukaanga, vitu vitamu,maziwa..."

Kwa majibu, Hasan Basri alisema:

"Ulikua unaweza kuviweka vitu vyote ulivyovisema katika tumbo lako na usin-geweza kuhifadhi maneno yako?"

JE, HATUWEZI KUONA UPANDE WA MAZURI KWA NDUGU YAKO?

- ✿ Waislam wanatafuta kuunga udugu, sio kuuharibu. Hawasengenyi wala hawaenezi maneno ya uongo.
- ✿ Waumini wanatembeleana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, utukufu juu yake, katika nyakati nzuri na mbaya.
- ✿ Ndugu wa kiislam mar azote huombeana mazuri baina yao.
- ✿ Wanaonyesha mapenzi yao miongoni mwao.
- ✿ Ikiwa muumini atamwambia mwenzio makossa yake, huongea na ngudu yake kwa nia njema na katika mazingira ya usiri. Anakua mithili ya kioo kinachoakisi kwake yeze ni nani.
- ✿ Ndugu pia hupenda na huheshimu wapendwa wa ndugu yake.
- ✿ Ndugu hawatakiwi abadani kuchukiana na kuoneana wivu kati yao. Hawatakiwi kuent-delea kutoongea kwa Zaidi ya siku tatu.
- ✿ Ndugu hawadharauliani kati yao.
- ✿ Ndugu huwaombea ndugu zake waliotumbukia katika lindi la madhambi. Hujaribu kuwasaidia na kuwapa mkono wa msaada ili kutoka katika lindi hilo.
- ✿ Ili kuonyesha kuheshimiana, rehema na huruma kwa wengine, waislam ni kama viungo vya mwili mmoja. Ikiwa kiungo ki-moja kimeumia, inanyong'onyesha viungo vingine katika mwili. Mfano, kipindi jino lin-auma tunanyanya mkono kwenye shavu ili kulifariji. Miguu yetu inabeba mwili wote kwa daktari wa meno, ili tu kulifanya jino linalouma kupata tiba. Macho yanachangia maumivu yake kwa kukosa usingizi na kukaa macho. Mwili wote unajishirikisha kuponya maumivu ya jino moja. Haijalishi ni umbali gani wa kijeografia uliokuwepo kati yao,waislam wote ni kama viungo vya mwili mmoja.



Udugu ulioje!



Daktari kijana ambaye alikua amehitimu hivi karibuni katika chuo cha udaktari, alikwenda kliniki na kuanza majukumu yake ya mwanzo katika mji mdogo kiasi ndani ya Konya vijijini. Katika usiku wake wa kwanza, alijipumzisha katika nyumba ya mtu mmoja. Nyumba ilikua kari-bu kabisa na kituo cha garimoshi(treni). Baada ya chakula cha jioni alijumuika katika joto, mazungumzo ya kawaida na mwenyeji wake. Lakini daktari kijana alikua amechoka kutokana na safari ndefu na pia kutokana kujaribu kubabiana na hali ya ugeni wa mazingira. Muda ulikua umekwenda sana na bila shaka alikua anajitahidi kuupata usingizi mzito. Lakini alikua anaona aibu kumwambia mwenyeji wake jinsi gani alikua na usingizi. Muda mfupi baadaye, saa zinakwenda bila kuona maandalizi yoyote ya kulala.

Daktari kijana kwa uoga akamuuliza mkuu wa nyumba:

- ✿ "Hua mnalala muda gani hapa?"
- ✿ "Tunasubiria treni ya mwisho" alijibu bwana yule. "inatakiwa kuingia muda huu."
- ✿ "Mnamsubiria mtu mnayemjua?" aliuliza bwana mdogo. Jibu lilimuacha kwenye mshangao.
- ✿ "Hapana, kijana...hakuna yoyote tunayemjua anayekuja na treni. Ni kwa sababu tunaishi mji wa ndani sana na yawezekana kuna mgeni anayeweza kuja na treni. Na asipoona mwanga wa nyumba yoyote anaweza kuishia kulala mtaani.. tunasubiria ikitokea kunammoja yupo katika hali hiyo, ili tumchukue kama mgeni wetu."



HADITHI YA TENDO

Vita ya Yarmuk ilikua ni vita kali amba-yo ilipima uvumilivu wa maswahaba wote. Walikuwepo tu watu 46,000, wakikabiliana na jeshi gumu la kibyzantine la watu 240,000. Nyoyo zao zilikua zimejaa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, walipambana kwa umakini sana. Chini ya kamanda Khalid ibn Walid, aliyetukuzwa na Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) mwenyewe, walipata ushindi wa ghafla. Walipata mashahidi 3000 na kuua wabyzantine 100,000. Ushindi ulikua bila shaka hadithi ya tendo kubwa la kishujaa na kujitooa kuwahi kutokea katika historia.

Vita ilikua inakaribia mwisho. Uwanja wote wa vita, ulikua unanguza kwa jua kali sana la mchana, paligubikwa na vumbi la kutupa. Wakiwa wanapambana kwa masaa hadi mwisho, waislam mashujaa walikua wamebeba mikuki, mishale na majeraha ya mapanga. Hawakupata hata wasaa wa kunywa maji ya uvuguvugu wa jua kutoka katika chupa zao. Midomo ilikua inaomba tone la maji, mmoja baada ya mwingine, kinywaji cha uponyaji kwa waliokufa mashahidi ambako wangeweza kupoa milele, wakigumia maneno ya tawhid kwa ndimi zao kavu. Hudhaifa(Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) alisimulia matukio haya ya kujitoo yaliyofanywa na watu kutoa mapenzi yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, utukufu juu yake, na furaha ya milele kwa watu:

"Nilikuwa nimejeruhiwa na nimechoka. Katika kilichobaki kwenye nguvu zangu, nilinyanya na kwenda kumtizama binamu yangu Harith. Nilikuwa ninatembea kwa ndugu zangu waliolala kukatisha uwanja wa vita, wakiwa katika hatua za mwisho za uhai wao, wakigumia majeraha yao. Baadaye kidogo nilimuona. Alikuwa na majeraha mengi. Nilimuinamia, nikiwa na chupa ya maji mkononi mwangu.

Hakuwa na nguvu hata kidogo iliyobaki ya kuzungumza. Lakini alikuwa anajaribu kuni-

eleza kitu flani kwa macho yake. Niliharakisha kufungua kifuniko cha chupa na kumpatia, ili kuunganisha midomo yake iliyopasuka na maji ambayo alikuwa ameyasubiria kwa muda mrefu, nilisikia sauti ya ndugu yangu Iqrinah, akiwa amelala majeruhi katika ardhi karibu kabisa na pale tulipokua.

"Maji! Maji! Tafadhali....tone la maji" alikuwa anaguna. Matokeo ya kusikia sauti ya Iqrinah, binamu yangu alinipa ishara kwa macho yake, kuchukua chupa ya maji badala yake.

Haraka nikaenda kwa Iqrinah aliye kua ameuacha mwili wake, umejeruhiwa na yuko na vidonda mbalimbali vyta mapanga na miki-katika mchanga wa moto. Nikaweka chupa yangu katika midomo yake. alisita kuendelea kunywa funda lake la kwanza. Ilikua ni baada ya kusikia sauti ya ndugu yetu Ilyas, sio mbali kutoka tulipokuwepo.

Tone moja la maji tafadhali.....kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu! Alikua anagugumia.

Kabla hata maji ya uvuguvugu hayajagua-sa midomo yake, Iqrinah alinirudishia chupa; na kugeuzia kichwa chake uelekeo aliokuwepo Ilyas, akinashiria nimpelekee maji yeye. Hakuweza kustahili japo tone moja la maji ndugu yake Ilyas alikuwa akiyahitajia kwa kugumia.

Nilipokimbilia kwa Ilyas, nilikuta anavuta pumzi yake ya mwisho, akisema maneno ya tawhid. Mola wake alikuwa amemchukua Ilyas katika rehma ya milele, akimruhusu kugumia chemchem ya peponi kabla hata hajalowanisha midomo yake mikavu kwa maji ambayo Iqrinah alimuachia yeye. Mara moja nikarudi tena kwa Iqrinah, nikidhani natakiwa angalau kumpatia maji. Lakini, muda amba-o ninawasilii karibu yake, yeye pia alikuwa anakunywa kinywaji cha peponi walichoandaliiwa mashahidi. Harith alikuwa bado yuko hai angalau, hivyo nikakimbia kwake mara hii. Lakini kama wengine, Harith alikuwa katika hali ya kutohitaji maji tena.

KUONYESHA HESHIMA KWA WAKUBWA

Mtu ni kiumbe aliyetunukiwa na kuheshimiwa.

Kwa maarifa na uzoefu, wazee wanaujuzi mkubwa kulinganisha na watoto na vijana wadogo. Wanastahiki tunu na heshima kuliko mtu yoyote yule. Kwahiyo katika utamaduni wa kiswahili, vijana wadogo ni lazima wawaheshimu

wakubwa zao, wawape kipaumbele, na kuwasaidia majukumu yao. Wazee pia wawahudumikie wadogo kwa mapenzi, huruma na uelewa. Kwa namna hii mshikamano wa upendona heshima utatokea baina ya wadogo na wakubwa. Hii inajenga mazingira ya Amani katika jamii ya kiislam.



Jinsi gani tunaonyesha heshima kwa wakubwa wetu?

- ✓ Katika mazingira ya kukaa, tunapomuona mzee ameingia ndani, tunasimama na kama itahitajika, kumuonyesha sehemu ya kukaa; na kumsubiria yeye kukaa kwanza.
- ✓ Ikiwa mkubwa huyo ana umri mkubwa au elimu kubwa sana, tunaonyesha heshima kwa kumbusu mikono.
- ✓ Tunajua kuwa kipaumbele cha kuongea mara zote kinakua ni kwa watu wazima. Tunaweza kuongea endapo wamemaliza kuongea au tunaomba ruhusa ya kuongea.

Ibn Umar (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) alisimulia:

Niliku bado mdogo wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) alipoulima kundi la watu wazima kumzunguka yeye kuwaambia wataje jina la mtu ambao unafanana na sifa za muislam; mtu ambao unatoa matunda na unakua wa kijani muda wote."

Hakuna aliyekuwepo pale kusema jina la mtu ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alikua anaufikiria. Nikawaza akilini mwangu kua "Huu lazima utakua mtende"; lakini kwa kuwa niliku na maswahaba kama Abu Bakr na Umar (Mwenyezi Mungu awe radhi nao) nikaona hatikua sahihi kusema pendekezo langu. Muda baadaye, Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) akathibitisha kile kilichokuwepo katika akili yangu. "Ni mtende", alisema.

Kisha baada ya kuondoka katika mkusanyiko nikiwa na baba yangu, nikamwambia baba yangu kua jina la mtu lililokuja kwangu pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na Amani ziwe juu yake) alipoulima swali.

"Kwanini sasa hukusema?" baba yangu ali-niuliza. "Ingenifanya niwe na furaha sana kwa wewe kutoa jibu sahihi!"

"Niliona nyie wote mmeekaa kimya," Nilimjibu. Niliona ni sahihi zaidi ikiwa nitakua kimya pia, (Pindi ambapo ningeweza kuongea ambapo hakuna mmoja katika yao angeweza kufikiria jibu)". (See, Bukhari, Ilm, 4 Adab, 79)

- ✿ Hatutakiwi kupaza sauti zetu tunapokua tunagea na wakubwa. Tunashika akili zetu ili tusifanye mambo katika namna ya kuskosa haya.
- ✿ Hatutakiwi kuonyesha ujeuri kwa ishara na mikono.
- ✿ Tunapokula na watu wazima,tunasubiria wao waanzee kwanza.
- ✿ Tunapokua tunatembea nao njiani, hatutakiwi kutembea mbele yao, aidha nyuma kidogo kuliko wao au kushotoni mwao.
- ✿ Tukiwaona wamebeba mizigo mizito mikononi mwao, tunawasakiidha kuibeba.
- ✿ Tunakimbia kuwasaidia muda na kwa msaada wowote watakaohitaji kwetu.
- ✿ Katika usafiri wa magari ya umma, tunajitolea viti vyetu kwao, ikiwa hawawezi kupa viti vilivyo wazi vya kukaa.
- ✿ Wanapotoka katika mikutano, tunanyanya ka tukiwaona milangoni.

Siku moja Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikua amekaa na maswahaba zake. Kuliani kwake alikuwepo Abu Bakr na Umar (Mwenyezi Mungu awe radhi nao). Kisha ghafla, Abbas (Mwenyezi Mungu awe radhi naye), mjomba wa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), akafika. Abu Bakr akampisha Abbas, Abbas akakaa baina ya Mtume na Abu Bakr. Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kisha akasema:

"Ni wale tu wenyewe adabu na kuandaliwa wanajua thamani ya adabu na fahari ya watu."

Alipokua anaongea na mjomba wake, Mtukufu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake) alishusha sauti yake chini sana kiasi kwamba Abu Bakri akamwambia Umar:

"Kuna kitu kimetokea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu....inaonyesha kua atakua amepoteza sauti yake, ananifanya nipate hofu." Hatimaye Abbas aliondoka baadaye, ambapo Abu Bakr akamuuliza Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake):

"Ulikua haujisikii vizuri mwanzoni,ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?"

"Hapana," alijibu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake).

"Ilinifanya nipate hofu kukusikia umeshusha sauti yako sana....." kisha Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) akaelezea:

"Kama ambavyo Malaika Jibrir alivyowa-husia kushusha sauti zenu kwangu, amenishauri kushusha sauti yangu kwa mjomba wangu." (Ali al-Muttaqi, Kanzu'l-Ummal, V. XIII, 514/37321)


HII NI HESHIMA!

Mtukufu Mtume (S.a.w) alikua akisikiliza kila mmoja nje hadi watakapomiliza kuongea. Alikua haingilii mazungumzo ya mtu yoyote. kwa wale walionyoosha mikono yao kusalimiana, alikua akiutoa mkono wake na hakurudisha hadi yule mtu arudishe wa kwake kwanza. Kwa kipindi chote cha mazungumzo yao, Mtukufu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake) aliwasikiliza kwa kuwatazama moja kwa moja katika nyuso zao na hakugeuza macho yake popote hadi mtu yule afanye hivyo kwanza. (Tirmidhi, Qiyamah, 46)

Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) alikua na furaha mara zote kuwaona vijana wadogo wakiwasaidia watu wazima kwa heshima. Alikua anasema: "**Mwenyezi Mungu Mtukufu ambariki kijana mdogo anayemuheshimu mtu mzima kutokeana na umri wake, kwa watu kumsaidia yeye atakapokua mzeege**".

(Tirmidhi, Birr, 75)

Siku moja maswahaba Abdullah na Muhyayisa walikwenda katika mji wa Khaibar. Walikuwa wanakwenda kuonana na rafiki yao huko. Pindi rafiki yao aliposhindwa kutokea katika eneo walilokubaliana, walipata mashaka na kwenda kumtafuta. Baadaye kidogo



Walimkuta amekufa katika shimo, akiwa katika dimbwii la damu. Walifadhaika sana, walirudi Madina. pindi Abdurrahman, ndugu wa Abdullah alipopata habari kitu gani kilichotokea, alimchukua Muhayyisa pamoja na ndugu yake Huwayyisa kwa Mtukufu Mtume (rehma na Amani ziwe juu yake), kisha kijana Abdurrahman alianza kuelezea tukio lile kwa mshituko kwa sauti ya juu, bila ya kumruhusu mtu yoyote kuongea; wakati kwa uhalisia Muhayyisa hakua mtu pekee katika tukio lakini pia alikua ni mkubwa kuliko yeye, alikua upande wake wa kulia.

Hakuvutiwa na mtazamo wa Abdurrahman, Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alimkanya kwa maneno haya, "Acha mazungumzo kwa wakubwa zako....acha mazungumzo kwa wakubwa zako." (Bukhari, Jizya, 12) Kutokea hapo Abdurrahman akanyamaza na kuacha maelezo kwa wakubwa zake.

Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikua anapenda kuzungumza kwa sauti ya wastani na kidogo kidogo, neno kwa neno. Hakuwahi kuongea kwa sauti ya juu, kama ana-muungelesha mtu kiziwi au yupo katika mabishano. Alikua akitoa mfano bora kwenye adabu ya mazungumzo kwa wajukuu zake na watoto wen-gine. Alikua anawashauri waongee katika sauti laini, wakiwa wanaongea na wakubwa na wado-go. Kama mfano, alikua akitoa ushauri amabo Luqman (Amani iwe juu yake) aliompa mwanae: "Na uwe kati na kati katika mwendo wako, na shusha sauti yako, hakika sauti mbaya bila shaka ni sauti ya punda." (Luqman, 31; 19)

Mtukufu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alitamani watu wote kuonyesha heshima. Kama aliviyotamani kwa wadogo kuheshimu wakubwa, alikua akitamani wakubwa kuthamini na kuwapenda wadogo kwao. Alikua akisema: "yule ambaye hawathamini na kuwapenda wadogo kwake na hawatunuku na kuwaheshimu wakubwa kwake si katika sisi." (Tirmidhi, Birr, 15)

IKIWA TU WAMECHUKUA SOMO

Murad II sultani mkubwa wa Ottoman, anakumbuka moja ya uzoefu wake:

Tulipata maradhi katika uwanja wa vita Varna. Baadaye, nilizunguka katika uwanja, kukagua askari wanaodhaniwa waliouwawa na maradhi. Kitu kimoja nilichogundua kua wengi wao walikua vijana.

Kumgeukia bwana Azap, kiongozi mzoefu wa vita wa nchi.

Nilitoa maoni, "Takribani hakuna hata mtu mmoja mzee katika rundo la watu waliokufa, Azap....hakuna hata mtu

mmoja mwenye nywele ya kijivu..... unazungumziale?

Bwana Azap alielewa kitu gani nilikuwa ninamaanisha kisha akatabasamu. Baada ya kimya cha muda mfupi akasema,

 Wasingeweza kuthubutu kukabiliana na jeshi lenye nguvu na hamasa na kuijendesha wenyewe kwenye majanga, ikiwa wangekua na wazee wa kutosha wa kuongea nao vitu vyaa maana.....

 Labda wazee wao wote walishapata somo kuwa babu yenu Bayazid aliwapa katika uwanja wa vita.....zaidi ya yote wakahofia kuwarudisha nyuma! (kumbuka ushindi wa Nigbolu miaka arobaini na nane iliyopita)



ADABU YA KUINGIA NA KUTOKA NYUMBANI

Nyumba ya furaha

Majumba ni mahali ambapo kila mtu anaishi kwa furaha na starehe. Vizuri au vibaya, sehemu ambayo tunajihisi na kustarehe zaidi ni majumbani mwetu. Watu wako huru wakiwa nyumbani, wanakula, wanakunywa, wanatembea tembea, wanapumzika na kulala popote panapowaridhisha. Kwa muda, wanakua na vitu vyao binafsi ambavyo hawataki mtu yoyote kuviona. Kwahiyio kuna kanuni ambazo tunatakiwa kuzizingatia tunapoingia au kutoka nyumbani, kuwa wenyewe, kwa marafiki zetu na kwa mtu mwingine yoyote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na msipomkuta mtu humo ndani basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa: Rudini! Basi rudini. Hivi ni usafi Zaidi kwenu. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda.

(an-Nur, 24; 28)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mlaoamini! Msiingie nyumba zisizo zenu mpaka mwombe ruhusa, na muwatolee salam wenyewe. Hayo ni bora Kwenu mpate kukumbuka."

(an-Nur, 24; 27)



Mtukufu Mtume wetu anasema:

"takeni ruhusa mara tatu: mkiruhusiwa ingieni na msiporuhusiwa rudini mlipotoka."

(Bukhari, Istidhan, 13)



Kitu gani tunatakiwa kukizingatia tunapoingia au kutoka katika nyumba:

- ✿ Tunapoingia ndani ya nyumba, tunahitaji kugonga mlango na kuomba ruhusa, hata kama nyumba ni zetu.
- ✿ Tukiwa tunataka kuingia katika nyumba ziszokua zetu, tunahitaji kugonga mlango si zidi ya mara tatu.
- ✿ Tukiwa tunasubiri ruhusa ya kuingia mbele ya milango, tunageukia kidogo kwa pembeni, ili kwamba mlango utakapofunguliwa tusione mara moja kile kilichopo ndani.
- ✿ Au kuulizwa "Wewe ni nani?" Tunatakiwa kujibu kwa ufasaha majina yetu, ikiwa inahitajika na ubini wetu.
- ✿ Ikiwa mlango umeshafunguliwa, tunatakiwa kusema "Assalam alaykum" au kuomba ridhaa ya kuingia kabla hatujaingia ndani.
- ✿ Endapo ni nyumba zetu au nyumba za watu wengine, tunatakiwa kuingia ndani ya kwa bashasha na kuwa na maneno mazuri ya kuongea.
- ✿ Tukiwa tunaondoka tujitahidi kuaga wale tunaocha nyuma, kuongeza dua njema na kuwatakia ulinzi wa Mwenyezi Mungu.



NI LAZIMA KUOMBA RUHUSA

Akiwa na miaka nane, mama yake alimuacha Annas Ibn Malik(Mwenyezi Mungu awe radhi naye) akiwa na Mtukufu Mtume(rehma na Amani ziwe juu yake) ili kwamba kijana amhudumikie Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) hadi katika umri wa miaka ishirini. Akipata mafunzo maalumu toka kwa Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) hadi alipokua na miaka ishirini. Anas aliendelea kuishi miaka sabini baada ya Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) kufariki dunia. Akimpenda Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) sana kiasi kwamba hakuwahi kumtoa akilini mwake. Anas (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) alikuu akisema:

"Hakuna usiku ambao sijawahi kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu(S.a.w) katika ndoto zangu. Inshaallah, nikikutana naye tena akhera nitamwambia, "Tizama, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu....mtumishi wako mdogo Anas amekuja na kukuomba uombezi wake."

Anas(Mwenyezi Mungu awe radhi naye) alipitia katika moja ya hekima safi kabisa aliyojifunza kutoka kwa Mtukufu Mtume (S.a.w)-:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu aliniambia, "toa salamu zako kwa familia yako, mpendwa wangu, unapoingia nyumbani ili kwamba salamu yako itumike kama Baraka kwako na kwa familia yako.' (Tirmidhi, Istidhan, 10)

Mara moja mtu alikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na amani ziwe juu yake) na kumuuliza: "Ninatakiwa kuomba ruhusa hata kwa mama yangu ninapotaka kuingia nyumbani?"

"Ndio", alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani ziwe juu yake)-.

"Lakini ninaishi naye," alisema yule bwana-

"Ni lazima bado umuombe ruhusa, alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani ziwe juu yake).

"Ni lazima bado uombe.....je, utapenda kumuona uchi?" aliuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu(rehma na amani ziwe juu yake)-.

"Hapana!"

"Kwa namna hiyo omba ruhusa kabla hujalingia.' (Muwatta, Istidhan, 1)

Vitu gani hatutakiwi kufanya tukiwa tunaingia au kutoka katika nyumba:

- ✓ Mtu hatakiwi kuchungulia kupitia tobo la funguo, au dirisha au sehemu nyingine yoyote kabla ya kuingia ndani.
- ✓ Ukiwa katika nyumba ya mtu mwagine, hatutakiwi kuingilia vitu visiviyotuhusu au kupitia kitu chochote bila ruhusa ya mwenye nyumba.
- ✓ Hatutakiwi kutizama tizama vitu na samani za ndani ya nyumba kama unataka kununua-.
- ✓ Hatutakiwi kujaribu kutaka kujua muono wa watu katika vyumba vingine toka pale ulipokaa wewe.
- ✓ Hatutakiwi kusikiliza mazungumzo ya watu wa vyumba vingine.
- ✓ Baada ya kugonga mlango na kuomba ruhusa ya kuingia, hatutakiwi kuingia kwa nguvu kabla ruhusa hajiatolewa.
- ✓ Katika hali ya dharura inayotutaka kuondoka mara moja, tunamtaarifu mwenye nyumba, hata kama ikiwa kwa maandishi.

Sahl Ibn Saad (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) anaelezea:

"Bwana mmoja alikua anajaribu kuchungulia ndani kwa Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) kupitia kitobo cha mlango. Wakati huo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani ziwe juu yake) alikua na chanuo katika mkono wake. Akatambua tabia mbaya ya bwana yule, akasema,



Mtukufu Mtume wetu anasema:

"Ikiwa ninajua unanipeleleza kwa nia mbaya, ningeyatoboa macho yako na chanuo hili.omba ruhusa kabla hujaingia ndani imeamrishwa ili kuhakikisha kua aliyeuwepo ndani amelindwa kutokana na kuonekana."

(Muslim, Adab, 40, 41)



ADABU YA KUPOKEA NA KUTOA ZAWADI

Kupeana zawadi kunaimarisha mshikamano wa mapenzi.

Zawadi ni vitu tunavyovitoa kwa wapendwa wetu bila kutarajia chochote kwa mrejesho. Kutoa zawadi kunasaidia kuondoa ubinafsi, ubahili na maradhi ya vivu mbaya. Kupokea zawadi, kwa namna yake, kunaamsha hisia za huruma na wema, kama sukari kiasi kudondokea katika kikombe cha maji. Inafuta hali ya chuki na kua na moyo mgumu baina ya mtoaji na mpokeaji.


Mtukufu Mtume (rehma na amani ziwe juu yake) ametuhabarisha namna gani kupeana zawadi kunasaidia kuwaleta pamoja waumini na kuimarisha mshikamano wao wa mapenzi:

"Peaneni zawadi kati yenu; kwa zawadi inafuta dhana ya kumdhuru mwenzako na chukikutoka katika nyoyo. Basi mwanamke yoyote asiione ndogo zawadi anayoitao kwa majirani zake wanawake, hata kama ni kipande cha nyama ya kondoo."

(Tirmidhi, Wala, 6)

"Mpe zawadi aliyekupa zawadi wewe. Kama hauna uwezo wa kupta chochote, basi angalau muombee dua ili kwamba ile zawadi isibaki bila kurejeshwa." (Nasai)

**HAITAKUA VIZURI KUACHA TENDO ZURI
BILA MREJESHO, NI KWELI?**



Kipi tunatakiwa kuzingatia tunapokua tunatoa zawadi?

- ✓ Zawadi inatakiwa itolewe na kupokelewa kwa nia ya kutimiza Sunnah ya Mtukufu Mtume(rehma na amani ziwe juu yake), na kitendo cha ibada.
- ✓ Mtu asiangalie thamani ya kitu, ubora au ukubwa wa zawadi. Kilichokua cha muhimu katika kutoa na kupokea zawadi ni sehemu ya thamani baina ya watu wawili juu ya mwingine na mapenzi baina yao.
- ✓ Tunapokua tunatoa zawadi, ikiwa ni matamano ya kujionyesha au kutarajia

Pia ni Sunnah ya Mtukufu Mtume (rehma na amani ziwe juu yake) kutoa zawadi za vitu vyake binafsi kwa watu ambaeo hutokea kuvipenda.

"Siku moja mwanamke alimleta joho alilolifuma kwa mikono yake mwenyewe kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani ziwe juu yake) kama zawadi. Akasema::

"Nimelifuma hili joho kwa mikono yangu mwenyewe ili ulivae, Mtume wa Mwenyezi Mungu.'

Akihitajia joho la namna hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa upendo kabisa alipokea zawadi hii, akalivaa kisha akaja kwetu. Yupo mmoja alipomuona akasema, "Joho zuri kiasi gani hili....una-weza kunipatia?"

Kweli" alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani ziwe juu yake), baada ya

Kuketi kwa muda, kisha akarudi nyumbani, kisha akalikunja vizuri kabisa joho, akamtumia bwana yule kama zawadi." (Bukhari, Libas, 18)

UNASEMA NINI? TUNAWEZA KUTOA KALAMU AU KITABU TUNACHOKISOMA KAMA ZAWADI, KWA RAFIKI AMBAYE ATAONEKANA KUKIPENDA?

upendeleo badala yake tafuta nafasi njia katika moyo, zawadi itapoteza thamani. Zawadi haitoi hisia za mapenzi, huruma na udugu.

- ✓ Zawadi haitakiwi kuwa nje ya bajeti ya mtu;kwa kukumbuka na kukumbukwa ni kitu cha muhimu, sio thamani ya kidunia ya zawadi.
- ✓ Ikiwezekana, tunatakiwa kununua au kuandaa zawadi zetu kwa vitu vyetu.
- ✓ Wale wanaostahili zaidi zawadi zetu ni wanafamilia, ndugu zetu, marafiki zetu na majirani zetu, lakini Zaidi kuliko wote ni mama zetu wapendwa, waliyofanya mambo makubwa kuliko mtu yoyote yule.
- ✓ Tunatakiwa kuzifunga zawadi zetu katika namna bora kabisa na kuzitoa katika



kwa tabasamu na maneno mazuri nay a kiungwana.

Ni aina gani za zawadi ambazo hazikubaliki?

- ✓ Vitu ambavyo ni vyta haramu au haviruhusiwi katika uislam haviwezi kutolewa na kukubalika kama zawadi.
- ✓ Vitu ambavyo vinatisha au kufadhaisha mtu havitakiwi kutolewa kama zawadi.
- ✓ Ikiwa zawadi inatolewa kwa ajili ya rushwa au kwa sababu ya kusababisha kutotendeka kwa haki, ambazo zinakataliwa na uislam, basi zawadi hiyo haiwezi kukubalika.



SHATI MOJA

Mtukufu Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alikua anapenda kutoa zawadi kwa vitu anavyovimiliki. Ikiwa mtu atataka kitu kutoka kwake, alikua akihisi ni wajibu kumpa. Kulikua na nyakati alikua akitoa chakula cha mwisho kabisa alichokuwa nacho au nguo pekee aliokua nayo.

Kwa kweli, siku moja mtoto alikuja kwake na kusema, "mama yangu anataka shati kutoka kwako."

Mtukufu Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alikua na shati moja alilolivaa na hakua na jingine la kuvaad.

"Nitakupa shati....lakini njoo baadaye kidogo," alisema kumwambia mtoto.

Mtoto aliondoka na kurudi muda mfupi baadaye.


"Mama yangu anahitajia sana shati lolote utakaloweza kumpatia," alisema. Kutoka hapo Mtukufu Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) ailingia ndani katika chumba chake. Alilivua shati alilokua amelivaa na kumpatia yule mtoto. Swahaba aliyewasili msikitini muda mfupi baadaye, alikuta kua Mtukufu Mtume(rehma na amani ziwe juu yake) ametoa shati la pekee alilokua nalo na hakuweza kwenda msikitini kwa ajili ya swala. Haraka sana wakampatia shati Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w)-.

Kwa ukarimu wake wa kipekee usiopimika, Mtukufu Mtume (rehma na amani ziwe juu yake) alikua ni mfano bora sana kwa watu wote.

MAJIBU

MUONGOZO WETU KATIKA MAISHA: IMANI KATIKA VITABU VYA MWENYEZI MUNGU

Fumbo (Uk. 33)



Tafuta Majibu Yanayoendana (Uk. 34)

1	Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha ujumbe wake kwa mitume wake.	5	Kimetufikia sisi katika uhalisia wake bila mabadiliko.
2	Toka zama za nabii Adam(Amani iwe juu yake) mitume wametuletea	6	Maamrisho na makatazo ya Mola wetu Mtukufu.
3	Tunafuata amri katika vitabu hivi na,	8	Uzuri na ukweli wa vitabu vyote vilivytangulia.
4	Kwa kuzingatia mahitaji ya binadam Mola wetu mtukufu ametuma.	7	Watu walipoanza kuhamia katika Imani isiyokua sahihi.
5	Tunaamini kuwa Quran Tukufu ni	1	Moja kwa moja au kwakupitia malaika wake
6	Vitabu vitukufu vinatuambia	3	Kujaribu kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.
7	Ni lini nakala halisi za vitabu vitukufu vilingia hitilafu,	2	Maneno na ujumbe wa Mwenyezi Mungu.
8	Quran Tukufu inajumuisha	4	Kwa baadhi ya mitume wake vitabu vidogo vilivyoitwa suhuf.

Tujipime wenyewe (Uk. 34)


1- c 2- c 3- a 4- a 5- d 6- b

Jaza nafasi zilizoachwa wazi (Uk. 35)

- | | |
|-------------------------|--|
| 1. Injili, Nuru | 4. Kidogo kidogo |
| 2. Mkumbushaji, Mlinzi. | 5. Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Njia iliyonyooka |
| 3. Kitabu, Taurat. | 6. Yaliyomo, Shada |

WATU WA MFANO: IMANI KATIKA MITUME

FUMBO (Uk. 63)



Tafuta Maneno Yanayowiana Kwa Usahihi (Uk. 64)

1	Kuwapinga mitume	4	Upweke wa Mwenyezi Mungu na kumuabudu yeze peke yake.
2	Mitume walikua na jukumu la kupeleka dini ya Mwenyezi Mungu kwa watu	7	Mitume waliotangulia kwa upendo na heshima.
3	Japokua walipitia katika mateso na ugumu wa hali ya juu	6	Ni alama ya huruma ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake
4	Mitume wote waliwaita watu wao kuamini	8	Kuhusu kuwasamehe wale waliotudhuru na kulipizia ubaya kwa wema.
5	Mola wetu mtukufu alituma mitume wake	2	Na kuishi kwa mujibu wa kanuni zake
6	Kumsamehe Adam baada ya kula katika mti uliokatazwa	5	Kua kigezo chetu
7	Kipenzi chetu bwana Mtume alikua anakumbuka	3	Mitume hawakurudi myuma katika kuyaende majukumu yao.
8	Nabii Yusuf ni mfano mzuri kwetu	1	Inamaanisha kuipinga dini.

Tujipime Wenyewe (Uk. 65)

1- c 2- a 3- b 4- b 5- a

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi

- | | |
|------------------------------|-------------------|
| 1. Viongozi/amri yetu | 4. Somo/uelewa |
| 2. Habari njema/ombi | 5. Sala/ninafanya |
| 3. Mimi ni mfano bora kabisa | |

MSIMU WA HURUMA NA IBADA: RAMADHANI NA KUFUNGA

Tupime Uelewa Wetu (Uk.93)

1- NDIO 2- HAPANA 3- NDIO 4- HAPANA 5- HAPANA 6-HAPANA 7- HAPANA 8- NDIO

Tupime Uelewa Wetu (Uk.163)

1- a 2-b 3-c 4- a 5- b 6- c 7- d 8- b 9- a

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi (Uk164)

1- Huruma, Kusamehewa madhambi 2- Afya 3- Sitini na moja 4- Qadha
5- Nadhiri 6- Cheo,samehe 7- Rayyan

DARAJA KATI YA MATAJIRI NA MASIKINI: ZAKAT

Tupime Uelewa Wetu (UK.123)

- Wale wanaomiliki mali kiwango cha nisab wanachukuliwa kama matajiri kwa mujibu wa dini.
- Tunatoa robo ya dhahabu na fedha kwa maneno mwengine 2.5% ya mali kama zaka.
- Mtu hawezi kutoa zaka kwa mjukuu wake.
- Tunapokua tunatoa zaka Hatutakiwi kusahau kwamba tunatekeleza jambo la ibada.
- Kwa taasisi kama misikiti,shule na hospitali na kwa wahandisi wa barabara, visima na madaraja.
- Zaka inahudumia daraja ambalo linabeba vitu vya matajiri kwa masikini.
- Mchango wa muislam tajiri katika baadhi nya mali zake, kwa wapokeaji ambao dini yetu imeamrisha inaitwa "zakat."
- Mkono unaotoa, ni mbora zaidi kuliko mkono unaopokea.
- Kiwango cha nisab kwa dhahabu ni gram 80.18 .
- Kiwango cha chini cha sadaka ya Eid Al-Fitr ni Milo miwili ya mtu mwenye kipato cha kati au kiasi cha fedha kinacholingana nacho.

Tupime Uelewa Wetu (Uk. 123)

1- d 2- a 3- c 4- a 5- b 6- d 7- c 8- d

Jaza Nafasi Zilizoachwa Wazi (Uk. 124)


1- Haombi ombi 2- Katika mali 3- Mbegu 4- Moyo wako 5- Hutakasa

NINAJIFUNZA SIRA YA MTUME WANGU: SIRA

Tujipime wenyewe (Uk. 166)

1- c	2- c	3- c	4- b	5- c
6- c	7- b	8- c	9- d	10- b
11- d	12- b	13- d	14- d	15- c
16- c	17- d	18- c	19- c	20- d

Fumbo (UK. 169)






FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT
1550 BOOKS IN 59 LANGUAGES FOR FREE



Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org